# Nipashe

Ijumaa Novemba 22, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580082

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Waziri Mpango alia na Nida kuchelewa kwa vitambulisho

UKURASA 4


BUFE
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
UCHUMI
Alivyonusurika kutoka ndoa ya kitoto, akahamishiwa kuwa fundi cherehani
Mkulima aliyegeuka mafanikio ya kipekee kupitia kilimo cha mlimani
Biashara katika picha

UKURASA 13

# Udom yakiri rushwa ngono mbele ya JPM

**YASEMA** ni jinamizi linalowakabili, waandaa mpango kabambe kuitokomeza, Magufuli awapa salamu vibaraka... *Endelea ukurasa wa 2 & 3*



## ALIYEKATWA MIKONO ATAKIWA KULIPWA

UKURASA 2

Rais John Magufuli akitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**






## Korti yamtaka Tundu Lissu kufika mahakamani Des. 19

UKURASA 2


MICHEZO YONDANI, FEI TOTO WAITIBULIA YANGA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## Aliyekatwa mikono aamuriwa kulipwa

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imetakiwa kumlipa fidia, Mariam Staford (36) mwenye ualbino baada ya kukatwa mkono na watu wasiojulikana nyumbani kwake mkoani Kagera, Oktoba 17, 2008. Uamuzi huo umetolewa na Kamati ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRDP) Septemba 19, mwaka huu, baada ya Mariam kupeleka malalamiko.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Shirika la Under The Same Sun (UTSS), Berthasia Ladislaus, alisema Mariam alikuwa akiilalamikia Serikali ya Tanzania kutompa haki yake ya kimsingi ya ibara ya 5, 6, 8, 10, 14, 15(1), 16 na 17 za Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu ambako Tanzania ni nchi mwanachama wa mkataba huo tangu mwaka 2009.

Berthasia alisema waliohusika na tukio hilo walikamatwa na kufunguliwa mashtaka katika Mahakama Kuu kanda ya Kagera, hata hivyo waliachiwa huru kwa kutokuwa na ushahidi wa kujitosheleza.

Kufuatia kutoridhishwa na mwenendo huo, alisema Mariam aliamua kutafuta haki yake kwenye vyombo vya kimataifa na Juni 12, 2014 aliamua kupeleka malalamiko yake kwenye kamati hiyo.

"Baada ya shauri hili kupokolewa katika kamati, Serikali ya Tanzania ilipata fursa ya kutoa maelezo na kujieleza mbele ya kamati Juni 25, 2015, lakini ilikanusha uwapo wa uvunjifu wa vifungu hivyo na kueleza kuwa ulinzi wa watu wenye ualbino umeimarishwa," alisema.

Alifafanua kuwa baada ya kujitetea katika kamati, Mariam alipata fursa ya kuwasilisha maelezo kinzani dhidi ya serikali Agosti 25, 2016 na alitoa utetezi wake uliokuwa na maelezo tofauti na kinyume na maelezo hayo ya serikali ikiwa ni hoja binafsi.

Kwa nyakati tofauti, alisema kamati iliiomba Serikali ya Tanzania kuwasilisha maelezo kinzani dhidi ya maelezo ya mlalamikaji, na ilipofika Januari 16, 2018 serikali ilikiri kupokea maelezo ya mlalamikaji, hata hivyo, haikuwahi kuwasilisha maelezo mengine ya ziada katika kamati hiyo hadi hukumu inatolewa. "Kamati iliamua Serikali ya Tanzania impe fidia Mariam, igharamie matibabu yake, itoe visaidizi vitakavyomsaidia kuishi kwa kujitegemea, kufanya uchunguzi na upelelezi wa kina ili kuhakikisha wahalifu wote waliomdhuru Mariam wanasakwa na kuchukuliwa hatua," alisema Mkurugenzi huyo wa UTSS.

Alisema kamati imeagiza Serikali ya Tanzania kufanya marejeo ya mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuhakikisha haki za watu wenye ualbino zinalindwa ikiwamo usafirishaji wa viungo vya binadamu.

Lingine ni kuhakikisha kesi zote zilizoko mahakamani zinaisha na wahusika wanachukuliwa hatua, kuandaa programu za uelimishaji umma kuhusu hali ya ualbino.

"Kwa mujibu wa ibara ya 5 ya itifati ya mkataba huo, kanuni ya 75 ya kanuni za uendeshaji wa kamati, serikali inatakiwa kuwasilisha maelezo kwa kamati ndani ya miezi sita kuanzia Oktoba 15, mwaka huu juu ya hatua ilizozichukua kuhusu hukumu hii," alisema.

Hata hivyo, Mwanasheria wa UTSS, Maduhu Willium alisema hakuna kiasi maalum kinachopaswa kutolewa katika fidia, inapaswa kuendana na uhalisia wa madhara wa tukio.

Akizungumzia hukumu hiyo, Mariam alisema: "Nimefurahi kwa ushindi huu, ninachotaka ni utekelezaji wa maamuzi hayo".

# Udom yakiri rushwa ya ngono

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Dodoma (Udom) kimekiri mbele ya Rais John Magufuli kuwapo kwa dosari ya baadhi ya wahadhiri wake kuomba rushwa ikiwamo ya ngono kwa wanafunzi.

Kutokana na dosari hiyo, uongozi wa chuo hicho umeunda kamati ya maadili ili kudhibiti unyanyasaji wa kijinsia na kupambana na rushwa ya aina hiyo dhidi ya wanafunzi.

Hayo yalibainishwa jana na Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Faustine Bee, katika mahafali ya 10 ya chuo hicho ambayo Rais Magufuli alikuwa mgeni rasmi.

Alisema chuo hicho kinasifika kwa mambo mazuri yanayofanyika, lakini kumeibuka baadhi ya wafanyakazi wasio na maadili kujihusisha na unyanyasaji wa kijinsia.

Hata hivyo, Prof. Bee alisema dosari hiyo haiko tu chuoni kwake, bali hata vyuo vingine nchini. Hivi karibuni, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliunda kamati maalum kufuatilia madai ya kuwapo kwa tatizo hilo katika chuo kikuu hicho kikongwe zaidi nchini.

"Wafanyakazi wamekuwa wakiomba rushwa ya ngono au fedha kwa wanafunzi ili kuwafaulisha, hali kadhalika, wapo wanafunzi wanaowalazimisha wafanyakazi kuwapa rushwa ya ngono ili kufaulishwa masomo yao," Prof. Bee alisema.

Alisisitiza kuwa hali hiyo haikubaliki na Baraza la Chuo limekubaliana kuhakikisha linatokomezwa na litamvumilia yeyote atakayebainika kufanya vitendo hivyo.

"Katika kufanikisha hilo, chuo kimeunda kamati ya maadili (Anti-Corruption and Integrity Committee) ili kudhibiti tabia na mienendo kama hii.

"Kamati hii ilishazinduliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, aliyekuwa ameambatana na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu, Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), Diwan

INAENDELEA UK. 8



Mariam Stanford ambaye alikatwa mikono miwili na watu wasiojulikana, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uamuzi wa Kamati ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Under the Same Sun, Berthasia Ladislaus. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mahakama yaamuru Lissu kufika mahakamani Des. 19

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemwagiza mdhamini Ibrahim Ahmed wa mbunge wa zamani wa Singida Mashariki kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu Lissu, anayekabiliwa na kesi ya uchochezi kumtaka afike mahakamani Desemba 19, mwaka huu kusikiliza kesi yake.

Mahakama hiyo imesema kwa kuwa mdhamini ameieleza mahakama kwamba Lissu amepona, afike mahakamani siku iliyotajwa ili kesi iweze kuendelea.

Amri hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya kumhoji mdhamini.

**Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya hakimu na mdhamini:**

**Hakimu:** Mdhamini wa mshtakiwa, Lissu yuko wapi?

**Mdhamini:** Mheshimiwa hakimu Lissu amepona, lakini amekataa kuja kwa sababu anahofia usalama wake.

**Hakimu:** Hatutaki mambo ya siasa hapa namtaka Lissu aje hapa mahakamani kesi yake iendelee.

Alisema kesi hiyo itatajwa Desemba 19, mwaka na Lissu anatakiwa afike mahakamani siku hiyo.

Mapema mahakama hiyo iliagiza wadhamini wa Lissu kupeleka taarifa jana kuhusu mshtakiwa huyo.

Mbali na Lissu washtakiwa wengine ni, wahariri Simon Mkina, Jabir Idrisa na mchapishaji wa Kampuni ya Jamana, Ismail Mehbooh. Kwa pamoja washtakiwa hao, wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume na Sheria ya Magazeti ya mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016 jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari kisemacho, 'Machafuko yaja Zanzibar.'

Katika shtaka la pili wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016 walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar.

Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13, 2016 katika jengo la Jamana lililopo Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi. Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

## HABARI KITAIFA




Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Dk. Allan Kijazi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mafanikio ya shirika hilo katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanapa yajivunia kupaisha mapato

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (Tanapa), limesema katika kipindi cha miaka minne imeongeza mapato kutoka Sh. 175,089,696,000 hadi kufikia Sh. 279,406,200,806.

Kamishna wa Uhifadhi Tanapa, Dk. Allan Kijazi, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia miaka minne ya mafanikio waliyofikia tangu Rais John Magufuli aingie madarakani.

Dk. Kijazi alisema katika kipindi hicho Tanapa imeongeza mapato ikilinganishwa na makadirio yaliyowekwa kila mwaka.

"Tumeongeza mapato kutoka Sh. 175,089,696,000 ambacho kilikusanywa mwaka wa fedha 2015/16 hadi kufikia Sh. 279,406,200,806 mwaka wa fedha 2018/19" alisema.

Alisema mwaka wa fedha 2016/17 walikusanya Sh. 207,587,218,000 na 2017/18 yaliongezeka na kufikia Sh. 254,794,242,000.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu kumekuwa na ongezeko la makusanyo la Sh. 566,697,964,806 sawa na asilimia 60.

Alisema ongezeko hilo limetokana na juhudi za shirika hilo ilizozifanya ndani na nje ya nchi kwa kuyafikia masoko mapya.

Pia, alisema limetokana na kuongeza idadi ya watalii kutoka wageni 957,576 mwaka 2015/16 hadi 1,141,462 mwaka 2018/19 sawa na asilimia 19.2.

Kwa upande wa uhifadhi, Dk. Kijazi alisema kumekuwa na ongezeko la hifadhi mpya tatu ambazo ni Ibanda iliyopo Kyerwa, Burigi iliyopo Chato na Rumanyika wilayani Karagwe.

Alisema serikali ipo katika hatua ya mwisho ya

INAENDELEA UK. 8

# JPM awapa neno vibaraka ubeberu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli ametunukiwa shahada ya heshima ya Udaktari wa Falsafa katika Sayansi na Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), na kubainisha kuwa miaka minne ya urais wake imemuimarisha na hakatishwa tamaa na vikwazo vya watu wanaotumiwa na mabeberu.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana katika mahafali ya 10 ya chuo hicho kilichomtunuku shahada hiyo kutokana na mafanikio mbalimbali ya kimaendeleo yaliyopatikana nchini chini ya uongozi wake.

Alibainisha kuwa kwa kipindi cha miaka minne ya urais wake, kimemuimarisha na mafanikio mengi zaidi yatapatikana kama Watanzania watajituma na kutanguliza uzalendo mbele kwa kuwa Tanzania si nchi maskini.

"Si watu wengi ambao waliamini kuwa Watanzania wataweza kufanya mambo yote kwa kipindi kifupi, lakini tumeweza kwa kuwa mara zote Watanzania tukiamua hakuna linalotushinda.

"Miaka minne ya urais imeniimarisha, tukishikamana na kukusanya mapato, kuwa wazalendo, tutafanya makubwa zaidi," alisema.

Alieleza kuwa wapo wanaobeza na kukejeli, lakini nchi ni tajiri kutokana na kubarikiwa kuwa na rasilimali nyingi.

Alisema pamoja na kuwapo kwa mafanikio mbalimbali, vikwazo havikosekani na vingine vinaendelea kujitokeza.

"Kikwazo kimoja wapo ni jitihada zinazofanywa na mabeberu na vibaraka wao kwa kuwatumia wa ndani ya nchi kwa kujaribu kuweka vikwazo ili malengo yasitimie.

"Ndiyo maana kila mara mtasikia hili mara lile, ninyi ni mashahidi, sitaki kutaja yote mnayosikia, mara kuna mgonjwa huyu, mara kuna hiki, ni jitihada za kunifanya nikate tamaa, mimi sitakata tamaa.

"Miaka minne ya urais wangu nimejifunza uwezekano wa kuvishinda vikwazo hivyo upo na ni mkubwa sana ikiwa sisi Watanzania tutashirikiana na kushikamana na kwa kutanguliza uzalendo na maslahi ya taifa mbele," alisema.

Rais Magufuli alieleza kuwa alipopata barua kutoka kwa Mkuu wa Udom, Rais Mstaafu Benjamin Mkapa, kuhusu kutunukiwa shahada hiyo, alijiuliza maswali mengi.

"Nilijiuliza maswali mengi sana na maswali haya sikupata majibu yake haraka: Kwanza, ilikuwa kwanini mimi; kwanini sasa wakati nimekuwapo siku zote? Lakini, swali lingine kwanini bila kusota?

"Inawezekana mzee bure alishakufa zamani, lakini nimeandikiwa barua na Rais aliyekuwa wa kwanza kuniteua kuwa naibu waziri, nitafanyaje?

"Baada ya kupata barua, nilikaa mwezi mzima bila kujibu, baadaye wasaidizi wangu walinikumbusha 'bado hujajibu barua ya Mzee Mkapa', nikawaambia nitajibu na bado nikachelewa.

"Dhamira yangu ilikuwa inanisuta 'kwanini nipewe cha bure?' Ile dhana niliyoipata kutoka kwa baba yangu kila kitu lazima nikisotee, dhamira ilikuwa inanisuta. Hata hivyo, pamoja na hayo yote, baada ya kukumbuka historia yangu na Mzee Mkapa

INAENDELEA UK. 8




# Hukumu ya Malinzi sasa Desemba 5

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imesema itatoa hukumu dhidi ya Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi, na wenzake watatu, Desemba, mwaka huu.

Malinzi na wenzake hao wanakabiliwa mashtaka 20 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha Dola za Kimarekani 173,335.

Hukumu hiyo iliyopangwa kusomwa jana lakini Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, alisema bado haijakamilika na kwamba itasomwa tarehe iliyopangwa.

Kesi hiyo imesikilizwa na Hakimu Mkazi Maira Kasonde lakini kwa sasa amehamishwa kituo cha kazi

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikiliza hukumu na upande wa Jamhuri ulikuwa tayari.

Hata hivyo, Hakimu Shaidi alisema hukumu ya kesi hiyo itasomwa Desemba 5, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu. Mapema mahakamani hapo, upande wa Jamhuri uliita mashahidi 15 na vielelezo tisa kuthibitisha kesi hiyo na utetezi ulileta mashahidi wanne kupangua tuhuma hizo.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Celestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga na Karani Flora Rauya

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wako rumande kwa kukabiliwa na mashtaka ya utakatishaji wa fedha ambayo ni miongoni mwa mashtaka ambayo kwa mujibu wa sheria hayana dhamana huku Rauya akiwa nje kwa dhamana.




Kamishna Msaidizi wa Gesi katika Wizara ya Nishati, Sebastian Shana (kulia), akikata utepe kuzindua kitabu kipya kinachohusu usimamizi wa raslimali za mafuta na gesi nchini, kilichoandaliwa na Repoa, Taasisi ya CMI na Takwimu, kwa ufadhili wa serikali ya Norway, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk. Donald Mmari, Balozi wa Norway Tanzania, Elisabeth Jacobsen na mmoja wa wahariri wa kitabu hicho, Prof. Odd-Helge Fjeldstad. **PICHA: JOHN BADI**




# Mpango aitaka Nida kurahisisha utoaji wa vitambulisho vya taifa

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameitaka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), kurahisisha utoaji wa vitambulisho vya taifa kwa ajili ya kusaidia utoaji wa huduma za fedha nchini.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo, ikiwa ni siku moja tangu Rais John Magufuli, kumuagiza Mkurugenzi Mkuu wa Nida, Arnord Kihaule, kwenda mkoani Morogoro kushughulikia changamoto za utolewaji wa vitambulisho hivyo baada ya kupokea malalamiko kwa wakazi wa mkoa huo juzi, akiwa njiani kuelekea jijini Dodoma kwa ziara ya kikazi ya siku tano.

Akifungua mkutano wa 19 wa taasisi za fedha nchini, ulioandaliwa na Benki Kuu kwa kushirikiana na Umoja wa Benki nchini jana jijini Dar es Salaam, alisema anatambua juhudi zinazofanywa na serikali na wadau mbalimbali kuboresha sekta ya fedha ikiwamo kujenga kanzi data za taarifa za wateja na utoaji wa Vitambulisho vya Taifa.

"Natoa rai kwa mamlaka husika kuharakisha utoaji wa vitambulisho vya taifa kwa upande mmoja na benki kuhakikisha wanaboresha utoaji huduma za kifedha," alisema Dk. Mpango.

Pia, Dk. Mpango, aliutaka mkutano huo wa siku mbili kujadili na kutoa mapendekezo ya mkakati ya kushusha riba ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa gharama nafuu na hivyo kuchochea maendeleo ya uchumi.

"Riba ya mikopo bado ipo juu kiasi kwamba watu wengi wanashindwa kukopa na baadhi ya waliokopa kushindwa kurejesha. Hivyo licha ya juhudi za kuboresha sekta hii, ningependa mkutano huu utoe mapendekezo ya mikakati ya kushusha riba," alisema Dk. Mpango.

Aliwataka pia kujadili na kubainisha mikakati mipya ya kupunguza na kudhibiti kiasi cha mikopo chechefu katika benki.

Kadhalika alisema, mikopo kwa sekta kilimo siyo ya kuridhisha kwa sababu imekuwa chini ya asilimia tano ya mikopo yote itolewayo na benki.

Alisema sekta ya kilimo ni muhimu katika kutoa malighafi kwa ajili ya viwanda, chanzo kikuu cha chakula na fursa za ajira kwa Watanzania wengi na sekta yenye uwezo wa kupunguza umaskini na kuchangia upatikanaji wa fedha za kigeni kwa kasi kubwa.

"Ni matarajio yangu kuwa mjadala wenu utaangalia namna bora ya kuzifanya taasisi za fedha kuongeza mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya kilimo cha mazao, ufugaji, uvuvi na biashara husika," alisema Dk. Mpango.

Vile vile, aliwataka kujadili na kutoa mapendekezo ya namna ya taasisi hizo zinavyoweza kuchangia katika upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya kimkakati ya serikali na ya sekta binafsi nchini.

Awali, Gavana wa Benki Kuu (BoT), Prof. Florens Luoga, alisema sekta ya fedha imekua kwa wastani wa asilimia 3.1 na inachangia katika ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 2.6 kwa kipindi cha miaka mitano iliyoishia 2018.

Alisema taasisi hizo zimeenea maeneo mbalimbali nchini na kwamba kuna benki 61 na matawi 838 nchi nzima.

Prof. Luoga alisema pia akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuongezeka na kufika Dola za Marekani bilioni 5.4 mwezi Oktoba mwaka huu na kiasi ambacho kinatosheleza kuagiza bidhaa kutoka nje kwa zaidi ya miezi sita.

## TOLEO MAALUM MIAKA MINNE YA MAGUFULI


# Tancoal yampongeza Rais John Magufuli kwa utawala bora baada ya miaka minne

Katika kipindi hicho cha miaka mine, sekta ya madini imeshuhudia mageuzi makubwa ya kihistoria chini ya uongozi wa Rais Magufuli ambaye binafsi ametoa mchango mkubwa katika mageuzi hayo. Tancoal ni moja ya makampuni ambayo yamenufaika na mageuzi hayo makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imetoa ushirikiano ulifanikisha kukua na ongezeko la uzalishaji wa makaa yam awe nchini.

Tancoa imeongeza uzalishaji na kukua kama kampuni lakini pia yamejitokeza makampuni madogo nay a kati yanayo chimba makaa yam awe ambapo wote kwa pamoja tunachangia ukuaji wa uchumu wetu.

Uzalishaji wa makaa yam awe unaofanywa na Tancoal umekuwa ukiongezeka kutoka tani 237,735.93 kati ya Juni 2014 na Julai 2015. Katika mwaka wa fedha wa Julai 2018 na Juni 2019, Tancoal imeuza tani 788,702 za makaa yam awe ambalo ni ongezeko la zaidi ya asilimia 300 katika kipindi cha miaka mine iliyopita. Kwa kipindi cha Julai 2019 na Oktoba 2019, Tancoal imeshauza tani 225,616 za makaa ya mawe. Mauzo haya siyo katika soko la ndani bali pia soko la kimataifa ambalo mauzo yake yameongezeka kwa kwa zaidi ya asilimia 30 katika kipindi hicho cha miaka minne na kwa hivo kuipatia nchi pesa za kigeni.

Aidha, ukuaji huu wa mauzo ya makaa yam awe kwenda soko la kimataifa, yanatarajia kuongezeka zaidi kwa kupitia bandari ya Mtwara iliyoboreshwa kwani kuna nchi zimeonesha nia ya kununua bidhaa hiyo kama vile Uturuki, Madagascar na Ethiopia. Pia, mauzo hayo yataongezeka pia kutokana na mango wa serikali kuwekeza katika miundombinu ya Ukanda wa Kusini kwa njia ya reli kwenda bandari ya Mtwara jambo ambalo litaifanya shehena yetu ya makaa yam awe kuwa na bei bora na kuweza kushindana kimataifa. Tancoal inayahusisha mafanikio haya yote moja kwa moja na utendaji uliotukuka wa Rais Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano.




Ongezeko la mauzo ya makaa ya mawe kwa miaka minne iliyopita

***Viwanda***


Tancoal inaendelea kuviuzia viwanda nchini bidhaa bora ya makaa yam awe kwaajili ya nishati katika uzalishaji katika viwanda vinavyo zalisha bidhaa mbalimbali nchini. Miongoni mwa wateja wakubwa wa Tancoal ni karibia viwanda vyote vya saruji nchini ambavyo hutumia makaa yam awe kama nishati kuzalisha bidhaa zao lakini pia viwanda mbalimbali kama vile vitengenezavyo vigae na bidhaa za jesi.

***Mahusiano***

Tancoal inaendelea kushirikiana na Serikali na taasisi zake zote kushughulikia mambo mbalimbali yaliyopo katika meza ya majadiliano ili kufikia muafaka. Tancoal inapenda kupongeza ushirikiano inaopata kutoka Wizara na Madini na taasisi zake kama Tume ya Madini na hasahasa Ofisi ya Mkoa ya Madini Songea ambayo Tancoal inafanya nayo kazi kila siku.

Katika kuunga mkono dhana ya kutoa kipa umbele katika ushiriki wa Watanzania kwenye sekta ya madini, Tancoal imemteua ndugu Daniel James Mikeze kama mjumbe wa bodi tangu Oktoba 23, 2019. Mikeze ambaye ni Mtanzania mwenye uzoefu mkubwa katika sekta ya madini na ujenzi, atasaidia sana kampuni kufikia marengo yake siku za baadae.









## SALAMU ZA PONGEZI

**Tancoal Energy Limited (Tancoal)** inaungana na Watanzania wote pamoja na jumuiya ya kimataifa kumpongeza **Rais John Pombe Magufuli** kwa kutimiza **miaka minne** ya utawala uliotukuka tangu aapishwe kushika wadhifa huo mwezi Novemba mwaka 2015.

Tancoal Energy Limited
5th Floor, Amverton Tower, Plot No.1127
Chole Road, Masaki
P. O. Box 23059, Dar es Salaam
Tel: +255 222 13 7512
E-mail: info@tancoalenergy.com
www.tancoalenergy.comes Salaam, Tanzania

TANCOAL

215528702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Talaka za kuwatesa watoto zisivumiliwe

NI jambo linalowapa furaha mke na mume ndani ya ndoa pamoja na watoto wao kuishi kwa upendo kama wanafamilia.

Ndoa kwa taifa ni msingi wa mambo yote, hapo ndipo wanapozaliwa raia wema, walipa kodi, wapiga kura na kwa ujumla nguvu kazi na tegemeo la taifa. Hata hivyo siku hizi ndoa zinayumba kiasi kwamba kasi ya kuvunjika iwe kwa kupeana talaka au kutelekeza na kukimbia familia ni mambo yanayotishia hatima ya taasisi hiyo.

Haya ni miongoni mwa mambo ambayo yanalihofisha taifa. Kama Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Dk. Faustine Ndungulile, anavyodokeza hivi karibuni.

Analitaja tatizo la kuvunjika kwa ndoa na taathiri kwenye malezo ya watoto ambao wanaachwa kujilea wenyewe, kukosa huduma za kijamii na muhimu kama elimu na pia kuwa wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia. Tunaungana na Naibu Waziri kusema kuwa suala la kuvunjika ndoa kwa kasi kubwa limekuwa mwiba kwa watoto.

Wengi wanakoseshwa matunzo na huduma muhimu na za lazima, mara ndoa zinapovunjika.

Wanandoa wanapotoa talaka kila saa wanawafikiriaje watoto? Ufike wakati wakumbuke kuwa ndoa zinapovunjika mara nyingi zinawakosesha watoto matunzo na huduma muhimu ambazo ni haki yao kama binadamu. Tungependa kuwashauri wana ndoa kuwa kama wamegombana na kukosana wakumbuke kwanza kuwa wenye tatizo ni mke na mume wala watoto hasa waliochini ya umri wa miaka mitano na walioko shuleni hawahusiki wala hawalifahamu hilo.

Tunaona kuwa kuwatelekeza watoto na kuwaacha kuhangaika kiasi hicho kisa ndoa imevunjika hatuwatendei haki.

Ikumbukwe wakati wenza hao wanafunga ndoa, walifuata taratibu, kanuni, misingi, matakwa, maelekezo na ahadi kuwa watavumiliana na kupendana bila kujali ni Wakristo au Waislamu au wana imani za kimila. Tunajiuliza hawa wanaoachana wanatumia misingi na kanuni zipi kuwatelekeza watoto? Na kuwakosesha watoto matunzo na huduma kwa madai kuwa ndoa imevunjika.

Kuna masuala mengi yanayoeleza jinsi watoto wanavyohangaika kwa kukosa matunzo. Pengine wakati umefika kwa serikali na wadau kuweka mikakati ya kuandaa muswada wa sheria wa kuhudumia watoto baada ya ndoa kuvunjika. Tunaamini sheria hii itawawajibisha baba na mama wanaoachana kujipanga namna ya kuwahudumia watoto wao na kuwajibika kwa kila namna hadi watakapofikia umri wa kujitegemea.

Haitoshi kama taifa kukaa kimya na kuwaacha watuhumiwa wa kuzikimbia familia zao wakistarehe bila kujali matunzo kwa watoto wao wakiendelea kufurahia maisha.

Kama kasi ya talaka inatisha ni lazima serikali ichukue hatua kuhakikisha huduma na matunzo kwa watoto wa wanandoa walioachana zinaendelea kutolewa.

Taasisi za kisheria, mahakama, polisi na ustawi wa jamii pamoja na madhehebu ya dini nazo zisifumbie macho tatizo hili la kutelekeza watoto. Kama wapo wanaharakati walioifikisha serikali mahakamani hadi kufutwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kuwa inanyanyasa watoto waanze tena harakati za kuwatelekeza watoto.

Tunawategemea pia kuhamasisha na kupinga talaka zisizo na tija kwa afya na ustawi wa watoto.

Tunaamini kuwa kila jambo linawezekana ikiwa kila mmoja atatimiza wajibu wake bila ya kusimamiwa. Kama tuliaminiana na kuona lengo lilikuwa ni kuwa na ushirika wa maisha, lakini kupata watoto na jukumu kubwa ni kuwatunza watoto inakuwaje tunajisahau? Ni wakati wa kuwa na fikra mpya juu ya talaka huria zinazotolewa bila kujali hatima ya maisha ya watoto. Tuache kutelekeza watoto na kuachana na utaratibu huu ambao unaliangamiza taifa letu. Shime tushirikiane kuwanusuru watoto ambao ndilo taifa letu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hakuna ruksa kwa ajali hizi kupitia sura yoyote

NI miaka sasa, bodaboda ndizo zinalalamikiwa kwa ajali na kuongoza kusababisha vifo na majeruhi, kutokana na ajali za barabarani nchini.

Hivi sasa inaelezwa kwamba, hali hiyo imebadilika na kugeukia magari binafsi, kwamba yanazidi kuongeza kwa kusababisha ajali katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo wa mwaka huu wa 2019, kuliko bodaboda.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Mrakibu Msaidizi wa Polisi ASP Deus Sokoni, wanachukua hatua mbalimbali kudhibiti ajali za magari binafsi.

Ni hatua zinazoenda sambamba na kufungia leseni za madereva wanaosababisha ajali kwa uzembe, kujihusisha na ulevi, mwendo kasi na makosa mengineyo, yakiwamo ufungaji wa mikanda.

Kamanda huyo ametoa taarifa hiyo kwa vyombo vya habari Septemba mwaka huu, na kwamba wanatarajia kufanya mabadiliko ya kisheria, yatakayosaidia kudhibiti hayo ya magari.

"Tupo kwenye mchakato wa mabadiliko ya sheria, ili iwe lazima kwa abiria wote wanaopanda magari binafsi kufunga mikanda. Kwa sasa anayelazimika kisheria ni dereva na abiria wa mbele tu," anasema ASP Sokoni.

Taarifa ya Polisi inafafanua katika kipindi cha miezi sita, kati ya Januari na Juni mwaka huu, zinaonyesha magari binafsi yamekuwa vinara wa kusababisha ajali vifo kwa majeruhi.

Hadi sasa taarifa hiyo inatamkwa magari hayo yamesababisha ajali zipatazo 528, vifo 222 na majeruhi 453, kwa wastani kila siku magari binafsi yanasababisha ajali tatu, kifo cha kati ya mtu mmoja na wawili, idadi na wastani kama huo kwa majeruhi.

Pia, taarifa inaonyesha kuwa kwa upande bodaboda, kwa miezi sita ya mwanzo wa mwaka uliopo, imeshasababisha ajali 334, vifo 176 na majeruhi 319.

Kwa wastani, bodaboda zinahusika katika ajali mbili kila siku na kusababisha kifo cha mtu mmoja, majeruhi mmoja hadi wawili.

Vivyo hivyo, mabasi ya abiria yanapata ajali 103 na kusababisha vifo 61 na majeruhi 195 katika kipindi hicho.

Taarifa hiyo kwa upande wa malori ni kwamba yalihusika katika ajali 167 na kusababisha vifo vya watu 130 na majeruhi 142, wakati daladala zilipata ajali 143, na kusababisha vifo 89 na majeruhi 268.

Nimeeleza kwa kirefu jinsi hali ilivyo. Pia, ni muhimu kujua ajali hizo zina athari kubwa katika jamii, ikiwamo kuongezeka yatima, zao la wazazi kupoteza maisha, huku wapo wanaosababishiwa ulemavu wa kudumu na wakati mwingine kunamfanya muathirika ashindwe shughuli zake za kila siku za kumwingizia kipato na kulazimika kuwa mtu wa kusaidiwa.

Kimsingi ajali hazina kinga, lakini zinaweza kuzuilika, ni muhimu zizuilike ili kuokoa maisha ya Watanzania badala ya kuendekeza uzembe na kusababisha vifo vya watu wasio na hatia.

Inasikitisha kwamba baadhi ya ajali zinasababishwa kwa uzembe, kujihusisha na ulevi, mwendo wa haraka na makosa mengineyo yakiwamo ya kutofunga mikanda.

Kwa hali kama ya namna hiyo, madereva hawana budi kuheshimu sheria za usalama barabarani kuokoa maisha ya Watanzania, yanayopotea na wakati mwingine ni sababu za kizembe.

Inaelezwa kwamba kila sekunde 24, kuna maisha ya mtu mmoja anayepoteza maisha katika ajali barabarani duniani na kwamba chanzo kikubwa cha vifo miongoni mwa watoto na vijana wa umri wa kuanzia miaka mitano hadi 29 ni ajali hizo.

Ndivyo Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, alikaririwa na vyombo vya habari akisema, wakati akitoa ujumbe maalum, katika maadhimisho ya kimataifa ya usalama barabarani, Novemba 17. Kwamba hatari ya kufa kutokana na ajali za barabarani iko juu mara tatu zaidi katika nchi za kipato cha chini kuliko kwenye nchi za kipato cha juu na anatoa wito kila mtu kushughulikia tatizo la usalama barabarani.

Anasema, zaidi ya nusu ya vifo vyote vya ajali za barabarani, miongoni mwa makundi walio katika hatari ni watumiaji wa barabara kama watembea kwa miguu, waendesha baiskeli na waendesha pikipiki.

Kwa sababu ajali hizi zinawakumba waliomo na wasio kuwemo, ni wajibu wa kila mmoja kuzikemea hasa zile za kizembe zilizotajwa na Kamanda Deus Sokoni, ambazo kimsingi zinaweza kuzuilika.

Wote tunaweza kuamua kwamba Tanzania bila ajali za kizembe inawezekana na kila mmoja akachukua hatua ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa mamlaka husika anapona kuna uzembe unataka kufanyika.

# TANGAZO

TANZANIA UGANDA COMOROS DJIBOUTI

## UFAFANUZI JUU YA TUHUMA ZINAZOENDELEA KUHUSU BENKI YA EXIM TANZANIA

Siku za hivi karibuni kumekuwa na machapisho kwenye baadhi ya magazeti (sio magazeti makubwa ya kila siku) yakiandikwa na mwandishi ambaye bado hajajulikana, akijaribu kuharibu sifa nzuri za makampuni imara nchini Tanzania, ikiwemo benki yetu (benki ya Exim), Wakurugenzi wetu na wanahisa wetu.

Madai hayo yasiyokuwa na msingi wala uthibitisho ambayo kwa namna moja ama nyingine yanailenga benki yetu, wakurugenzi au wadau wetu na kuwahusisha na uchukuaji wa mali ya mteja kinyume na sheria kwa lengo la kuinufaisha benki yetu au mkurugenzi fulani ama mwanahisa fulani. Machapisho katika magazeti hayo yanahusu mali hiyo inayomilikiwa na Nimrod Mkono na kesi namba 59 ya mwaka 2018 iliyopo Mahakama Kuu Kitendo cha Biashara Dar es Salaam.

Kujibu madai haya yasiyokuwa na msingi na ambayo yametolewa kwa nia mbaya, Benki ya Exim ingependa kufafanua kama ifuatavyo.

i. **Deni la Mkopo kwa Nimrod Mkono**
Muheshimiwa Nimrod Mkono ni mteja wetu kupitia mkopo ambao alichukua yeye binafsi, akiweka dhamana ya nyumba yake iliyopo jijini Dar es Salaam. Kulingana na masharti ya makubaliano ya mkopo yaliyotimizwa na Mteja huyu, Nimrod Mkono, alikubaliana na masharti ya mkopo ikiwa ni pamoja na ulipaji wa pesa zilizokopwa benki, kulingana na masharti ya mkopo na sheria za Tanzania. Cha kusikitisha, mteja hakufuata masharti ya mkopo kama alivyokubaliana na Benki.

Kufuatia kutofuata masharti ya kulipa mkopo kama ilivyokubaliwa na licha ya kuongezewa muda wa kulipa mkopo mteja hakuweza kulipa mkopo kama ilivyokubaliwa. Hivyo basi Exim Benki kwa kufuata sheria na miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania na baada ya jitihada mbali mbali za kumtaka Mheshimiwa Nimrod Mkono kulipa deni kutofanikiwa, haikuwa na chaguo zaidi ya kuanza utaratibu wa kukusanya deni kutoka kwa Bwana Mkono. Benki iliamua kwenda katika Mahakama Kuu – Kitengo cha Biashara na kufungua Kesi namba 21 ya 2018.

Kesi hii ilishughulikiwa na kutatuliwa kwa mujibu wa makubaliano katika kesi nyingine (Kesi ya Bishara Na. 59/2019) ambayo ilimuhusisha Mhe. Mkono kama Mdhamini wa kampuni ijulikanayo kama Baobab Properties Limited

ii. **Deni la Mkopo kwa Baobab Properties Limited**
Baobab Properties Limited ("Baobab") pia ni mteja wa benki. Juni 2014, Exim Bank walitoa mkopo kwa Baobab, Dola za kimarekani 750,000.00. Mheshimiwa Nimrod Mkono kama Ilivyolezwa awali alikuwa mmoja wa wadhamini binafsi wa mkopo wa kampuni ya Baobab

Baobab haikulipa deni. Kitendo hiki kilisababisha Benki kutoa notisi ya kisheria ya siku 60 kwa Baobab na wadhamini wake tarehe 13 Juni 2016 Ikiwata Baobab na wadhamini wake kulipa deni Licha ya hii notisi ya kisheria na jitihada kadhaa za benki kutaka Baobab na wadhamini wake kulipa deni walishindwa kulipa mkopo kama ilivyotakiwa.

Sanjari na majukumu yake chini ya sheria , Benki Ilijitahidi kurudisha deni hilo kupitia dhamana ya ardhi ambayo yenye umiliki wa Baobab, Iliyopo eneo la Kunduchi. Hata hivyo, Baobab Ilipinga jitihada hiyo kwa kufungua kesi dhidi ya benki (Kitengo cha Ardhi, Maombi ya Ardhi Na. 315 ya 2017) wakizuia benki kuuza mali Iliyowekwa kama dhamana ya mkopo na kuweka pingamizi la kuuza mali hizo (Mis. Land Application No. 723 /2017)

Hivyo basi, bada ya jitihada za Benki kutaka kuuza kisheria mali zilizowekwa kama dhamana ya mkopo kupingwa mahakamani kwa kuwekewa mapingamizi mbalimbali, Benki ikaona njia pekee ni kufungua kesi mahakamani kuiomba mahakama imumuru Baobab na wadhamini wake akiwemo Mheshimiwa Mkono kulipa deni walilokopa. Benki Ikafungua Kesi namba 59/2018 katika Mahakama Kuu kitengo cha Biashara Dar es Salaam.

Kwa ufanunuzi Kesi namba 59/2018 katika Mahakama Kuu kitengo cha Biashara Dar es Salaam. haikufunguliwa na mwanahisa yeyote au mkurugenzi yeyote wa Benki kama ilivyopotoshwa na magazeti husika ambayo yalichapisha habari hii bila kujua ukweli halisi wa tukio zima. Kesi hiyo ilifunguliwa na Benki dhidi ya Kampuni iliyoshindwa kulipa deni (Baobab) na wadhamini wake.

Wakati kesi hiyo ikiendelea Mahakamani, Baobab Properties na Wadhamini wake waliingia katika majadiliano ya kulipa deni ambapo makubaliano yalifikiwa na baadaye kusajiliwa Mahakamani na kutolewa kama **Hukumu (Consent Judgment)**. Hukumu kama hii hutolewa na Mahakama - kwa kuzingatia makubaliano kati ya pande zinazohusika katika kesi.

Baadhi ya makubaliano ambayo yamo katika hukumu hii (consent judgment) ni kama Ifuatavyo:

i. Wadaiwa kwa pamoja na wadhamini wao wanatakiwa kulipa deni pamoja na riba katika Kesi zote mbili Kesi Namba. 21 ya 2018 (Kesi dhidi ya mkopo binafsi wa Bw. Nimrod Mkono) na kesi Namba 59 ya 2018) zilizofnguliwa kwenye Mahakama Kuu kitengo cha Biashara

ii. Baobab awali ya yote atauza mali zake ziliyojumuishwa katika Hati Nambari 59293/4/1, 59293/4/3 na 39534 ambazo zinapatikana kwenye ghorofa ya 8 na 10 za jengo linalojulikana kama Exim tower kwenye viwanja Na. 1403/45 na 1404/45 Eneo la Kati (Central Area), Ghana Avenue, Dar es salaam na Kiwanja No. 1 Kunduchi Beach, Dar es Salaam kwa mfuatano ("Mali") ili kulipa kiasi kilichoamuliwa kulipwa kutokana na malalamiko katika kesi za Biashara Na. 21 ya 2018 na 59 ya 2018;

iii. Benki haitatekeleza amri ya mahakama kwa muda wa miezi sita (06) tangu tarehe ya kurekodi makubaliano hayo kama mahakamani ili kuruhusu uuzaji wa Mali hizo ufanyike na taratibu za malipo ya mauzo kwa Benki kuelekea kukamilisha Amri hiyo

iv. Baobab Properties Limited itatoa mapato yatokanayo na Uuzaji wa mali husika kwa Benki ambayo itayahifadhi mapato hayo katika Akaunti ya Benki iliyochaguliwa na kwamba mapato hayo yatatumika kama ifuatavyo:

    a. Kwanza kulipa Kamisheni ya Wakala wa mauzo na ushuru wote unaotokana na Uuzaji wa mali hizo;
    b. Pili, kukidhi amri ya mahakama katika Kesi ya Biashara Na. 59 ya 2018;
    c. Tatu, kukidhi amri ya mahakama katika kesi ya biashara nambari 21 ya 2018 (ambayo ni dhidi ya Nimrod Mkono ya mkopo binafsi); na
    d. Kama kuna ziada kulipa salio lililobaki kwa Baobab Properties Limited

v. Kwamba katika kipindi cha miezi sita ya kuruhusu Baobab Properties Ltd na wadhamini wake kuuza mali zake, Benki haitatoza riba yoyote katika mikopo hiyo.

vi. Baada ya kumalizika kwa kipindi cha miezi sita (6), Benki itakuwa na uhuru wa kutekeleza Amri ya mahakama katika kesi za Biashara No 21 ya 2018 na 59 ya 2018 kwa njia yoyote ile Benki inayoona inafaa.

vii. Baada ya kurekodi makubaliano haya, Baobab Properties Limited itachukua hatua za haraka za **Kuondoa Kesi ya Ardhi Na. 315 ya 2017** iliyopo katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Idara ya Ardhi, Dar es Salaam.

Licha ya Baobab na washirika wake kuongezewa muda zaidi wa miezi sita kulipa deni kama Ilivyokubaliwa, Baobab na wadhamini wake walishindwa kutoa kulipa deni kama ilivyokubaliwa mahakamani.

Kutokana na kushindwa kufanya hivyo, benki haikuwa na chaguo zaidi ya kurudi mahakamani (Chini ya Kipengele cha vi hapo juu, ambayo ni aya ya 11 ya Hukumu ya Makubaliano) Kutekeleza kwa ajili ya kutekeleza amri ya mahakama. Utekelezaji wa amri ya mahakama unaendelea chini ya agizo la Mahakama Kuu ya Tanzania kitengo cha Biashara.

**HIVYO**, kimsingi benki haihusiki na madai yoyote ya mchezo mchafu unaohusisha benki, wakurugenzi au wanahisa wake katika jambo hili. Benki ya Exim ni benki ya kistaarabu, yenye sifa ya muda mrefu katika tasnia ya mabenki nchini Tanzania na kwingineko. Shughuli zote za benki hufanywa kwa mujibu wa sheria, kanuni na maagizo yanayosimamia sekta benki nchini Tanzania.

Kwa kuwa kampeni hizi mbaya na za makusudi zenye lengo ya kuichafua Benki ya Exim kwenye jamii, tunapenda kuwataarifu wateja wetu kuwa tumeanzisha taratibu za kuwachukulia hatua za kisheria dhidi ya wote waliojihusisha na uchapishwaji wa habari hizi potovu dhidi ya Benki na wakurugenzi na wanahisa wake

Uongozi,
Benki ya Exim Tanzania

**KUMBUKA:**
Taarifa hiyo hapo juu inapatikana kwa umma na inaweza kuthibitishwa kwa njia ya kumbukumbu za Mahakama katika Mahakama kuu ya kesi ya Biashara Na. 21/2018 na kesi ya biashara Namba 59/2028 katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Biashara (Msajili wa Mahakama Dar es Salaam).

EXIM BANK
*Innovation is life*

# CUF yafafanua madai ya kuandamana Dar

Na Mwandishi Wetu



CHAMA cha Wananchi (CUF) kimesema hakina nia ya kufanya maandamano yoyote katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Prof. Ibrahim Lipumba (pichani), aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa zilizokuwapo kuwa chama hicho kinatarajia kufanya maandamano.

Prof. Lipumba alisema wanachama na uongozi wa CUF hawana nia wala kutarajia kufanya maandamano yoyote bali kijipanga katika kukijenga chama ili kiweze kushiriki uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2020.

"Kwa hiyo hatuna mpango wa kufanya maandamano Novemba 24, ambayo itakuwa ni siku ya uchaguzi wa serikali za mitaa, kazi tuliyonayo ni kukijenga chama kuhakikisha uchaguzi wa mwaka 2020 tunashiriki kwa kikamilifu," alisema Prof. Lipumba na kuongeza:

"Hatujatoa taarifa kwa mtu yoyote kwamba tunaandamana, endapo tutahitaji kuandamana tutafuata utaratibu na sheria zilizopo nchini za kuandamana, Tutatoa taarifa katika vyombo husika na siku ya kufanya maandamano ambayo ni saa 48 kabla ya siku ya kuandamana," alisema Prof. Lipumba.

Alisema endapo watahitaji kuandamana wataandika barua ya kuwa na nia ya kutekeleza tukio hilo na kwamba watajiandaa vizuri ikiwamo kuwaandaa wanachama, kuandika barua rasmi kwa mamlaka husika kuwa wanahitaji kufanya maandamano siku fulani na wataanzia eneo moja kwenda lingine.

Prof. Lipumba alisema alilazimika kwenda kuwazuia wanawachama wa CUF waliokusanyika katika ofisi za chama hicho zilizopo Temeke jijini Dar es Salaam wasiende maeneo ya Zakhem Mbagala ambako ilidaiwa kuwa maandamano hayo yangefanyika.


KDF Kilimanjaro Development Forum

P.O Box 32055,
Dar es Salaam, Tanzania
+255 688 591 182
john@stageneraltz.com

**MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANACHAMA**

Wanachama wa KDF wanatangaziwa kwamba kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama wote utakaofanyika tarehe 21, Desemba, 2019 katika ukumbi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi.

**Agenda:**

1. Kupokea taarifa ya maendeleo ya KDF;
2. Kupokea na kupitia taarifa ya fedha ya KDF;
3. Kuchagua maafisa wa KDF na wajumbe wa bodi ya uongozi;
4. Kuteua wakaguzi na wadhamini au kuwathibitisha wanaoendelea;
5. Kupanga michango/ada za mwaka unaofuata, na
6. Kupitia na kupitisha marekebisho ya katiba.

**Uchaguzi wa viongozi katika nafasi zifuatazo;**

1. Mwenyekiti
2. Makamu Mwenyekiti
3. Katibu
4. Naibu Katibu
5. Mweka Hazina
6. Mweka Hazina Msaidizi

**Maombi ya kugombea nafasi hizi yatumwe kwa anwani zifuatazo:**
**Dr. Jonas Kipokola,**
**Katibu (KDF),**
**S.L.P 8448, Moshi au barua pepe**
**info@kilimanjarodevelopmentforum.org au piga simu 0754386003**
**Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya kugombea ni tarehe 7 Desemba, 2019.**

Mkutano Mkuu utafuatiwa na sherehe ya Kilimanjaro Day itakayofanyika siku hiyo hiyo. Umoja wetu ndiyo nguvu ya mafanikio yetu, karibuni sana

**Imetolewa na:**
**Dr. Jonas Kipokola**
**Katibu, Kilimanjaro Development Forum**

615528802


# Udom yakiri rushwa ya ngono

INATOKA UK. 2

Athumani," alisema.

Aliongeza kuwa uongozi wa chuo utahakikisha unachukua hatua kali za kinidhamu kwa mfanyakazi yeyote atayejihusisha na tabia hizo.

"Pia wanafunzi wameanzisha klabu ya kukabiliana na mambo haya na tunaipa uzito ili kuwa na 'zero tolerance' kwenye hili," alisema. Katika hatua nyingine, kiongozi huyo wa Udom alisema vyeti vilivyotolewa kwa wahitimu wa mwaka huu vimetengenezwa kwa ubora mkubwa na si rahisi mtu yeyote kughushi kwa kuwa vimeongezwa alama za siri.

"Chuo kilitarajia kudahili wanafunzi 15,000 kwa mwaka huu wa masomo. Hadi sasa, 9,674 wamedahiliwa, hadi wiki ijayo tunatarajia kuongeza idadi hii," alisema.

Sambamba na hilo, alisema chuo kina watumishi 1,465 na kwamba idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya chuo hicho.

"Tunaomba serikali mtusaidie kupata idadi ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya chuo, pia tumefanya ukaguzi wa taaluma za wafanyakazi ili kuwa na watu stahili katika maeneo stahili," alisema.

Alisema wafanyakazi watakaoonekana waliyosomea hayahitajiki chuoni hapo, watarudishwa kwa Katibu Mkuu Utumishi ili kupangiwa kazi nyingine.

Prof. Bee pia alisema watapitia mikataba yote ili kupunguza gharama ikiwamo ya kupangisha makazi ya wanafunzi kwa mikoa ya Iringa na Singida.

# JPM awapa neno vibaraka ubeberu

INATOKA UK. 3

aliponitoa, nikaona nikubali.

"Kingine kilichonifanya nikubali kutunukiwa, nikakumbuka shahada hizi huwa hazitolewi kwa kumpa mtu binafsi bali kwa niaba ya wengine, na imetolewa kwa kutambua mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

"Natambua si yangu binafsi, bali ni ya Watanzania wote, hasa wenye kuchapa kazi kwa bidii na kulipa kodi, kila Mtanzania mwenye kufanya hayo afurahie shahada hii," alisema.

Rais Magufuli alikumbusha kuwa mwaka 2015 Watanzania walidai mabadiliko ambayo yanahitaji kuwa na fedha na hivyo kulazimika kuongeza ukusanyaji mapato ya kodi kutoka Sh. bilioni 850 kabla ya Novemba 2015 hadi wastani wa Sh.trilioni 1.2 kila mwezi.

Alisema shahada hiyo imempa nguvu yeye na wasaidizi wake ya kujituma zaidi kutokana na kutambua mafanikio yaliyopatikana.

Alisema serikali yake pia inahitajika kudhibiti matumizi ya fedha ikiwamo kudhibiti safari za nje, kuondoa watumishi hewa na wenye vyeti vya kughushi, mikopo hewa, wanafunzi hewa, pembejeo hewa, likizo hewa, safari hewa na kile alichotania kuwa ndoa hewa na mapenzi hewa.

Alieleza kuwa waliamua kuwa fedha zipelekwe maeneo ya maendeleo hususani miradi mbalimbali ili kuleta tija kwa nchi kwa kuongeza bajeti yake.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Gaudencia Kabaka, alisema wameanzisha kitengo kipya chuoni kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika kazi kwa taasisi mbalimbali na kupunguza gharama zisizo na tija.

Alisema wametoa shahada hiyo kwa viongozi watatu hadi sasa ambao ni Rais mstaafu Jakaya Kikwete, Waziri Mkuu mstaafu, Hayati Rashid Kawawa na Rais Magufuli.

# Tanapa yajivunia kupaisha mapato

INATOKA UK. 3

kuanzisha hifadhi za taifa mpya tatu ambazo ni Nyerere, Kigosi na mto Ugala ambapo kukamilika kwake utazifanya zifikie 22.

Dk. Kijazi alisema wameongeza mchango wa kodi kwa serikali kutoka Sh. bilioni 31 mwaka 2016/17 hadi kufikia Sh. bilioni 42 mwaka 2018/19.

"Katika kipindi cha miaka minne Tanapa imetenga Sh. 111,374,526,023.00 ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2018/19. "Miradi hii imehusisha uimarishaji wa huduma za utalii ikiwamo ujenzi wa maeneo ya malazi ya gharama nafuu, miradi ya kuongeza bidhaa za utalii, nyumba za wafanyakazi, vifaa vya kazi kama boti, magari na ndege," alisema.

Pia alisema Tanapa imetatua migogoro ya matumizi ya ardhi ambapo mwaka 2018/19 walishirikiana na vijiji vya pembezoni mwa hifadhi za taifa kuandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na kuweka alama za kudumu za mipaka kwenye maeneo ya hifadhi.

Pia, alisema kumekuwa na jitihada za kukabiliana na changamoto ya ardhi ikiwamo ya uingizaji mifugo kwa ajili ya malisho.

Akizungumzia vita dhidi ya ujangili na ongezeko la idadi ya wanyama waliohatarini kutoweka, Dk. Kijazi alisema wamewaongeza faru kwa asilimia 10 na kudhibiti ujangili kwa zaidi ya asilimia 90.

"Majangili 14, 464 wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo mbalimbali vya dola," alisema.

Kadhalika, alisema kumekuwa na ongezeko la masoko mpya ya watalii wa nje kutoka 518,457 na kufikia 715,314 baada ya masoko mapya ya bara la Asia na Mashariki ya mbali hususani Israeli, Uturuki, China na Urusi.

Alisema kumekuwa na ongezeko la vitanda vya watalii wa nje kutoka 2,400 hadi kufikia 5,829 na vya wageni wa ndani kutoka 3,601 hadi 4,970, na kwamba kwa ujumla vitanda kwa ajili watalii wa nje ya mipaka na wa ndani ni 10,799.

HABARI KITAIFA

# Waziri awabana wasafirishaji gesi asilia athari za mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** KILWA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, ameagiza kituo cha kupokea gesi asilia cha Songas eneo la Somanga, kuwasilisha mpango kazi wa usimamizi wa mazingira unaoonyesha madhara na hatua zinazochukuliwa pindi yanapotokea maafa.

Sima alitoa agizo hilo wakati wa ziara yake wilayani Kilwa mkoani Lindi, kukagua kituo hicho ambacho hivi karibuni kilipata tatizo la kuvujisha bomba la gesi katika eneo hilo.

Katika ziara yake hiyo, Sima alifuatana na Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) Prof. Esnat Chagu na Mkurugenzi Mkuu wa baraza hilo, Dk. Samuel Gwamaka.

Alisema ni muhimu wananchi wa vijiji zaidi ya 60 vilivyopitiwa na mradi wa bomba la gesi asilia kupatiwa elimu sahihi kuhusu faida za mradi huo na madhara pindi yanapotokea matatizo kama lililotokea juzi. Naibu waziri huyo aliongeza kuwa nchi imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi na hasa gesi asilia huku akiwataka wahusika kuhakikisha mikataba inayoingiwa na makandarasi ionyeshe ushiriki wa wananchi na utolewaji wa elimu kwao kuhusu madhara ya gesi inapolipuka.

"Tumekuja hapa tuone kama miradi hii inafuata Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na hapa tunataka tuone kwenye eneo hili yakitokea madhara ni hatua gani zinachukuliwa, tunataka kuona taarifa kamili na tuangalie kwenye eneo letu la mazingira mnachukua hatua gani.

"Hebu turudi kuangalia mkataba huu, makubaliano gani tunawekeana, siyo valvu mpya imetoka maabara imekuja ikawekwa hapa halafu ikajivusha gesi, hapana! Lazima tuje na majibu sahihi.

"Natambua wizara husika imefanya kazi yao na sisi tunaoratibu shughuli za mzingira, lazima tufanye kazi yetu," Sima alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Nemc, Prof. Chagu alisema ni muhimu kwa wataalamu kuhakikisha vifaa vinavyotumika vinakuwa na viwango vilivyoidhinishwa na mamlaka husika.

Prof. Chagu alisema matumizi ya vifaa vyenye viwango yatasaidia kuhakikisha matatizo kama la hivi karibuni la kuvuja kwa gesi, hatokei na kusababisha madhara kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai, alisema tukio la hivi karibuni la kuvuja kwa gesi lingesababisha madhara makubwa kama hatua za haraka zisingechukuliwa kudhibiti cheche za moto ambazo zilikuwa zinatokea.

Ngubiaga alibainisha kuwa, siku ya tukio, wananchi wanaotumia Barabara ya Kilwa, hasa waliosafiri kwa mabasi ya kwenda au kutoka Mtwara na Songea, waliathirika kutokana na kushindwa kuendelea na safari.

Alisema athari za kiuchumi pia zilionekana kutokana na kuzimwa kwa Kituo cha Umeme cha Kilwa kwa saa kadhaa kulikoathiri maeneo mengi ya mikoa ya Pwani, Lindi, Dar es Salaam na mingine inayotumia umeme wa mkondo huo.



Mafundi wa kampuni ya CRSG, wakiendelea na ujenzi wa barabara inayounganisha eneo la Kijitonyama na Sinza Uzuri, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wakulima walilia bei elekezi ya pembejeo

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

WAKULIMA wilayani Kalambo mkoani Rukwa, wamelalamikia kukosekana kwa pembejeo na bei elekezi katika msimu huu wa kilimo, hali inayotia hofu kutopata mavuno kutokana na wakulima wengi kulima bila kutumia pembejeo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wamesema kuwa hadi sasa pembejeo hazijafika wilayani humo na msimu wa kilimo umeshaanza. Mmoja wa wakulima hao, Samu Mwasomola, alisema kuwa kumekuwapo na changamoto ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kitendo kinachosababisha wakulima kutumia mbegu zisizo faa na zisizo na ubora.

Naye Edwini Mwasabwite aliiomba serikali kuwa na mazoea ya kuwahisha pembejeo kabla ya msimu kuanza kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata mazao mengi na kuondokana na adha ya kutumia pembejeo zisizo na ubora.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Nikoraus Mrango, alisema serikali imesambaza pembejeo za kilimo katika maduka yote yanayouza pembejeo sambamba na kutoa bei elekezi.

Alisema kinachofanyika sasa ni kukagua kama pembejeo hizo zinawafikia wakulima na kuwataka wakulima kutoa taarifa endapo kuna changamoto zinazowakabili. "Tutachukua hatua kali kwa mujibu wa sheria na kuna wauzaji wa pembejeo watakaobainika kukiuka taratibu wakati wa kuwauzia pembejeo wakulima," alisema Mrango.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Julieth Binyura, aliwataka watendaji wa halmashauri hiyo kufuatilia iwapo wanauza pembejeo za kilimo kwa bei elekezi.

Pia alisema wilaya inaendelea kusisitiza wakulima kulima kibiashara mazao mbalimbali ikiwamo alizeti na kahawa ili kuongeza wigo wa mazao yanayopimwa na kupunguza utegemezi kwenye zao la mahindi ambalo wakati mwingine bei yake haitabiriki.

Hivi karibuni, mkoa wa Rukwa ulizindua msimu mpya wa kilimo mwaka 2019/2029, ambapo unakusudia kulima hekta 603,637.13 za mazao mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na uhakika wa chakula.

## TTB yaja kivingine kutangaza utalii

**Na Romana Mallya**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) kwa kushirikiana na Kampuni ya Huduma za Usafiri wa Anga (NAS), wamesaini makubaliano ya kutangaza utalii uliopo Tanzania kupitia matangazo yatakayowekwa kwenye mabasi, runinga na vyumba vya abiria, viwanja vya ndege vya nchi za Afrika, Asia na Mashariki ya Kati.

Uzinduzi wa ushirikiano huo ulifanyika jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere Terminal 3.

Akizindua ushirikiano huo pamoja na gari lililowekwa matangazo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangalla, alisema sekta ya utalii inachangia pato la Taifa kwa asilimia 17.6 na kutoa ajira kwa asilimia 11.

"Sekta hii inaingiza asilimia 25 ya fedha za kigeni, hivyo ili iendelee kukua lazima tuwekeze na ndiyo maana Rais John Magufuli amefufua Shirika la Ndege la Tanzania ili kuisaidia," alisema.

Dk. Kigwangalla alisema imekuwa ikipokea wageni milioni 1.5 na kati yao watalii 900,000 hutumia usafiri wa ndege.

"Benki ya Dunia (WB) inaikadiria Tanzania ifikapo mwaka 2025 tunapaswa kupokea zaidi ya Dola za Marekani bilioni 16," alisema.

Dk. Kigwangalla alisema serikali imewekeza TTB ili waweze kutangaza na kuwafikia wateja wote duniani.

Alisema kwa sasa Tanzania imewekeza nchi za Afrika Mashariki na Mashariki ya Kati kama China, Urusi na sasa wameelekea nchi za Uarabuni.

"Ninazitaka kampuni binafsi za utalii zishirikiane na TTB ili wapeleke vifurushi vyao vitakavyoonwa na watalii kupitia NAS," alisema.

Balozi Costa Mahalu mwakilishi wa NAS akizungunza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, alisema wana jumla ya vyumba (kumbi) zaidi 40 Afrika, Asia na Mashariki na Kati na matarajio ni kufikia 50.

Alisema kampuni hiyo ya Nas inatoa huduma katika viwanja vya ndege 40 na matarajio ni kuvifikia vingine ili kuwa 100.

Naye, Mwenyekiti wa TTB, Jaji Thomas alisema bodi itatumia fursa hiyo wanayoingia katika nchi za Afrika, Asia na Mashariki ya Kati kutangaza utalii kwenye kumbi (lounges) za kusubiria ndege na magari ya watalii.

Alisema TTB iliona Nas imekidhi vigezo vya kushirikiana nao katika utangazaji utalii.

"Tunawaomba wanaotoa huduma kwa watalii waweze taarifa zao kwenye kumbi hizi," alisema.

# NMB yasaidia shule mil. 70/-

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA utaratibu wake wa kila mwaka wa kutumia asilimia moja ya pato lake la mwaka kwa miradi ya kijamii, Benki ya NMB imekabidhi misaada ya vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. miloni 70, kiasi kinachoifanya kufikisha jumla zaidi ya Sh. mil. 850 tangu mwaka huu uanze.

Misaada hiyo iliyotolewa wiki hii, ni kwa ajili ya shule za msingi, sekondari na zahanati wilayani Geita mkoani Geita na Halmashauri ya Morogoro mkoani Morogoro.

Hafla za makabidhiano ya vifaa hivyo, zilifanyika kwa nyakati tofauti, ambako Shule za Msingi Kilimani, Uhuru, Mchongomani, Shilabela na Nyakamwaga wilayani Geita, zilikabidhiwa madawati 274 yenye thamani ya Sh. mil. 25, yaliyopokelewa na Mkuu wa Mkoa huo, Robert Gabriel.

Katika hafla hiyo, Gabriel pia alipokea kutoka kwa Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Abraham Augustino, mabati 348 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Kaseme na Kituo cha Afya Butundwe wilayani Geita, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 10. Huku akiishukuru NMB kwa msaada huo, Gabriel pia alipokea vitanda sita vya wagonjwa, kikiwamo kitanda kimoja kwa ajili kujifungulia kinamama wajawazito, pamoja na mashuka 50 na magodoro matano vyenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa ajili ya Zahanati ya Kashishi.

Augustino alisema misaada iliyotolewa wiki ya jana, inaifanya NMB kutumia Sh. milioni 850 kwa shughuli za kijamii kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), ikiwa ni sehemu ya Sh. bilioni 1 (ambayo ni sawa na asilimia 1 ya pato la mwaka), ilyotenga kwa miradi ya kijamii.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada huo, hafla iliyofanyika katika Shule ya Msingi Kibwaya, Tarafa ya Mkuyuni, Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, msaada huo umekuja baada ya maombi yaliyotokana na idadi kubwa ya wanafunzi shule za msingi kukaa chini wakati wa masomo yao.

Katika Halmashauri ya Morogoro, Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Baraka Ladislaus, ndiye aliyekabidhi msaada wa benki yake kwenda kwa shule za Kibwaya, Bwakila Chini, Newland, Kinole na Mfumbwe, zilizopewa madawati 275 yenye thamani Sh. milioni 25.

Baraka aliwataka walimu na wanafunzi kwa kushirikiana na Kamati za Shule, kujenga utamaduni wa kutoa elimu ya namna ya kutunza madawati hayo.

"Tumetoa haya madawati 275 kwa shule tano na sisi kama NMB tutaona fahari kama madawati haya yanatunzwa na wanafunzi wa shule husika wakati serikali na wadau wanatafuta mbinu ya kumaliza changamoto ya upungufu wa madawati na kuhamia kwenye changamoto nyingine," alisema. Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, alisema kuwa wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari kutosita kuwachukulia hatua wazazi wa wanafunzi ambao watabainika kuharibu miundombinu, ikiwamo kuharibu madawati makusudi.

"Agizo lililotolewa na Waziri wa Tamisemi, Seleman Jafo kwa wakuu wa shule la kuwataka wazazi kuchukuliwa hatua baada ya kubainika mtoto wake ameharibu miundombinu ya shule, ikiwemo kuharibu madawati kwa makusudi, lazima lifanye kazi sasa," alisema Chonjo.

# Mwekezaji wa saruji akosa eneo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

OFISA Mipango Miji wa Manispaa ya Shinyanga, Salu Ndongo, amesema kutokana na kutokuwapo utengwaji wa maeneo ya uwekezaji mjini humo, kumesababisha mwekezaji wa kiwanda cha saruji kukosa eneo la kuweka. Alibainisha hayo juzi wakati akiwasilisha taarifa ya mpango wa mji mpya wa Shinyanga kwa watumishi wa serikali, ambapo mchakato wake ulianza tangu mwaka 2016, na hadi kufikia mwaka 2036 ndani ya miaka 20 ijayo, mji huo utakuwa umeshajengwa upya na kukua kimaendeleo.

Alisema kutokana na mji wa Shinyanga kutojengeka vizuri, kumesababisha kutokuwapo utengwaji wa maeneo ya uwekezaji, hali ambayo imekuwa ikisababisha baadhi ya wawekezaji kukosa maeneo ya kuwekeza.

"Mpango wetu huu wa mji mpya wa Shinyanga "Master Plan" ambao mchakato wake ulianza mwaka 2016 na hadi 2036 Shinyanga itakuwa mpya... tunatarajia kutenga maeneo ya makazi, taasisi za serikali, huduma za afya, maeneo ya biashara, yakiwamo na maeneo ya uwekezaji," alisema Ndongo.

"Hivi karibu tulipata mwekezaji wa kiwanda cha saruji, lakini kutokana na kutokuwa na maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya uwekezaji...tukamwambia hatuna eneo, lakini kama Shinyanga ingekuwa imejengeka toka zamani, kusingekuwapo na uhaba wa maeneo ya uwekezaji na ndio maana tunataka kuijenga upya," aliongeza.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, ambaye alikuwa mgeni rasmi na mwenyekiti wa kikao hicho, alipongeza mpango huo wa kuujenga upya mji wa Shinyanga, huku akitoa mapendekezo kuwa pale watakapokuwa wanatenga maeneo hayo, yakiwamo ya uwekezaji wasiweke karibu na kambi za jeshi.



Mmoja na mwanachama wa KCB Biashara Klabu, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Texas Hardware Ltd, Jonex Kinyonyi, akizungumza na wafanyabiashara katika hafla ya klabu hiyo, iliyofanyika jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi kudhibiti magonjwa ya wanyamapori kwa binadamu

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

KATIBU Tawala Mkoa wa Kigoma, Rashidi Mchatta, amewataka wananchi wa Wilaya ya Uvinza kutoa ushirikiano kwenye Shirika la Bushi to Base Solution (B2B), ambalo linashughulikia magonjwa kwa sokwe, wanyama wa majumbani na binadamu ili kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Akizungumza na wananchi wakati wa ufunguzi wa Shirika hilo katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Mchatta alisema, taasisi ilianzishwa zamani Marekani, lakini ilisajiliwa Tanzania mwaka 2017, na sasa itafanya shughuli zake katika mkoa huo hususan Wilaya ya Uvinza katika eneo la Hifadhi ya Taifa ya Mahale.

Aidha, alisema taasisi ina mradi ambao itautekeleza katika Wilaya ya Uvinza ni mradi wa kimkakati kwa upande wa hifadhi za Mahale ambao utazuia mlipuko wa magonjwa ambayo yanaweza kutokea kutokana na mchanganyiko wa mazingira, wanyamapori, wanyama wa nyumbani pamoja na watu ambao wanaishi katika mazingira yale.

Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mwanamvua Mlindoko, aliutaka mradi huo kuangalia maeneo yote ya kusini wilayani Uvinza kwa sababu maeneo hayo yanapakana na Hifadhi za Tanapa ambapo kuna wanyamapori aina mbalimnbali.

Mlindoko alisema wananchi waelimishwe juu ya mradi huo ili waweze kufuata yale ambayo wataalamu wanawaelekeza ili kujiepusha kupata maradhi ya magonjwa yanayohusiana na wanyama.

Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, Hasina Mwilima, alisema sokwe wana maradhi ambayo ni rahisi kumpata binadamu, hivyo mradi utasaidia wananchi kujuaa maradhi yanayotoka kwa wanyama kwenda kwa wanadamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa B2B, Dk. Tereza Sylvina, alisema mradi huo utaanza Desemba mwaka huu na utamalizika Desemba 2021, na lengo ni afya moja kwa wanyama aina ya sokwe, wanyama wa nyumbani na binadamu, na kuwa utakuwa katika hifadhi ya Mahale pamoja na vijiji vinavyozunguka katika hifadhi hiyo.

# Waungana kumalizia kero za kilimo mkoani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya taasisi 12 za utafiti wa kilimo mkoani Arusha, zimeungana kwa ajili ya kutafuta njia mbadala za kutatua matatizo yanayowakabili wakulima wa vijijini Wilaya ya Arumeru.

Akizungumza na watatifi hao, Katibu Tawala wa Wilaya ya Arumeru, James Mchembe, alisema, hatua ya kuwakutanisha watafiti hao, itasaidia kutatua matatizo yanayowakabili wakulima katika sekta ya kilimo wilayani humo.

Mchembe alisema, kitendo cha kuwakutanisha watafiti hao, kinalenga kuanzishwa kwa jopo la wataalamu wa kilimo ambao watapita vijijini kusikiliza kero za wakulima. "Nawapongeza kwa kufikia hatua hii ya kukutana na watafiti mbalimbali wa kilimo ambao kwa pamoja mmekuja na mwarobaini wa kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili wakulima hususani katika wilaya yetu ya Arumeru," alisema Mchembe.

Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii ya Tengeru, Dk. Bakari George, alisema Wilaya ya Arumeru ina taasisi nyingi za utafiti hivyo, ni wajibu wao kuungana na kuwa kitu kimoja kutatua matatizo ya ardhi yanayowakabili wananchi wilayani humo. Bakari alisema wilaya hiyo, ina tatizo la ufinyu wa maeneo ya kilimo ambapo imekuwa kero kwa wataalamu wa tafiti wanapotaka kutengeneza chombo kimoja kwa ajili ya kushughulikia kero katika sekta ya kilimo.

"Wote tunafahamu bila kuwa na takwimu hatuwezi kufanikiwa, hivyo sisi kama Chuo cha Maendeleo ya Jamii tumeona ipo haja ya kuwakutanisha wataalamu hawa ili kila mmoja aeleze ujuzi wake ambao utasaidia kuondokana na matatizo yanayowakabili wananchi vijijini," alisema.

Mtafiti Mwandamizi wa Viuatilifu na Visumbufu vya mimea kutoka Taasisi ya Utafiti ya TPRI, Maneno Chidege, alisema mabadiliko ya hali ya hewa yamekuwa tatizo kubwa lililosababisha kushuka kwa uzalishaji wa mazao sehemu nyingi nchini.

Aidha, yameleta njaa kwa wananchi kwa kuwa na hali ngumu kiuchumi, alisema na kuongeza kuwa kitaundwa chombo kimoja cha utafiti kitakachosaidia kutatua matatizo ya wakulima, huku akiwataka wananchi kwa kulima kilimo cha kisasa kwa kutumia eneo dogo, lakini linalozalisha kwa tija.



Mfanyabiashara wa matofali na bidhaa za ujenzi, akiziandaa kwa ajili ya kuwauzia wateja katika eneo la Florida, jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wamiliki ardhi waomba JPM awasaidie kupata haki yao

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAMILIKI saba wa viwanja katika eneo la Naura jijini Arusha, wamemuomba Rais John Magufuli, kuingilia kati mgogoro wa miaka 32, kati yao na Halmashauri ya Jiji la Arusha, ili wapate haki yao.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wamiliki wa viwanja hivyo, ambao ni pamoja na Issack Kassam, Manleo Auye, Joshua Kaiza Ndosi, Kanubhai Rameshner Patel na Akber Sanjani, walisema viwanja hivyo wanavimiliki kwa mujibu wa sheria na wana hatimiliki.

"Tunamuomba Rais Magufuli atusaidie tupate haki yetu tuliyoitafuta kwa muda mrefu kwani tumepita katika ofisi mbalimbali za umma tumekuwa tukizungushwa bila ya kupata msahada wowote,"alisema Sanjani.

wWalilalamika kuwa eneo lao linamilikiwa na nani? Tena kuna kampuni za kigeni zimekodishiwa sehemu hiyo.

"Chakushangaza maeneo yetu yamekodishwa kwa kampuni moja ya ujenzi kutoka China bila ya sisi kujulishwa wakati tunamiliki kisheria,"alisema Sanjani.

"Taarifa tulizonazo ni kwamba kampuni hii ya ujenzi inalipa kodi Sh.milioni 50, kwa mwezi tunataka kufahamu ni nani aliyekodisha eneo letu pia anayopokea kodi wakati wahusika tupo ,"alisema Ndosi.

Kwa mujibu wa nyaraka za umiliki wa eneo hilo, Halmashauri ya Jiji la Arusha iligawaa maeneo hayo kwa wananchi, kati ya mwaka 1986 na 1987 .

Kwa mujibu wa maelezo ya wamiliki wa viwanja hivyo, baada ya kupewa waliomba vibali vya kujenga na kuendeleza ardhi yao.

"Baada ya kuwa na mgogoro na halmashauri kila tulipojenga nyumba kwenye maeneo yetu nyumba zilibomolewa bila ya kupewa taarifa ,"alisema Ndosi.

Kwa mujibu wa nyaraka kutoka kwa wamiliki wa eneo hilo, kwenda halmashauri , Julai 25 mwaka 2019, walituma maombi ya kupewa vibali vya kujenga ukuta katika kiwanja namba 17,kitalu "U"sehemu F.

"Sisi wamiliki halali wa kiwanja tajwa hapo juu chenye namba 10258, ni muda mrefu sasa hatujaendeleza viwanja hivi kulingalina na mgogoro uliopo katika eneo hilo, hata hivyo tumekuwa tukilipa kodi ya serikali hadi leo,"

"Kwa barua hii tunaleta ombi kwako la kuomba kibali cha ujenzi wa ukuta kuzunguka eneo letu ili tuweze kuendelea na mipango iliyopo katika kiwanja bila ya kusumbuliwa," hii ni kwa mujibu wa barua.

Aidha, walisema baada ya mgogoro huo kudumu kwa muda mrefu mwaka 1996, walipokea barua ya kurejeshewa viwanja hivyo.

Mwaka 1999, Wizara ya Ardhi ,ilitoa agizo kwa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha,Mkurugenzi wa Halmashauri na Meya wa Jiji la Arusha kurudisha maeneo hayo kwa wahusika ili wayaendeleze.

"Viwanja hivi tuna hatimiliki kwa vipindi vyote tumeomba vibali vya kuviendeleza na kujenga lakini hatukupewa kilichotokea ofisi zote za serikali tulizopita kudai haki yetu wametuzungusha bila ya kutupa masahada wowote,"aliongeza Ndosi.

Hatimiliki hiyo inaonyesha kuwa wamiliki wa maeneo hayo, wameshailipa halmashauri ya Jiji la Arusha kodi hadi kufikia mwaka 2020.

# Waomba madarasa, nyumba za walimu

**Na Jaliwason Jasson,** MANYA

WANAFUNZI na walimu wa chuo cha ufundi stadi mkoani Manyara, wameiomba serikali kuongezea miundo mbinu ya madarasa, mabweni na nyumba za walimu ili kuwa na ufanisi wa utendaji kazi chuoni hapo.

Maombi hayo, yalitolewa mwishoni mwa wiki Mjini Babati, wakati wa mahafali ya sita ya chuo hicho.

Akisoma risala kwa mgeni rasmi Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, kwa niaba ya wahitimu wengine Wiston Mteka, alisema chuo hicho kinakabiliwa na tatizo vyumba vya madarasa, mabweni na nyumba za waalimu.

Alisema upungufu wa vyumba vya madarasa kwenye chuo hicho, umesababisha msongamano na mrundikano wa wanafunzi darasani.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa wanafunzi wa kike wamekuwa wakikumbana na tatizo la vishawishi kutoka kwa wanaume barabarani wakati wa kwenda na kurudi nyumbani.

Mteka alilitaja tatizo jingine kuwa ni uhaba wa nyumba za walimu unaosababishwa baadhi ya waalimu kukaa nje ya chuo na wengine kuchelewa vipindi.

Licha ya kuzungumza hayo, aliiomba serikali kutoa fursa ya kuwapatia mikopo ili waweze kufanya shughuli zao kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

Mkuu wa Chuo, Felix Olendukai, alisema chuo hicho, kinakabiliwa na tatizo la vyumba vya madarasa,nyumba za waalimu pamoja na ukosefu wa karakana nne.

Aliishukuru serikali kwa kuwapatia Shilingi milioni300, kwa ajili ya ujenzi wa karakana kubwa ambayo itawasaidia kufanya shughuli zao.

Mgeni rasmi katika mahafali hayo, Mkuu wa Wilaya ya Babati Elizabeth Kitundu, aliwataka wahitimu hao kuutumia ujuzi waliopata chuoni hapo kufanya kazi ili wajikwamue kiuchumi.

Alisema ujuzi walioupata utawasaidia kupata ajira huku akiwasisitiza wahitimu hao kufanya kazi kwa bidii ili wafikie malengo waliyojiwekea.

Akizungumzia suala la mikopo waliyoomba, Mkuu hwa Wilaya aliwataka wahitimu kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali ili kuomba mikopo inayotolewa na halmashauri kupitia mapato ya ndani.

Kitundu alisema serikali itatafuta njia mbadala ya kukabiliana na matatizo hayo, kulingana na bajeti zilizopitishwa katika vikao halali.

## Waanzisha maktaba maalumu kuongeza ufaulu

**Na Mary Mosha,** SIHA

WAKAZI wa Kata ya Karansi, wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro wameanzisha maktaba maalumu ya kujisomea ili kuongeza ufaulu katika mitihani ya kitaifa katika ngazi za msingi.

Diwani wa kata hiyo, Duncan Urassa, alisema hayo jana alipokuwa akieleza hali ya elimu katika kata hiyo.

Alisema kata hiyo ilipata bahati ya kujengewa maktaba kutoka ufadhili wa watu wa Marekani ili kuleta tija kwenye ufaulu ambao mpaka sasa bado unasuasua.

Kadhalika alisema jamii haioni umuhimu wa kusomesha watoto wao na badala yake hukimbilia kuchunga mifugo au kuolewa, jambo linalowalazimu kutumia sheria kuwabana ili kuhakikisha mtoto anapata haki ya msingi kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

''Jamii ninayoiongoza kiukweli haipendi shule au kujisomea licha ya mazingira rafiki yaliyowekwa na serikali ya awamu ya tano hivyo inatulazimu sisi kutumia sheria ili kuwabana… lakini tunaomba taasisi nyingine ambazo zinaweza kuja kuhamasisha elimu kwa kushirikiana na kata wafike ili kuhakikisha vijana wanipenda elimu," alisema.

Wakati huo huo, diwani huyo aliiomba serikali vyumba vipya vya madarasa katika Shule ya Msingi Kandash kutokana na vilivyopo kuwa chakavu.

"Shule ya Sekondari Karansi bado ina upungufu wa walimu hususani na mchepuo wa Sayansi na kuonyesha mwamko wa elimu chumba kimoja cha darasa kimejengwa kwa nguvu za wananchi katika Shule ya Msingi Lekrumun," alisema.

Mzee wa kimila Ezekeeli Moleli katika kata hiyo, alisema uelewa mdogo wa wazazi wa umuhimu wa watoto kupata elimu ndiyo sababu ya kutowapeleka watoto wao shuleni.

"Sisi jamii ya wafugaji tulikuwa nyuma katika kupeleka watoto wetu shule, kutokana na uelewa mdogo, lakini kuanzia sasa tumeelimika na tutahakikisha wanasoma kwa ajili ya kuongeza ujuzi na maarifa katika ulimwengu wa sasa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alinukuliwa wakati wa uchimbaji wa msingi wa Shule ya Sekondari ya Biriri kuwa uhai wa maendeleo ni kuwekeza katika elimu na hawatamvumilia mtu yeyote atakayekuwa tayari kukwamisha mipango ya maendeleo hasa katika elimu.

"Kwa yeyote atakayebainika kwa makusudi kuzuia elimu kusonga mbele au kumkatisha mwanafunzi masomo, serikali ya wilaya haitasita kumchukulia hatua kali za kisheria ili kuleta tija kwenye uchumi wa kati," alisema.



Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Kilimanjaro, Vicent Lyimo (kulia), akimkabidhi Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Salum Hamdun, gari aina ya Noah yenye thamani ya Sh. milioni 14 kwa ajili ya kusaidia kutoa elimu ya usalama barabarani kwa shule za msingi na sekondari pamoja na vijiwe vya waendesha bodaboda, katika hafla iliyofanyika, mjini Moshi jana. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# Abiria wasiodai risiti sehemu za vyakula kutozwa faini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MENEJA wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, amewataka abiria wote wanaosafiri kwenda mikoani, kudai risiti wanapofika katika maeneo ya kununua vyakula.

Alisema abiria wengi hawana tabia ya kuchukua risiti wanapopewa huduma jambo ambalo ni kinyume na sheria na taratibu za nchi. "Tayari tumetoa matangazo mbalimbali ya kuwataka abiria kuhakikisha wanachukua risiti wanaposimama kwa ajili ya kujinunua vyakula na ununuzi mwingine kwa kuwa baadhi ya maofisa wetu wapo huko na wanaendeleza na operesheni maalumu hasa katika maeneo ya Korogwe, Mombo, Babati na Singida," alisema.

Alisema baadhi ya maofisa wa TRA wako katika maeneo hayo kwa ajili ya ukaguzi wa matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki za (EFD) na atakayekutwa na hatia adhabu ni faini ya kuanzia Sh. 30,000 mpaka Sh. 1,500,000 kwa mnunuzi asiyedai risiti ya huduma au bidhaa. Elias Sichuma, ni dereva wa mabasi makubwa anayefanya safari zake Moshi - Morogoro, alisema elimu kwa wamiliki wa maeneo ya vyakula na abiria inahitajika pamoja na madereva kuhakikisha wanatoa elimu kwa abiria kabla hawajashuka kupata huduma hiyo.

"Mimi nashauri hata kama wanahitaji kufanya msako wa maeneo hayo kwa ajili ya kufuata sheria na taratibu za nchi, lakini upo umuhimu wa kuhakikisha wanatoa elimu...wanaweza kuweka wataalamu ambao watatoa elimu kwa njia ya matangazo ili kusaidia wasioelewa," alisema.

Mmoja wa abiria, Adelina Mmari, anayetoka Moshi kwenda Dodoma, alisema ipo haya ya kutolewa matangazo kwa wingi ili kuepusha adhabu kwa watu wasio na hatia.

"Madereva wasaidizi wote wa magari ni vyema wakatoa tangazo mara abiria wanapofika katika maeneo ya chakula ili kukumbushana mara kwa mara kuisaidia serikali ukusanyaji wa mapato," alisema.

# Mgombea CCM aahidi kutekeleza ilani

**Na Mary Mosha,** MWANGA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, amesema wananchi hawakipa chama hicho ushindi kwa sababu sio wanakiogopa bali wanakiamini katika kuwatumikia na kuwaletea maendeleo.

Mabihya alitoa kauli hiyo jana katika kijiji cha Mbambua wakati wa kampeni za kumnadi mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbambua kilichopo Kata ya Lembeni, wilayani Mwanga.

Alisema Chama Cha Mapinduzi kinaongozwa na ilani yake yenye lengo la kuwatumikia wananchi.

Alifafanua kuwa wagombea wa nafasi mbalimbali katika chaguzi za sasa za serikali za mitaa maeneo mengi wamepita bila kupingwa kutokana na kuaminika na wananchi.

"Wananchi wanawachagua wagombea wanaotokana na CCM sio kwa sababu wanakiogopa chama hapana ni kwa sababu wanaona kwa macho jinsi kinavyopambana na matatizo yao na tutaendelea kuwatumikia wananchi," alisema Mabihya.

Katibu huyo alisema kuwa ili Ilani ya uchaguzi itekelezwe vizuri ni lazima viongozi wa chini wa serikali za mitaa kuongea lugha moja ya maendeleo na kuwataka wananchi kuwachagua viongozi wanaotokana na CCM.

Katika hatua nyingine, Mabihya aliwataka wananchi wote waliojiandikisha kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa kujitokeza kwa wingi Novemba 24, kutimiza haki yao ya kikatiba kwa kumchagua kiongozi wanayemtaka awaongoze.

Diwani wa Kata ya Lembeni, Godwin Mmbaga, alisema Kijiji cha Mbambua ni miongoni mwa vitano vinavyopatikana katika kata ya Lembeni, lakini kinaongoza kwa kuwa nyuma kimaendeleo na kuwaomba wananchi kumchagua Willium Mvungi ili washirikiane katika kuleta maendeleo.

Mmbaga alisema, kijiji hicho kina shule moja ya msingi ambayo ni Mbambua, lakini kuliikuwa na tatizo la kuanguka kwa jengo moja la darasa kutokana na kuwa chakavu na kuwatafuta wananchi wa kijiji hicho wanaoishi nje ya Mbambua kuchangishana na kujenga chumba hicho cha darasa.

Naye mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbambua kupitia CCM, Mvungi alisema kuwa, nia yake ya kugombea nafasi hiyo ni kuwaletea wananchi maendeleo na kuahidi kushirikiana na diwani kusimamia Ilani ya uchaguzi itekelezwe.

Aliwaahidi wananchi kusimamia mapato ya kijiji yanayotokana na ushuru wa mchanga ili yawanufaishe wananchi wa kijiji hicho pamoja na kutumika kwa shughuli za maendeleo.



Neno la Profesa Beno Ndulu kwa digitali mpya duniani, sera zake

Ukurasa 19

UCHUMI



## Alivyonusurika kutoka ndoa ya kitoto, akahamishiwa kuwa fundi cherehani

Ukurasa 14


# BUFE

Ijumaa Novemba 22, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




# Mkulima aliyegeuka mafanikio ya kipekee kupitia kilimo cha mlimani

Ukurasa 16


UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

# Alivyonusurika kutoka n akahamishiwa kuwa fund

- Baba akiri kuchukua 'advansi' na ng'ombe
- Baba analipa vya watu, mtoto safari Veta
- Gazeti liliibua, wanaharakati wakafanya kazi



Mwalimu Theresia Masinga, wa mafunzo ya ubunifu wa mavazi na ushonaji nguo, katika chuo cha Veta, Shinyanga, akimwelekeza Binti Nchambi.

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA,**

HUYU ni mtoto aitwaye Nchambi mwenye umri miaka 17, lakini si jina lake halisi. Ni mkazi wa Maganzo wilayani Kishapu Mkoa wa Shinyanga, aliyenusurika kuozeshwa ndoa ya utotoni na kuhamishiwa maandalizi ya kuwa mfanyabiashara, fundi cherehani.

Anayeonyeshwa kidole katika tuhuma hiyo ni baba yake mzazi, Lyuba Seif. Leo hii, mtoto huyo leo hii ana ufadhili wa masomo ili kutimiza ndoto zake.

Binti huyo alikuwa mbioni kuozeshwa mnamo Juni mwaka jana, na baba mzazi alishakuwa tayari kampokea mahari ya ng'ombe watano na fedha taslimu Sh. 300,000.

Hilo linaelezwa kufanyika pasipo binti huyo kujua kilichoendelea dhidi yake, kwani aliishia kushuhdia ng'ombe wapya zizini, alikuwa na maoni zimenunuliwa na baba yake.

Baada ya ndoa hiyo kutibuliwa, baba huyo ilibidi arudishe ng'ombe alizochukua ukweni na kubaki na deni la Sh. 300,000, huku akisubiri mtoto huyo atimize umri wa miaka 18 mwaka ujao, ili ndoa ihitimishwe aweze kupata mali za kumkwamua kiuchumi.

**APATA UFADHILI**

Baada ya kuripoti taarifa hiyo, Septemba 10 mwaka huu, hatimaye binti huyo alipata ufadhili wa kuanza masomo katika Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta), katika chuo cha mkoani Shinyanga.

Katika hilo, huko anaelezwa ameingizwa katika fani ya ushonaji nguo kwa matarajio itamsaidia kutimiza ndoto zake za kujikwamua kimaisha.

Meneja Mradi wa Huduma za Msaada wa Kisheria, kutoka Shirika la (PACESH) mkoani Shinyanga, John Shija, anasema wameguswa na tukio la binti huyo kutaka kuzimwa ndoto zake kwa kuozeshwa na babaye, ndipo wakaamua kumfadhili katika masomo ya ufundi.

Anasema, katika nafasi yao ya usaidizi wa kisheria, kamwe hawakubaliani na matukio hayo ya ndoa za utotoni kuendelea kuwapo Shinyanga, ndio maana wakaguswa na tukio hilo waliloliochukulia hatua, sasa mhudika ni mwanafunzi wa bweni- Veta.

"Shirika letu lilikaa na mzazi wake na kukubaliana tumpeleke chuo cha ufundi. Tutamfadhili masomo yake hadi pale atakapomaliza na ataishi kwenye hosteli za chuoni," anasema Shija na kuendelea:

"Akimaliza masomo yake tutampatia mtaji wa kuanza maisha, pamoja na kumnunulia cherehani huku tukiendelea kumsimamia hadi pale atakapoanza kujitegemea.

"Tunaomba wazazi mkoani Shinyanga waachane kabisa na tabia za kuozesha watoto wao ndoa za utotoni, bali wawasomeshe ili wapate kutimiza ndoto zao, ambao watakuja kuwasaidia baadae na kuwanunulia hiyo mifugo ambayo wanaitaka."

**BINTI AFUNGUKA**

Binti huyo anasema, kwa sasa anajisikia amani na huru baada ya kupata ufadhili huo wa masomo na ataweza kutimiza ndoto zake zilizotaka kuzimwa na mzazi, kwa hitaji la mifugo.

> **"Umri wangu wa kuolewa ulikuwa bado na nilikuwa sitaki kabisa kuolewa, kwa sababu nilikuwa sijatimiza ndoto zangu... kwa bahati nzuri ndoa yangu ikatibuliwa na sasa naendelea na masomo na mshukuru sana mwenyezi Mungu," anasema Nchambi.**

Anaahidi kujitahidi masomoni ili apate umahiri katika fani ya ushonaji nguo, afikie lengo la kuwa fundi mzuri, ikimfungulia mlango wa kuendesha maisha binafsi na wazazi wake.

"Umri wangu wa kuolewa ulikuwa bado na nilikuwa sitaki kabisa kuolewa, kwa sababu nilikuwa sijatimiza ndoto zangu... kwa bahati nzuri ndoa yangu ikatibuliwa na sasa naendelea na masomo na mshukuru sana mwenyezi Mungu," anasema Nchambi.

"Baada ya kuingia hapa chuoni ndani ya wiki mbili tu, sasa hivi nimeshaanza kukata nguo, jambo ambalo ni jema kwangu na nina imani nitakuja kuwa fundi mzuri wa kushona nguo, nitawasaidia na wazazi wangu," anaongeza.

**BABA MUOZESHAJI**

Seif Lyuba, baba wa binti huyo, katika kauli ya kuwa ameelimika na kubadilika, anawashukuru wafadhili waliojitokeza kumsomesha mtoto wake huyo na anaanika siri alitaka kumuozesha kutokana na kukosa fedha za kumpeleka chuo cha ufundi, mara baada ya kutovuka elimu ya msingi.

> **"Tunaomba wazazi mkoani Shinyanga waachane kabisa na tabia za kuozesha watoto wao ndoa za utotoni, bali wawasomeshe ili wapate kutimiza ndoto zao, ambao watakuja kuwasaidia baadae na kuwanunulia hiyo mifugo ambayo wanaitaka."**

Anasema, kwa sasa hana tena mpango wa kumuozesha binti yake huyo. Kwa mujibu wa mpango wa awali, alilenga hilo kufanyika mwaka ujao, akilenga binti kufikisha umri wa miaka 18, kutokana na hadi sasa anadaiwa Sh.300,000, licha kurudisha ng'ombe watano aliyopewa awali.

"Sina mpango tena wa kumuozesha binti yangu. Nimeridhia aendelee na masomo yake ya chuo cha ufundi na fedha Sh. 300,000 ambazo bado nadaiwa ukweni, itanibidi nifanye maarifa ya kuzirudisha, kwa sababu nilikuwa nimeshazitumia kufanya maandalizi ya harusi," anasema Lyuba.

**CHUONI VETA**

Theresia Masinga ni mwalimu wa fani ya ubunifu wa mavazi na ushonaji nguo kutoka Chuo cha Veta, mkoani Shinyanga, anasema tangu alipoingia binti huyo chuoni hapo kuanza masomo, binti amekuwa na bidii ya kupenda kujifunza.

Kaimu mkuu wa chuo cha ufundi

# ndoa ya kitoto, di cherehani



Jengo la utawala la chuo cha Veta, Shinyanga. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

stadi veta mkoani Shinyanga, Mangu Mabelele, anaeleza binti huyo itamchukua muda wa miezi sita kufahamu kabisa ushonaji nguo.

Anatoa wito kwa wazazi mkoani Shinyanga, kuacha tabia ya kuozesha watoto wao, hasa wanaopata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza, wapelekwe katika vyuo vya elimu ya ufundi, ili wapate ujuzi utakaowasaidia kutimiza ndoto zao.

"Binti huyo tumempokea chuoni hapa mara baada ya taratibu zote kumalizika, na anaishi bweni na sasa anaendelea na masomo yake kama kawaida ya kujifunza namna ya kushona nguo, ujuzi ambao utamsaidia kutimiza ndoto zake," anasema Mabelele.

**ALIVYONUSURIKA**

Tedsony Ngwale ni Katibu wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Serikali wa Kupunguza Ukatili wa Kijinsia Dhidi ya Wanawake na Watoto Mkoani Shinyanga, (MTAKUWWA), anasema baada ya taarifa ya mtoto huyo kunusurika kuolewa kupitia vyombo vya habari, walichukua hatua ya kwenda kuzungumza na mzazi wake na kumuonya.

Gazeti la Nipashe, ndilo lililotoa taarifa ya kuwapo mpango wa binti aliyenusurishwa kuolewa mkoani Shinyanga, hata zikaanza kufuatiliwa na mamlaka za umma.

Ngwale anasema, walipofika kwenye kaya hiyo waliwachukua wazazi wa binti huyo na kuwapeleka katika kituo cha Polisi, kisha wakaandikishana mkataba wa kutomuozesha tena, hata kipindi chote binti atakapkuwa masomoni, ili afanikiwe kutimiza ndoto zake.

"Navishukuru sana vyombo vya habari kwa kuandika habari hii, kwa sababu hata sisi tulikuwa hatulijui tukio hili la binti kutaka kuozeshwa na mzazi wake. "Tumelisoma kwenye gazeti la Nipashe, ndipo tukachukua uamuzi wa kulifuatilia na kwa bahati nzuri tukamkuta binti amepata ufadhili wa masomo.

"Baada ya kupata taarifa hiyo ya ufadhili wa masomo ya binti huyo, ikatubidi tumchukue baba yake na kwenda naye kwenye kituo cha Polisi ili kuandikishana naye mikataba ya kumtombugudhi tena, bali amuache aendelee na masomo yake." anasema.

Ngwale anataja takwimu za ndoa za ututoni Mkoa wa Shinyanga, kwa mwaka wa fedha uliopita Juni iliyopita, kuna watoto 32 walio na umri chini ya miaka 18 walishaolewa.



Binti Nchambi, mkazi wa Maganzo wilayani Kishapu, akiwa masomoni katika chuo cha Veta, Shinyanga.



Aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Kenya, Amos Wako. **PICHA: MTANDAO**

## Wako ang'aka dai la ufisadi marufuku kuingia Marekani

MWANASHERIA mkuu wa zamani wa Kenya, Amos Wako, amepinga vikali hatua ya Marekani kumpiga marufuku yeye na familia yake kuingia nchini humo.

Wako anasema hatua hiyo ni kufufua kesi ya zamani ambayo haelewi lengo lake lilikuwa nini. Anasema:"Kwa miaka nane sijakuwa serikalini. Tangu nilipostaafu japo visa vya ufisadi vimekithiri mno, jina langu halijatajwa au kuchunguzwa kuhusiana na visa vya ufisadi."

Anaeleza kushangaa marufuku ya kutosafiri Marekani, anayoiona kwa mara ya kwanza, huku akijitetea hata kutajwa jina lake kwa 'hili na lile' ni matokeo ya kazi yake ya zamani kama Mwanasheria Mkuu wa Kenya.

Wako anaitaka Marekani kutoa ushahidi wa madai dhidi ya vidole vya ufisadi kwake anavyonyooshewa, akisema: "Badala ya kukabiliana na ufisadi, wanafufua visa vya zamani ambavyo havina msingi wowote.'

Mwanasheria Mkuu huyo anaitaka Marekani kutoa ushahidi wa madai kwake, akisema ni mara ya pili sasa kauli za namna hiyo dhidi yake.

Kwa mujibu wa Waziri wa Marekani Mike Pompeo, marufuku hiyo ni kwa sababu ya Wako kuhusishwa na 'ulaji rushwa na ufisadi.' Hata hivyo, taarifa hiyo haikueleza kwa kina ni rushwa au ufisadi upi alihusika navyo.

Hatua ya Marekani kumpiga marufuku Wako, inachukua sura mpya, baada ya Mkuu wa tume ya EACC, Dk, Eliud Wabukala, aliyenukuliwa na vyombo vya habari vya Kenya, akisema tume imekuwa mstari wa mbele kutoa habari na maelezo kuhusu ufisadi kwa Marekani na balozi za kigeni.

Wadadisi wa mambo wanasema huenda vikwazo vya usafiri vinavyomkumba Wako, vilitokana na kashfa ya kifedha ya Anglo Leasing, iliyosababisha serikali ya Kenya kupoteza mabilioni ya pesa.

Kashfa hiyo iliibuka wakati Wako alipokuwa kazini katika nafasi hiyo ya kisheria na alinyooshewa kidole cha lawama kwa madai ya kuwa kizuizi katika uchunguzi wa sakata hilo.

Mwaka 2009, aliyekuwa Naibu Waziri nchini Marekani, Johnnie Carson, aliyezuru nchini Kenya, alitangaza kwamba Bwana Wako amepigwa marufuku kuzuru Marekani kwa madai amekuwa kikwazo kwenye vita dhidi ya ufisadi, Kenya.

Hatua ya sasa ya kuwanyima vibali vya kusafiri Wako, mkewe Flora Ngaira na mtoto wake, Julius Wako, inamaanisha hawawezi kuzuru Marekani au kufanya biashara na kampuni za Kimarekani.

Tume ya Kupambana na Ufisadi ya Kenya (EACC) kupitia kwa Mwenyekiti, Eliud Wabukala, ilieleza imeshirikiana kwa kiasi kikubwa na wachunguzi wa Marekani, iliyozaa marufuku hayo.

Wadadisi wanadai, huenda matatizo ya Wako yalitokana na sakata ya Anglo Leasing iliyohusu kandarasi za usalama zenye thamani ya mamilioni ya dola na serikali ilipoteza fedha hizo zinazoaminika ziliishia kufichwa katika mataifa ya nje.

Wako alikuwa mwanasheria mkuu wa Kenya kwa muda wa miaka 20, kati ya mwaka 1991 na 2011. BBC

UCHUMI

# Mkulima aliyegeuka mafanikio ya kipekee kupitia kilimo cha mlimani

- Abuni umwagiliaji wa visima vya aina yake
- Halmashauri ilimpika, leo shamba darasa

**Na Mary Mosha, MWANGA**

NI takribani umbali wa kilomita 80 kutoka iliko stendi kuu ya mabasi ya mjini Moshi, hadi nyumbani kwa mkulima mbunifu, Nzinyangwa Elieneza (60).

Hapo ni kijijini Vucha Ndembwe, katija Kata ya Shingatini katika tarafa ya Ugweno, wilayani, Mwanga. Ni sfari inayoanza saa moja asubuhi hadi saa tisa alasiri.

Mara inapokamilika kulima, anayejisifu, licha ya kuishi milimani ambako wengi wameshindwa kujiendeleza kwenye kilimo, binafsi yuko upande wa pili wa mafanikio.

Hapo linaibuka swali, kwanini hivyo? Elieneza hafichi ukweli, kwamba inatokana na elimu aliyopewa na Halmashauri ya Wilaya Mwanga, iliyomfanya aamue kupafanya milimani, sehemu sahihi ya kilimo.

Anapataja kuwa sehemu sahihi inayompa kipato, sanjari na mazao kujikimu na familia yake. Anaendelea:“Baada ya kupata mafunzo ya kilimo cha matuta, nilianza kupiga matuta katika eneo nililoachiwa na marehemu baba yangu.”

Elieneza anataja ukubwa wa matuta hayo: “Mwanzo wa shamba hadi mwisho wa shamba, wenye ukubwa wa mita 45 kwa mita ‘nne- nne’ yapatao 70, ambayo yananisaidia kukabiliana na mmomonyoko wa udongo.”

**UMWAGILIAJI MILIMANI**

Elieneza anataja mazao yake ni mchanganyiko, zikiwamo kahawa, mbegu kutoka taasisi ya utafiti ya TaCRI, hiliki, mboga, maharage, mahindi na viazi na hatagemei maji ya mvua, kwa sababu hayatabiriki.

Anaendelea kuwa ili kukidhi mvua zisizotabirika, inamlazimu kuchimba kisima shambani, kina cha mita 900, lengo ni kujikwamua kiuchumi.

Ni eneo analolitafsiri linajenga ulazima mkulima anunue mipira na vinyunyuza mrashi, kwa ajili ya kumwagilia wakati wote, ili kuwapo uhakika kwa mwaka maji kupatikana

Anakiri vinyunyiza mrashi hivyo alivyovitengeneza wastani wa miaka 20 sasa, vimewasaidia wengi, wakiwamo wakulima.

“Nimeanza kutengeneza vinyunyuzi mrashi toka mwaka 1994 ambavyo vimeweza kunisaidia mimi mwenyewe pamoja na wakulima wenzangu. Nimekuwa nikipata oda mbalimbali kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro ila nakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mtaji,” anafafanua.

Anasema, kuwapo maji ya uhakika kunamsaidia mkulima, kulima mazao mbalimbali, ikiwamo mboga mboga kahawa na hiliki kuanzisha vitalu vya miti kwa ajili ya kuotesha na kuendelea kulinda uoto wa asili, hasa milimani.

**CHANGAMOTO**

Mkulima Elieneza, anasema mitaji kwa sasa ni tatizo kwao, kutokana wakulima wengi hawakopesheki na kwenye taasisi za fedha, hali inayowakwaza washindwe kujiendeleza na kulima kikamilifu, katika matokeo bora kuelekea uchumi wa kati.



Mkulima Nzinyangwa Elieneza, akiwajibika shambani na uhalisia wa matunda ya kazi zake. **PICHA ZOTE: MARY MOSHA.**

> **“Mimi nalima mazao mbalimbali ikiwemo hiliki na kahawa, lakini bado hatujapata soko la uhakika kuuza mazao yetu, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na bei elekezi kwa muda wa mazao hao hali inayofanya wachuuzi kufika maeneo yetu na kutulangua,” anasema.**

“Mimi nalima mazao mbalimbali ikiwemo hiliki na kahawa, lakini bado hatujapata soko la uhakika kuuza mazao yetu, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na bei elekezi kwa muda wa mazao hao hali inayofanya wachuuzi kufika maeneo yetu na kutulangua,” anasema.

Elineza anasema, hiliki inastawi mlimani na licha ya kukosa soko la uhakika, baadhi ya wachuuzi huzunguka waliko wakulima kununua kwa bei ndogo isiyomnufaisha mkulima.

“Tunasikia zao la hiliki lina soko kubwa nje ya nchi.. Lakini sisi hatuna uwezo wa kufika huko, hivyo tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa zao hili kama mazao mengine ya kimkakati,” anasema.

Elieneza ana maoni kwamba, kuna haja ya kupatikana njia ya kuanzisha ushirika wa zao hilo, ili kumsaidia mkulima kuepukana na wachuuzi wanaozunguka kwenye makazi ya wakulima.



**KILIMO CHAKE**

Anataja mavuno na bei iliyopo, ni kwamba katika kila shina la mti wa hiliki, kuna uwezo wa kupata kilo mbili na zinapokuwa mbichi na kilo moja na nusu, inapokauka, ambayo sasa inayouzwa Sh. 10,000 kwa kilo.

Kwa mujibu wa mkulima huyo, ni ishara kwamba hiliki bado ina soko, iwapo itaweka mkono katika kuliangalia zao ili kumsaidia mkulima.

“Wapo wananchi ambao hawajawahi kuiona hiliki ikiwa shambani,” anasema Elieneza na kuuendeleza ufafanuzi: “Mche wake upo kama wa mgomba. Unapaswa kuchukua na kuuweka kwenye shimo la upana wa futi moja na nusu, kwa urefu wa futi moja, unachanganya udongo na mbolea na kisha kuupanda nche huo,”

Anasema, ili mtu aweze kupata mavuno ya kwanza, ni lazima mmea wa hiliki ichukue miezi 18 na baada ya hapo, mlimaji atakuwa na uwezo wa kuchuma mara kwa misimu wa mwaka mmoja.

**RAI YAKE**

Anasema, katika kilimo milimani kuna changamoto nyingi kutokana na mambo kama gharama za upatikanaji maji, milimani kutofikika kirahisi.

Ombi lake serikalini ni kuangaliwa uwezekano wa kuweka miundombinu rafiki na kutoa elimu zaidi kwa wakulima kutoa kipaumbele cha kilimo.

Anafafanua: “Yapo mazao ya kimkakati yaliyopewa kipaumbele na serikali, tunaomba Wizara ya Kilimo, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, kuangalia soko la hiliki nje ya nchi au kuwaalika wawekezaji katika kujenga kiwanda.”

“Kitakachosaidia wakulima kuacha kuuza malighafi na kuyaongezea thamani, lengo ni kumkomboa mkulima ,” anasema.

**MAJIRANI NAO**

Elizabeti Mzava, ni mkulima jirani, anayesema kuwapo kwa mkulima Elieneza, kumeleta mabadiliko makubwa kwa baadhi ya wakulima kijijini. Ana ombi la kuangaliwa uwezekano kutumiwa wenye ujuzi jirani, na badala ya wataalamu kutoka vyuoni wasio na uzoefu.

“Baadhi ya wataalamu wa kilimo wanaokuja, wamezoea kukaa ofisini, wanapofika kwa wakulima wanageuka ‘mzigo’ hali inayofanya wakulima kupata hasara za mbegu, mbolea na viatilifu, bila ya kupata matokeo chanya,” anasema

Mariam Mchome, anasema baadhi ya watendaji wa kiserikali wilayani Mwanga, wanakwamisha jitihada za serikali ya sasa, kwa kuwanyima ushirikiano wakulima pindi wanapowahitaji.

Anasema, Mwanga ni wilaya inayopata mafuriko kila mwaka na kupatiwa misaada kila mara kutoka serikalini na anaushari mwelekeo mpya sasa kwamba:

“Tumechoka, tumeamua kuongeza nguvu maeneo ya milimani, lakini tunakwamishwa na wataalamu kutoka halmashauri. Tunaomba wataalamu kutoka Wizara ya Kilimo kufika na kutusaidia elimu.”

Ofisa Mtendaji wa Kitongoji cha Vanja, Jeremiah Mfinanga, anasema mkulima Elieneza, ameleta tija kwa wenzake, kwani kazi yake imekuwa shamba darasa kwa watendaji na wakulima wengine.

“Ni ukweli usiopingika kuwa mkulima huyo amekuwa mbunifu hasa katika kulima kilimo cha umwagiliaji katika maeneo,” anasema

Ofisa Kilimo wa Mkoa Kilimajaro, Simon Msoka, anasema jitihada za mkulima huyo ni za kuigwa, huku uamuzi wa wataalamu kilimo limeshafanyiwa kazi.

“Wataalamu wetu wana elimu ya kutosha na tutaomba wakulima kuwapa ushirikiano kwa ajili ya matokeo bora zaidi kwenye sekta ya kilimo,” anasema Msoka.

## BIASHARA KATIKA PICHA




Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, Simon Karikari, akizungumza katika Mkutano wa 19 wa Taasisi za Kifedha nchini, uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Godfrey Simbeye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mamalishe akimrudishia chenji mteja wake baada ya kumuuzia chai katika eneo la kata ya Daraja mbili, jijini Arusha jana, **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Kinamama wa kimaasai wachuuzi wa maziwa wakisubiri wateja katika eneo la kwa Mathias, wilayani Kibaha, Mkoa wa Pwani hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

BIASHARA



Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Injinia Mshamu Munde,akiwa katika moja ya majukumu. Chini, mkazi wa Mkuranga na wanawe, wakibangua korosho baada ya kuzichoma. **PICHA: YASMINE PROTAC.**

# Mwenyekiti Mkuranga aanika sasa 'korosho na wao, wao na korosho'

## • Kangomba wako katika 'ole wao'

**Na Yasmine Protace**

MKURANGA hivi sasa iko katika wilaya zinazobeba majina makubwa kitaifa. Sababu kuu mi moja, kwamba mbali na kuwa na aradhi yenye rutuba, ina sifa ya ziada kwamba ni moja ya wenyeji waandamizi wa sera za Rais Dk. John Magufuli, kutoa fursa ya ujenzi wa viwanda.

Ni uamuzi ambao hauishii katika mikakati tu, la hasha! Tayari viwanda vinajengwa na si muda mrefu sana Rais Dk. Magufuli alikuwa huko kuzuru kuona viwanda vyake.

Ikirejewa katika kilimo nako si haba. Mkuranga, ambako pia ni njia ya barabara kuu kuelekea mikoa ya Kusini; Lindi, Mtwara hadi baadhi ya wilaya za mkoa wa Ruvuma kama vile Tunduru.

Hapo ni kiunganishi cha kwanza cha mikoa wa Pwani na Dar es Salaam, ikiendelezwa na majirani za kimkoa, wilaya za Kibiti na Utete ambayo ndio jirani mkuu wa mkoa Lindi.

Mkuranga na majirani zake hao wa Pwani, hadi kuendelea mikoa ya Lindi na Mtwara, korosho zimesheheni kila upande, huku Mkuranga nao walishaliweka kuwa zao lao la kimkakati.

Wakazi wa Dar es Salaam, ambao wametawaliwa na itikadi ya 'ardhi ni mali' kasi yao ni kubwa kuelekea huko, kama ilivyofantyika katika siku zilizopita katika maeneo jirani au ndani ya wilaya za mkoa Pwani; Bagamoyo, Kibaha na Kisarawe.

Katika lugha rahisi, hadi sasa Mkuranga inazidi kuwa 'mali' na 'mjini' ingawaje kunakamatwa pia na mvuto wa shughuli za kilimo.

Hiyo ni tofauti na zamani, Mkuranga wakati huo ikiwa sehemu ya Wilaya ya Kisarawe, hadi mwaka 1990, haikuwa hata na shule ya sekondari ya umma, bali ikivuma kwa maeneo yake kama kituo cha mpaka wa barabarani; Jaribu mpakani na Pori la Vikundi.

Vivyo hivyo, maeneo kama Kiparang'anda ilikuwa na ushuhuda wa mabasi aina ya Cocabs, yalifanya usafiri na eneo hilo kati yake na Dar es Salaaam.

**NENO HALMASHAURI**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Juma Abeid, anasema kuna jumla ya wakazi zaidi ya laki mbili kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012, ina kata 25, vijiji 125 na vitongoji 475, zao lao kuu la biashara ni korosho.

Pia, anataja mazao mengine wilayani ni pamoja na nanasi, mihogo, korosho na maembe.

Abeid anasema, korosho inayolimwa na jumla ya wakulima 15,496 mpaka sasa. idadi ya kilo zilizokusanywa za korosho katika msimu uliopita zaidi ya kilo milioni tisa.

Pia, anasema matarajio katika kilimo hicho cha korosho ambacho kazi ya maandalizi inaendelea, ni kuvuka zaidi makusanyo yaliyopita, kwa kuwa na jumla ya kilo milioni 10 za korosho na halmashauri imejipanga kuhakikisha lengo linafikiwa vizuri.

Anatoa angalizo kwa wote watakaothubutu kwenda kinyume na malengo, hatua kali zitachukuliwa na anafafanua: "Tumejipanga kuhakikisha kila mkulima ananufaika na alichovuna, lakini mtu yoyote akijaribu kuharibu mfumo huu, hatua kali za kisheria dhidi yake zitachukuliwa."

> **"Anatoa angalizo kwa wote watakaothubutu kwenda kinyume na malengo, hatua kali zitachukuliwa na anafafanua: "Tumejipanga kuhakikisha kila mkulima ananufaika na alichovuna, lakini mtu yoyote akijaribu kuharibu mfumo huu, hatua kali za kisheria dhidi yake zitachukuliwa."**

**DC MKURANGA**

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Philiberto Sanga, amewataka viongozi wa Vyama vya Msingi (AMCOC) kuzingatia mwongozo wa utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, ili kuepuka sintofahamu kwa wakulima wa korosho, kama ilivyokea katika msimu uliopita.

Akifungua mafunzo kwa vyama hivyo, aliwataka washiriki kuwa makini na mafunzo hayo na akawataka kuyafanyia kazi, hatimaye uwe mwarobaini wa kumaliza changamoto mbalimbali kwa wakulima.

Sanga, aliyewakilishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mhandisi Mshamu Munde, alitumia fursa hiyo kuwaonya viongozi hao kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atayekwamisha malipo ya korosho kwa wakulima katika msimu wa sasa.

Ni agizo alilolielekeza pia kwa walanguzi wa korosho wa kupitia 'Kangomba' anawatangazia kwa kauli "watafute kazi nyingine ya kufanya' ili kuepuka mkono sheria katika enedo hilo la ununuzi wa korosho.

Mkuu wa Wilaya anaviambia vyama vya ushirika, ambavyo kimsingi ni wateja wa mazao yao kutoka shambani, kwamba wakulima wao wananufaika na zao hilo waweze kuinua kipato chao.

" Vyama vya ushirika vinatakiwa kuhakikisha wakulima wananufaika Kwa kuinuka kiuchumi kutokana na wao kuwatambua wakulima," anasema.

Anaongeza kwamba, wakulima wanatumia muda mwingi katika kuzihudumia korosho mpaka hatua ya uvunaji na atakayehujumu mfumo huo, ajiandae kuchukuliwa hatua za kisheria.

Pia, Munde anawataka wakulima kutokuwa tayari kurubuniwa na wajanja wachache, cha msingi kwao ni kuwa wepesi na weledi kufuata taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kunufaika na zao hili.

"Nitashangaa kuona pale mlipohangaika kutunza mashamba na hatimaye mkafanikiwa kuvuna korosho, lakini mwisho wa siku mkazipeleka kwa walanguzi," anasema.



UCHUMI

# Neno la Profesa Beno Ndulu kwa digitali mpya duniani, sera zake

## • Mwelekeo wa uzalishaji, soko na bima

Na Nimi Mweta



Profesa Benno Ndulu. **PICHA;MAKTABA.**

ALIYEKUWA Gavana wa Benki Kuu(BoT) nchini, Profesa Benno Ndulu anasema kuna eneo jipya ya kumulika katika uchumi kwa jumla, ambalo ni umuhimu kwa nchi zinazoendelea.

Hilo ni kujenga taswira ya zinakotaka kufikia na njia ya kujijengea Teknomaha ya Habari na Mawasiliano au (teknohama) katika uchumi.

Nchi zinazoendelea zinahitaji ramani mapema ya teknohama katika uchumi ujao, ili kutumia fura zinazotokana na teknohama, kuitumia kuleta mageuzi ya teknolojia katika uchumi.

Ametoa mtazamo huo wakati wa kujadili ripoti ya tume ya kitafiti yenye uhusiano wa karibu na Benki ya Dunia, iliyozinduliwa siku moja baadaye jijini Nairobi.

**TEKNOLOJIA SHIRIKISHI**

Ripoti hiyo inatoa mchanganuo wa kuweka ramani ya kidigitali kwa nchi zinazoendelea, kuona jinsi gani zinaweza kusonga mbele. Imetayarishwa na Tume ya Kubuni Njia Mpya za Maendeleo (Pathways to Prosperity Commission) ambayo suala muhimu la kutafiti ni teknolojia na maendeleo shirikishi.

Maelezo yake katika kuweka wazi kilichomo katika utafiti huo, ina umuhimu zaidi kuhusu uchumi kwa jumla kuliko hata lengo lake la teknolojia yenyewe.

Anatoa mfano, nchi zinazoendelea ni lazima zijitahidi kuongeza thamani katika kilimo kwa kujaza upungufu katika mtiririko wa thamani na kuunda njia mpya za kuingia katika mtiririko wa tija katika soko la dunia.

Hiyo inaweza kufikiwa kwa kuhakikisha mawasiliano ya haraka na masoko, kwa kuchambua jinsi ya kutumia urahisi wa mawasiliano na kufanya vizuri katika soko la ushindani duniani.

Profesa Ndulu, anagusia jinsi biashara ya kimataifa kwa sasa inafika hatua ya kuhamisha utoaji huduma kwa wawekezaji au wajasiriamali wa ndani na nje na kuingiza sehemu kubwa ya mahitaji kijamii katika huduma zinazoweza kuendeshwa kibiashara.

Profesa Ndulu anasema, huduma tofauti za kiuchumi na kijamii zinaonyesha huduma za kiuchumi na kijamii zinachangia asilimia 50 ya uchumi wa dunia kwa jumla,wakati viwanda vinachangia asilimia 16 ya thamani katika uchumi wa dunia.

Ni takwimu ambayo ilikuwa haijawahi kutajwa katika hadhara ya kisomi au kisera hapa nchini, na hivyo inaweza kuleta tija.

Anataja mfano wa kuunganisha sekta isiyo rasmi na sekta rasmi kupitia teknohama, inavyofanya kazi kupitia mpango wa kutoa huduma za bima kwa waendesha pikipiki kibiashara 'bodaboda.'

Profesa Ndulu, anaeleza hicho ni kielelezo cha majukwaa ya kidigitali, yanayounganisha wanaohitaji huduma na watoaji na ili nchi zifikie lengo hilo, inabidi ziwe tayari kidigitali, chembe ambayo ni muhimu sana katika mchakato huo wa uwezeshaji.

Anasema hilo linabidi lijikite katika uhalisia wa nchi katika digitali, ikiangalia umakini wa wale wanaoweza kufaidika au kuachwa nyuma katika mtiririko wa thamani unaohusishwa.

Utafiti ulilenga kuangalia nchi zinavyoweza kuchukua upana wa ubunifu na maboresho ya huduma pana zinazopatikana katika teknohama na huduma zilivyo kidigitali kwa jumla .

Anasema, linaonyesha jinsi nchi zinazoendelea zinavyoweza kujikita katika mtiririko huo na kujengea thamani ya wanachofanya.

**UKARIBU SOKONI**

Suala la kujenga ukaribu na masoko kwa huduma za kidigitali ni kielelezo kimojawapo, wakati kupatikana bima kwa kundi kama 'bodaboda' ni kielelezo kingine na anasema hapana shaka kuna makundi yanayohitaji kuduma hizo, hata kama hazifahamu moja kwa moja.

Ziko jitihada katika sekta ya tiba kuwa na bima za kulipia kwa michango midogo kila wakati (kwa mfamo mwezi mmoja) kukamilisha kiwango, ili kila mtu awe na bima, asipate tabu endapo ugonjwa unamfikia na watu wake wa karibu zaidi katika familia.

Profesa Ndulu, anasisitiza katika suala la kuchochea maendeleo kwa kutumia nyenzo za kidigitali, hakuna 'kiatu kinachofaa kwa wote' ila kila nchi itafute usawa inakoweza kuingia na kupanua wigo la matumizi ya dijitali kwa ufanisi na tija zaidi.

Hata hivyo, anasisitiza umuhimu wa serikali kuwa ncha ya majadiliano kijamii, kuhusu nini kinawezekana au kifanyike, kwani haiwezekani nchi kuchukua kutoka nje sera za teknohama, bila kuwa na sheria na kanuni wezeshi zinazoenda na mazingira yake (baadhi wataita muktadha) katika nchi husika.

Kuweza kutunga sheria kama hizo na kufafanua kanuni zinazohitajiwa, inabidi kwanza kuwapo maafikiano kitaifa kati ya makundi ya wadau, kutaka nini hasa kifanyike.

Majadiliano katika semina hiyo yaligusia kuwa nusu ya dunia kwa mara ya kwanza, itakuwa imefikiwa na teknohama mwaka huu.

Hapo kuna ujumbe kwamba, nusu ya watu wote duniani watakuwa wanatumia 'simu janja' au kompyuta kwa mawasiliano na kupokea taarifa kwa njia mbalimbali.

Kupatikana sera zinazofaa katika eneo la teknohama, nako kutawezesha mabadiliko ya teknolojia yatumike kwa maendeleo ya wote na siyo wachache peke yao.

Endapo nchi zitazembea kutafuta mbinu bora za kuingia katika utoaji huduma kidigitali katika nyanja tofauti za uchumi, hali hiyo itapanua pengo liliko kati ya nchi tajiri na maskini na ndani ya nchi.

Jambo la msingi katika maelezo ya Profesa Ndulu, ni kutafiti ni uwiano kati ya huduma za kibiashara (kijamii na kiuchumi) na viwanda katika maendeleo ya nchi na kupatikana ajira.

**TOFAUTI KISEKTA**

Kuna tofauti kubwa kati ya sekta inayotoa asilimia 50 ya pato la dunia na inayotoa asilimia 16, na inavyoelekea hali hiyo haitabadilika hivi karibuni, na si ajabu pengo liongezeke.

Maana yake ni kwamba, katika sera za serikali kunahitajika kulenga maboresho ya mazingira ya kutoa huduma, ambayo kimsingi yanahitaji uwezeshaji kupitia sera za kodi, kwani zinapokuwa kubwa, zinavuruga uwezo wa kumudu ushindani na kupandisha bei ya bidhaa.

Hisia ni kwamba, watoa huduma siyo wazalishaji na mkazo wote uwekwe katika uzalishaji siyo sahihi, kwa sababu viwanda vichache kimataifa na ndani ya nchi vinatosha kwa mahitaji ya kila siku ndani na nje ya nchi.

Haina maana kuwa viwanda siyo sera, ila ichukuliwe kwa uangalifu kama sehemu ya kutoa huduma, iachiwe wajasiriamali wenye uhakika wanachofanya.

Hivyo mkazo wa sera uendelee kuwa ni kuwapo mazingira wezeshi iwe ni huduma au viwanda, si kupanga idadi ya viwanda.

> “
> **Ziko jitihada katika sekta ya tiba kuwa na bima za kulipia kwa michango midogo kila wakati (kwa mfamo mwezi mmoja) kukamilisha kiwango, ili kila mtu awe na bima, asipate tabu endapo ugonjwa unamfikia na watu wake wa karibu zaidi katika familia.**

BIASHARA

HITAJI LA USHIRIKA...

# Mkulima anavyoteketezwa na dhuluma toka kwa msimamizi

Na Sabato Kasika



Shughuli za kilimo zikiendelea shambani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

KILIMO cha kibiashara kina nafasi kubwa ya kuchagiza maendeleo ya kiuchumi kwa mkulima mmoja mmoja na jambo linalowezekana kupitia ujenzi bora wa vyama vya ushirika vya msingi nchini (Amcos).

Hilo linawanfanya wakulima na hasa wadogo, wasibaki nyuma katika kunufaika na fursa kupitia vyama vya ushirika vya msingi, ndivyo ni tegemeo la kila mkulima.

Vyama hivyo ndivyo vinavyotakiwa kuwapa wakulima wadogo msaada wa kufungua milango ya masoko na kuna wakati ndio wanakuwa wateja wenyewe.

Pia, kuna maeneo ya kiufundi, kifedha, teknolojia ya kisasa na kuwajengea uwezo, katika kuboresha kilimo cha kibiashara, ili wafaidike nacho.

Hata hivyo, kumekuwapo migogoro kwenye baadhi ya vyama hivyo, huku chanzo chake kikiwa ni wanachama wakiwamo viongozi kuwaibia au kuwadhulumu wakulima fedha zao zinazotokana na mazao.

Kwa mazingira kama hayo, baadhi ya wananchi wamekuwa wakishindwa kujiunga katika vyama hivyo wakihofia kuibiana au kudhulumiwa na kulazimika kuendesha shughuli zao nje ya ushirika.

Vyama vya ushirika vinasajiliwa na kuendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013. Katika kutekeleza majukumu yake, vyama hivyo vinapaswa kuhakikisha vinatoa huduma stahiki kwa wanachama wake kwa kuzingatia sheria, kanuni na masharti yao.

Amcos, pia zinatakiwa kujiwekea mikakati ya kutekeleza mipango yake ya kiuchumi na kijamii ya muda mfupi na mrefu. Kwa mujibu wa Sheria inayoongoza uendeshaji wake.

Viongozi wake wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao huchukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kuwaondoa katika nafasi zao, lakini pale inapoonekana wamejihusisha na vitendo vya wizi, ubadhirifu au vitendo vinavyohusiana na matumizi mabaya ya nafasi zao, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika huchukua hatua zaidi za kisheria; ikiwamo kuwafikisha katika vyombo vya dola.

Pamoja na kuwapo maelekezo hayo, ambayo pia yanahimizwa na serikali, inaonekana bado kuna viongozi wa Amcos, ambao wameamua kufumba macho na kuziba masikio na kuendelea kudhulumu wakulima.

Inaweza kuelezwa kuwa, viongozi wa Amcos wa aina hiyo ni wanaoshindwa kusoma ishara za nyakati na sasa baadhi yamejikuta wakikumbana na vyombo vya dola.

Mfano mmojawapo ni viongozi 99 wa vyama ushirika vya msingi 31 kutoka mkoa wa Lindi, walionaswa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kwa tuhuma za kuibia wakulima wa ufuta Sh. bilioni 1.2.

Taarifa iliyotolewa hivi karibuni vya vyombo vya habari na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John mbugo, inasema hatua hiyo inatokana na agizo la Rais John Magufuli.

> “Pamoja na kuwapo maelekezo hayo, ambayo pia yanahimizwa na serikali, inaonekana bado kuna viongozi wa Amcos, ambao wameamua kufumba macho na kuziba masikio na kuendelea kudhulumu wakulima.

Rais alitoa agizo hilo mwezi uliopita akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Ruangwa mkoani Lindi na kumtaka Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Takukuru kuhakikisha vyama hivyo vinawalipa wakulima, kabla ya msimu wa korosho wa mwaka kuanza.

Kwa mujibu wa taarifa ya Takukuru kwa vyombo vya habari, watuhumiwa wamehojiwa na kukiri, wakakubali kurejesha fedha zote kabla ya kumalizika mwaka huu wa 2019 na kwamba hadi sasa wamesharejesha Sh. milioni 255.

Takukuru inasema, fedha hizo ni sehemu ya zile, ambazo watuhumiwa walidhulumu wakulima wa ufuta, na pia serikali inahakikisha zote zinarudi na kuwakabidhi wakulima wote waliodhulumiwa.

Wakati mkoani Lindi wakishikiliwa viongozi 99, kuna taarifa nyingine kutoka mkoani Mtwara kuwa viongozi 50 wa vyama vya ushirika mkoani humo wanashikiliwa na Takukuru, kwa tuhuma za ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni moja za wakulima wa korosho za msimu wa mwaka 2016/ 2017.


Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mtwara, Enock Ngairo alikaririwa na vyombo vya habari kwamba viongozi hao ni kutoka vyama mbalimbali vilivyopo katika wilaya zote za Mkoa wa Mtwara.


Ngairo anasema, viongozi hao wamechunguzwa na kubainika na makosa ya kuwaibia wakulima kwa kuwadanganya kuwa fedha zao hazijafika, huku zikiwa zimefika na wanazitumia kwa manufaa yao.

Udhaifu wa aina hii usipodhitiwa unaweza kuua ushirika, uendeshaji ushirika wa kama huo ni chanzo cha migogoro na unasababisha wanachama kujitoa wanapobaini kudhulumiwa fedha zao.

Wito wa jumla ni kwamba, hivi sasa wanachama wa ushirika kuwa makini katika uchaguzi wa viongozi wao, jambo litakalomuondoa kwenye lengo lao kujinufaisha badala ya kuimarisha ushirika, ambao ni manufaa jumla.








Mbunge wa Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya, Haroon Pirmohamed (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 120 kwa Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, kwa ajili ya sare za wanafunzi waliofaulu darasa la saba mwaka huu, katika hafla iliyofanyika wilayani Mbarali juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mil. 120/- kuwashonea sare waliofaulu la saba

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANAFUNZI 4,800 waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu wilayani Mbarali, watashonewa sare za shule kabla ya kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, ambapo zaidi ya Sh. milioni 120 zitatumika kwa kazi hiyo.

Fedha hizo zilitolewa juzi na Mbunge wa Mbarali, Haroon Pirmohamed, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Mei 2, mwaka huu mbele ya Rais John Magufuli wakati wa ziara yake wilayani Mbarali.

Akikabidhi hundi ya fedha hizo kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya jana, Pirmohamed alisema uamuzi huo wa kuwashonea sare wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu una lengo la kuunga mkono jitihada za Rais Magufuli ambaye anaendelea kusomesha bure wanafunzi wote nchini kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne.

Alisema katika fedha hizo kila mwanafunzi aliyefaulu atashonewa sare zenye thamani ya Sh. 25,000 na kukabidhiwa kabla ya kuanza masomo ya kidato cha kwanza Januari mwakani.

"Fedha hizi nimeona nizikabidhi kwa mkurugenzi ili aone namna nzuri za kuhakikisha kila mwanafunzi aliyefaulu na kuchaguliwa kuingia kidato cha kwanza mwakani anashonewa sare yake ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yangu niliyoitoa mbele ya Rais Magufuli alipotembelea wilaya yetu," alisema Pirmohamed.

Alisema anayafanya hayo sio kwa lengo na kujipatia sifa au kujinufaisha kisiasa, bali ni kuwekeza kwa vijana wa kitanzania ambao wanatarajiwa kuwa nguvukazi ya taifa katika siku zijazo.

Akipokea hundi hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alionya kuwa fedha hizo zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na kuahidi kumwandikia Rais barua kumjulisha kuhusu utekelezaji wa ahadi hiyo.

Aliitaka Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kushirikiana na wananchi kukamilisha haraka ujenzi wa vyumba vya madarasa vinavyohitajika ili wanafunzi wote waliofaulu waanze masomo Januari mwakani.

"Naagiza jitihada ziongozwe katika ujenzi wa vyumba vya madarasa ili wanafunzi hawa pamoja na kupewa sare waweze kuanza masomo kwa wakati Januari mwakani," alisema Chalamila.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema Wilaya ya Mbarali alisema wilaya yake ina upungufu ya vyumba vya madarasa 54 kwa ajili ya wanafunzi wanaotarajiwa kuanza kidato cha kwanza mwakani.

Alisema wananchi kwa kushirikiana na halmashauri wameshaanza ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa ambavyo mpaka sasa viko katika hatua mbalimbali za ujenzi. "Kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi ambao wamefaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu, tuna upungufu wa vyumba vya madarasa 54, lakini tayari tumeshaanza kuchukua hatua za kutatua changamoto hiyo na hivi sasa ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa unaendelea na upo katika hatua mbalimbali," alisema Mfune.

Aidha, alisema kuwa msaada ambao umetolewa na mbunge, utasaidia wanafunzi wengi hasa watoto wa masikini kuanza masomo kwa wakati ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

## Vijiji asilimia 83 vyapata umeme

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 83 ya vijiji vya Mkoa wa Mbeya vimepitiwa na huduma ya umeme, kupitia wakala wa nishati vijijini (REA), huku lengo la serikali likiwa ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2021 kusiwapo na kijiji ambacho hakina umeme.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja, Shamu Lameck, wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na utekelezaji wa umeme vijijini kupitia REA awamu ya tatu, awamu ya kwanza.

Alisema katika utekelezaji wa Mpango huo, jumla ya vijiji 140 vimeunganishwa na umeme katika awamu ya kwanza ya REA awamu ya tatu na kufanya mkoa wote wa Mbeya kufikia asilimia 83 ya utekelezaji wa usambazaji umeme vijijini.

"Katika awamu hii, tulilenga wateja 7,549 wawe wameunganishiwa umeme na hilo tumefanikiwa, lakini tumefanikiwa kufunga transifoma 168 katika mtandao wa umeme vijijini wenye urefu wa kilomita, 332, hayo ni mafanikio makubwa sana katika awamu hii ya kwanza," alisema.

Aliwataka wananchi kulinda miundombinu ya REA, ambayo imeegeshwa au kusimikwa kwa ajili ya kupitisha mradi wa umeme ikiwa ni pamoja na kukubali kupisha miundombinu hiyo ipite katika maeneo yao ili serikali iweze kukamilisha kazi hiyo haraka kwa ajili ya maendeleo yao.

# Rungwe kujenga viwanda mazao matano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WILAYA ya Rungwe imejiwekea malengo ya kushirikiana na sekta binafsi kuanzisha viwanda vya kusindika mazao matano, ambayo yanazalishwa kwa wingi ndani ya wilaya hiyo ili kuyaongezea thamani na kuinua uchumi wa wakulima.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa eneo la Katumba, Kata ya Ibigi wilayani humo. Alisema wilaya hiyo inayo mazao makuu matano ya kibiashara ambayo yanauzwa nje ya wilaya hiyo yakiwa ghafi na hivyo kufifisha uchumi wa wakulima na kupoteza mapato ya halmashauri.

"Wilaya yetu inayo mazao makuu ya kibiashara yapatayo matano, lakini kwa bahati mbaya tunauza mazao mengi yakiwa ghafi hali ambayo tunadhani inatukosesha mapato tunayostahili, tunaamini kuwa kama tukiamua kuongeza thamani ya mazao yetu kwa kujenga viwanda vya kuyasindika tunaweza kuongeza kipato kuanzia kwa wakulima mpaka mapato ya halmashauri zetu," alisema Chalya.

Chalya aliyataja mazao hayo ni chai, kahawa, parachichi, kakao na maziwa, ambayo alisema sehemu kubwa ya mazao hayo yanauzwa nje ya wilaya hiyo yakiwa ghafi hali ambayo inayafanya yasiwe na thamani nzuri.

Alisema wilaya hiyo ina viwanda viwili vya kusindika chai, kuna kiwanda cha parachichi na sasa ujenzi wa kiwanda cha kusindika maziwa unaendelea na uko katika hatua nzuri. Alisema jitihada za wilaya hiyo kwa sasa zinaelekezwa kuandaa maandiko na kuwashawishi wawekezaji kufika wilayani Rungwe kuwekeza kwenye viwanda vya kusindika kahawa na Cocoa ili mazao hayo nayo yaweze kuongezwa thamani ndani ya wilaya hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Ezekiel Mwankota, alisema kuwa wananchi wa Rungwe wanachohitaji ni kuona mazao yao yanaongezewa thamani ndani ya wilaya hiyo pamoja na kupata soko la uhakika.

Alisema wakulima wanalazimika kuuza mazao yao kwa bei ndogo kutokana na mazao hayo kuharibika haraka, na kwamba wakipata viwanda vya kuyasindika mazao hayo yatakuwa na uwezo wa kuhifadhiwa kwa muda mrefu bila kuharibika na hivyo kuuzwa kwa bei nzuri kwa vile yatakuwa na uwezo wa kusafirishwa kwenda kwa wateja walio mbali bila kuharibika.

"Kuna mazao kama vile maziwa, yanakaa kwa muda mfupi tu yaharibika, hivyo wakulima wanalazimika kuyauza kwa bei ya chini ili yauzikwe mapema, lakini tunaamini kuwa tukipata kiwanda cha kuyasindika na kuyaongezea thamani yapata bei nzuri kwa vile pia yatakuwa na uwezo wa kukaa muda mrefu bila kuharibika," alisema Mwankota. Alisema endapo mazao ya wakulima yataanza kusindikwa wilayani humo, yatakuwa na manufaa makubwa kwa vile pia viwanda hivyo vya kusindika mazao vitatoa ajira kwa wananchi na pia mabaki ya mazao hayo pia yatatumika kwa kuzalisha bidhaa nyingine kama vile chakula cha mifugo na hivyo kuwa na faida kubwa kwa wakulima.



HABARI DODOMA

# Asasi zaliomba Bunge kubadili sheria kandamizi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASASI 12 zinazojishughulisha na kutetea haki za wanawake wajane kupewa urithi wa ardhi, zimeliomba Bunge kuwaunga mkono katika kampeni hiyo kwa kubadili sheria kandamizi.

Ombi hilo limetolewa jijini hapa na Ofisa Programu wa Asasi ya Tanzania Land Alliance (TALA), Jamal Kafumbee, wakati wa mkutano na Kamati ya Bunge ya Maliasili na Utalii.

Kafumbee aliwaomba wabunge kusaidia kuwatetea wanawake hasa wajane ambao hukatazwa kumiliki ardhi pale wanapofiwa na waume zao.

Alisema sheria nyingi za kimila zimekuwa zikitoa ardhi kwa wanaume au watoto wa kwanza wa kiume, lakini hazitoi ardhi kwa wanawake wafiwa na hata watoto wa kike ambao nao wanastahili kupewa.

"Wakati wa ukoloni mfumo uliruhusu wanaume pekee kumiliki ardhi, lakini sasa kwa msaada wa wabunge mnaweza kusaidia kutoa elimu katika majimbo yenu ili kupigania na wanawake wakawe wanamiliki ardhi," alisema Kafumbee.

Ofisa Programu Mwandamizi kutoka Hakiardhi, Joseph Chombola, alisema baadhi ya sheria bado zinawakandamiza wanawake na kukataza kupewa ardhi mara waume zao wanapokuwa wamefariki. Alisema ni vema elimu ya usawa iendelee kutolewa kwa makabila mbalimbali ili waweze kutambua suala hilo.

Alisema kuna baadhi ya makabila ambayo wanaume wanaruhusiwa kumiliki ardhi, yanakataza wanawake hata kuuza ardhi bila idhini ya waume wao kitendo ambacho kinawanyima haki kuwa na uhuru na uamuzi kuhusu ardhi.

Alisema kutokana na sheria kandamizi, hata kamati za vijiji zinazotoa mamlaka kuhusu umiliki wa ardhi, kutokana na kuongozwa na wanaume, zimekuwa hazitendi haki mara suala la watu wawili wanapoachana wamekuwa wakiwapendelea wanaume.

Alisema mila na desturi katika baadhi ya makabila hasa yanayoongozwa na wanaume zaidi ya asilimia 85 yamekuwa yakiwamilikisha wanaume ardhi, lakini asilimia 15 inayobaki ndiyo yamekuwa yakiwamilikisha wanawake mara waume zao wakifariki.

Alisema yote hayo yamechangiwa na tamko la kimila la mwaka 1964 ambalo linampa haki mwanaume kumilikishwa ardhi na mwanamke kumnyima na hivyo kuwafanya waendelee kukosa haki hiyo.

Mbunge wa Babati Mjini, Paulina Gekul, alisema hivi sasa watoto wa kike wanatakiwa kupewa haki ya kumiliki ardhi kwani wana haki hiyo na sheria zinazowabagua zinatakiwa kuangalia upya.

Alisema atashangaa kuona familia za wasomi wa karne hii wanashindwa kuwarithisha ardhi watoto wao wa kike, kwani familia nyingi zinazaa watoto wa kike hivyo ni haki kumilikishwa.

Naye Mbunge wa Korogwe Mjini, Timotheo Mnzava, alisema elimu inatakiwa kuendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali hasa katika ngazi za vijiji ambako mabaraza ya vijiji yamekuwa yakiwanyima haki wanawake pamoja na kuwapo wanawake wawakilishi.

Akifunga mafunzo hayo, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Shaban Shekilindi, alisema wabunge wamesikia ombi la asasi hizo watafanyia kazi kwa kuendelea kutetea haki hizo.

Lakini alisema walishazungumza na Waziri wa Ardhi kuhusu haki za wanawake kumilikishwa ardhi hasa wajane ambao baada ya waume zao wakifariki wanafukuzwa, na kwamba mikakati inaendelea ili kuliweka vizuri suala hilo.



Waziri Mkuu wa Bunge la Vijana 2019, Alvin Festus, akijibu maswali kutoka kwa wajumbe wakati wa mkutano wa sita, kikao cha nne cha Bunge hilo, katika Ukumbi wa Msekwa, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Wenye ulemavu waitwa uchaguzi mitaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU wenye ulemavu nchini wametakiwa kujitokeza kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Jumapili ili kuunga mkono dhamira iliyoonyeshwa na Rais John Magufuli ya kuwajali na kuwashirikisha kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Foundation for Disabilities Hope, Michael Salali, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema Rais Magufuli tangu aingie madarakani ameonyesha upendo wa hali ya juu kwa watu wenye ulemavu kwa kuwateua kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika serikali yake.

Alitolea mfano baadhi ya viongozi hao kuwa ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia watu wenye ulemavu, Stela Ikupa, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Abdallah Possi.

"Ndugu zangu walemavu huu ndio wakati wetu, tujitokeze kumuunga mkono Rais wetu ambaye ameonyesha kututhamini sisi walemavu, tujitokeze kuchagua viongozi watakao 'address' changamoto zetu, na sio kuchagua viongozi matumbo," alisema.

Alisema katika uchaguzi huo viongozi wanaofaa kuchaguliwa ni watakaolipeleka Taifa mahali ambapo litakuwa na uwezo wa kujitegemea, na hilo linapaswa kufanywa kuanzia viongozi wa ngazi za chini watakaohamasisha wananchi kufanya shughuli za maendeleo.

"Tunataka ifike mahali hii nchi tutoe misaada nje, na hili tayari Rais Magufuli ameshaonyesha mwanga kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa kwa fedha zetu wenyewe za ndani," aliongeza.

Salali alimpongeza Rais Magufuli, kwa kujaribu kuunganisha makundi yote ya watu kwenye jamii bila kujali tofauti zao. "Tunapoona mambo mazuri yanafanyika tusikae kimya, tujitokeze kumtia moyo kwa kuwa amethubutu na tumwombee kwa Mungu ili yote aliyopanga kwa ajili yetu yaweze kufanikiwa," alisema Salali.

Aidha, aliwakemea watu wanaomkwamisha Rais kwa njia mbalimbali kutekeleza mipango yake na kusisitiza kuwa kama jamii, viongozi wa dini hawanabudi kuwaonya watu hao.

# Kampeni Dodoma ya kijani yaanzishwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma kwa kushirikiana na kitengo cha mazingira, katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Wakala wa Misitu (TFS), wameanzisha kampeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Hayo yalibainishwa juzi jijini hapa na ofisa mazingira wa Jiji la Dodoma, Ally Mfinanga, alipokuwa akizungumza na wanahabari jiji hapa.

"Halmashauri yetu ya Jiji la Dodoma, imeanzisha kampeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani kwa kutoa elimu kwa jamii ya wakazi wa Dodoma kupanda miti na kutunza mazingira na namna ya utunzaji na kuheshimu vyanzo vya maji," alisema.

Aidha, alisema elimu hiyo ni pamoja na kuonya vitendo vya ukataji miti, kuchunga mifugo na kufanya shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji ambavyo vinaweza kusababisha kuwapo kwa jangwa.

Alisema kitengo hicho kinafanya uhamasishaji kwa jamii jinsi ya kuona umuhimu wa upandaji miti na utunzaji wa mazingira pamoja na faida zake.

Alisema Dodoma imekuwa ikitafsiriwa kama sehemu ya jangwa kutokana na baadhi ya jamii ya wakazi kutokuona umuhimu wa kutunza mazingira ambapo walio wengi wamekuwa wakikata miti bila kupanda jambo ambalo ni hatari.

Alisema kutokana na Dodoma kuwa makao makuu ya nchi, ni lazima iwe ya kijani kwa maana ya kuwa na miti ya kutosha ambapo kila mwanakaya awe na miti isiyopungua 10 hadi mitano ya matunda na kivuli.

"Katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira tumeandaa vikundi mbalimbali vya ngoma na maigizo kutembea kila kata kwa ajili ya kutoa elimu na kuhamasisha kwa kupitia nyimbo, mashairi, ngoma na michezo mbalimbali," alisema.

"Aidha tunawapa elimu juu ya umuhimu wa miti ya matunda mfano, mtu akiwa na miti ya matunda anaweza kula matunda kwa afya yake yeye na familia yake na jamii iliyomzunguka na anaweza kuuza na kujiongezea kipato cha familia," alisema.



# Makali Sheria ya Habari yaanza kubana waandishi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga marufuku kwa asiyekuwa mwandishi wa habari kufanya kazi hiyo au kujihusisha na uandishi wa habari, utangazaji au uhariri.

Kadhalika, imesema kuwatumia watu wasiokuwa na taaluma ya uandishi wa habari kufanya majukumu hayo katika vituo vya redio na televisheni hata za mtandaoni ni kwenda kinyume na sheria.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo Zanzibar, Dk. Juma Muhammed, alisema kwa mujibu wa Sheria Namba 5 ya Mwaka 1988 ya Magazeti, Vitabu na Mawakala wa Habari, kifungu cha 39 (1) (a), (b) na kifungu (1) (11) na (111) kila mwandishi wa habari lazima apate ithibati kutoka Idara ya Habari Maelezo.

Alisema wanapokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya uandishi wa habari hususan katika vituo vya redio na televisheni.

Aidha, alisema wamiliki wa vyombo vya habari, kuwa na mtu anayefanya kazi ya uandishi wa habari na utangazaji bila ya kuwa na taaluma ya uandishi wa habari ni chanzo cha ukiukwaji wa maadili.

Alisema kwa sababu hiyo kuna uwezekano mkubwa wa kufanya makosa ya kiutangazaji bila weledi.

Hata hivyo, alisema chombo chochote cha habari kitakachobainika kuwa na wafanyakazi wasiokuwa na sifa za kitaaluma, hatua za kisheria zitachukuliwa.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), Abdalla Mfaume, alisema kiwango kinachopaswa kuwekwa ili uwe mwandishi ni stashada na si shahada ya kwanza kama walivyokusudia Serikali ya Zanzibar kupitia mamlaka husika.

Alisema ipo haja ya kutoa muda zaidi kabla ya sheria hiyo kupitishwa na kufanya kazi ili wahusika waweze kujiongeza zaidi kielimu.



Baadhi ya wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, wakimsikiliza mkuu wa mkoa huo (hayupo pichani), katika kikao cha wafanyakazi kilichofanyika Vuga Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ataka wananchi kufunzwa matumizi bora ya ardhi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan, amewaagiza wajumbe wa kamati ya uongozi ya usimamizi na udhibiti wa ujenzi Zanzibar (DCU), kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi bora ya ardhi yanayofuata mipango miji.

Aliyaeleza hayo wakati akifungua mkutano wa kwanza wa kamati ya uongozi ya usimamizi na udhibiti ujenzi wa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2018/2019 wenye lengo la kujadili shughuli za kamati hiyo.

Alisema wananchi wanahitaji kupewa maelekezo ya matumizi bora ya ardhi ili kupunguza ujenzi usiozingatia mipango miji.

Aidha, alisema kuwa serikali ya mkoa haitohusika katika uvunjaji wa majengo yaliyojengwa kinyume na utaratibu wakati mamlaka husika hazikusimamia na kutekeleza vyema wajibu wake.

"Sisi uongozi wa serikali ya mkoa hatutahusika katika kuwabomolea wananchi wetu wakati tangu wanaanza kujenga katika sehemu zisizokuwa rasmi sheha wa shehia husika, diwani na DCU wote walikuwapo hawakuwachukulia hatua angalau ya kuzuia ujenzi,"alionya Hassan.

Mkuu wa mkoa huyo aliwaomba wajumbe wa kamati hiyo kutoa ushauri kwa taasisi husika kurudisha serikalini, viwanja vyote ambavyo vimekaa kwa muda mrefu bila ya kuendelezwa ili vitumike kwa shughuli za maendeleo.

"Kumekuwa na viwanja vingi katika maeneo mbalimbali ya mikoa yetu vimekaa kwa muda bila ya kuendelezwa, lakini ninyi ambao ni wasimamizi na watoa vibali mmekaa kimya hatujaishauri serikali vikarudishwa kwa ajili ya matumizi mengine,"mnafanya nini alihoji Mkuu wa Mkoa.

Hata hivyo, Hassan aliitaka kamati hiyo kushirikiana na taasisi nyengine za serikali katika kutekeleza majukumu yake ili kuhakikisha sera,sheria na taratibu za matumizi ya ardhi zinatumika vizuri.

Kikao hicho cha kamati ya uongozi ya usimamizi na udhibiti ujenzi Zanzibar DCU kilichokuwa kikijadili utekelezaji wa kazi zake pia kilipata kuangalia rasimu ya mwongozo wa utoaji vibali na udhibiti wa ujenzi.

## Wahimizwa kukumbuka wahitaji kwenye elimu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAHISANI na wadau mbalimbali wamehimizwa kuwakumbuka na kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalumu ili kuwawezesha kupata elimu itakayofanikisha maisha yao na kujiwezesha kujitegemea.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhunga, aliyasema hayo wakati akikabidhi vifaa mbalimbali vya kuwasaidia wazee wenye watoto wa mahitaji maalum huko Migombani Wilaya ya Mjini Unguja .

Alisema watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto nyingi hivyo wanahitaji misaada mbalimbali ili kuwasaidia kupata elimu bora.

Alieleza kuwa baadhi ya wazee hulazimika kuwabeba watoto wao wenye ulemavu na kuwapeleka shule kutokana na kutokuwa na visaidizi.

"Baadhi ya watoto hulazimika kutembea masafa marefu kufuata elimu, hivyo wazazi na walezi hulazimika kuwabeba kutokana na kutokuwa na vifaa kama kiti mwendo kwa ajili ya kuwasaidia,"alisema Naibu Waziri.

Aidha, aliongeza kuwa utoaji wa vifaa hivyo ni kufanya kazi zao kuwa nyepesi kwao na kwa wazazi wa watoto kwani vitasaidia kuwafikisha shule kwa wakati na kufikia malengo waliojiwekea. Naibu huyo aliwataka wazazi na walezi kuvitunza vifaa hivyo ili viweze kudumu kwa muda mrefu na vinapo haribika kufanyiwa matengenezo.

Ofisa wa Halmashauri za Wilaya, Yumna Ali Mwinjuma, alisema msaada huo utakuwa endelevu kwa watoto wengine wenye mahitaji maalum.

Akizungumza kwa niaba ya wazazi wenzake wenye watoto wenye ulemavu, Juma Suleiman, alisema kuwa vifaa hivyo vimekuja wakati muafaka na watavitumia kwa dhamira iliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na kuwapelekea shule watoto wao.

"Tunashukuru sana kwa msaada huu ambao tunaimani kuwa watoto wetu sasa watakuwa wanafika shule kwa wakati,"alisema.

Wazazi na walezi hao walipewa vifaa kadhaa vilivyojumuisha vigari vya kutembelea vilivyotolewa kwenye Wilaya ya Magharibi A na B Unguja kwa lengo la kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum kuwawezesha kwenda shuleni na kukuza viwango cha elimu kwenye jamii na taifa bila kujali maumbile.

# 4,000 hufa maji Ziwa Victoria kila mwaka

**Na Elizabeth Faustine,**
MWANZA

ZAIDI ya watu 4,000 hufa maji kila mwaka katika nchi zinazozungukwa na Ziwa Victoria kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo hali isiyoridhisha ya vyombo vya usafiri.

Sababu nyingine ni uwezo wa mabaharia, ubebaji wa mizigo, hali ya hewa, pamoja na ziwa kutofanyiwa vipimo kujua penye miamba na kina kirefu tangu ilipofanyika mara ya mwisho kabla ya uhuru.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), Emmanuel Ndomba, alipokuwa akizungumza na wanahabari jijini Mwanza, na kusema kuwa ili kupunguza idadi ya vifo, Tasac imeamua kuweka vituo vya uokozi na mawasiliano.

“Tunaposema ajali ni nyingi Ziwa Victoria hatusemi kwa Watanzania pekee, tunasema na nchi zingine kama Kenya na Uganda, namba zinazoonyeshwa kutoka kwenye data walizonazo ‘lake Victoria basin’, ipo kwenye watu 4,000 kwa mwaka.

“Kuna watu wengine wanakufa, wanazikwa tu, lakini hawaripotiwi, kuna vile vijiji ambavyo vipo kando kando... mtu anakufa kwa sababu ya maji, watu wanaamua kuzika tu hivyo hivyo wala hawahitaji kuripoti, lakini idadi ipo kwenye elfu nne,” alisema Ndomba.

“Tupo kwenye mikoa 11 Tanzania, mikoa yote ya maji kwa sababu kazi zetu tunazozifanya zinakwenda kwenye vituo vya forodha vyote,” alisema.

“Juzi juzi tulikuwa tumepita hapa kwa ajili ya kutambua maeneo ambayo tutaweka vituo vya uokozi na mawasiliano kwa ajili ya kupunguza vifo vinavyotokea katika maziwa, ikiwamo Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa alisema Ndomba.

Ndomba alisema yanayofanyika katika Ziwa Victoria yanahusu nchi tatu kwa maana ya Kenya, Uganda na Tanzania hivyo mara kwa mara hukutana pamoja ili kupanga mikakati.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mwanza, Joseph Mtandika, alimshukuru Rais kuanzisha Tasac hali itakayochangia upatikanaji wa mapato halisi.

Anwar Said kutoka Said Mohamed and Brothers inayomiliki vyombo vya usafiri wa majini Nyehunge Express, alisema tozo wanazotozwa ni kubwa ikilinganishwa na faida inayopatikana na kuomba mamlaka kuona namba ya kuboresha ili kutoathiri gharama za uendeshaji wa kampuni.

“Sisi tunahusika na usafirishaji wa meli kwa maana ya mizigo na abiria... Tunaomba mamlaka iangalie kwa upande wetu wadau kulipia tozo hizi, pindi muswada huu unapelekwa bungeni uliletwa kwa wadau na tuliomba tutozwe kwenye pato la faida tofauti na kutozwa kwenye pato la jumla kitu ambacho kinafanya gharama za uendeshaji iwe kubwa kuliko faida,” alisema Said.




Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, wakimsikiliza Meneja wa Benki ya NMB, Kanda ya Mashariki, Baraka Ladislaus baada ya kukabidhi madawati 275 kwa shule tano za Kibwaya, Bwakila Chini, Newland, Kinole na Mfumbwe katika hafla iliyofanyika Shule ya Msingi Kibwaya wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matukio 7,617 ukatili yaripotiwa mwaka jana

**Na Joseph Mwendapole**

WAKATI uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ukitarajiwa kufanyika siku ya Jumatatu mkoani Dodoma, matukio 7, 617 ya ubakaji yameripotiwa katika vituo mbalimbali vya polisi katika kipindi cha Januari mpaka Desemba 2018.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Mawasiliano na Ushawishi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Neema Meremo.

Alikuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia unaotarajiwa kufanyika tarehe 25 mkoani Dodoma.

Neema alisema takwimu hizo zimo kwenye ripoti ya tamwimu za hali ya uhalifu na matukio ya usalama barabarani, huku akiongeza kuwa idadi hiyo ya kuogopesha ni sawa na asilimia 64 ya matukio yote ya uhalifu yaliyoripotiwa mwaka 2018. Alisema ukatili dhidi ya wanawake Tanzania umekuwa changamoto kubwa na kizuizi kwa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kisiasa.

“Ukatili dhidi ya wanawake ni jambo linalohitaji mwamko wa kisiasa ili kubadili mifumo dume katika ngazi ya mtu binafsi watu walio kwenye uhusaiano wa kimapenzi, familia, jamii na taasisi kwa ujumla,” alisema.

Alisema ukatili dhidi ya wanawake huathiri wanawake katika kutambua uwezo wao wa kuchangia maendeleo ya nchi, hivyo alitoa wito kwa jamii kuripoti matukio hayo kila yanapotokea.

Neema alisema mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto Tanzania (MTAKUWAA) umedhamiria kuongeza idadi ya wanawake wanaofikia huduma za kifedha kutoka asilimia 51 hadi asilimia 65.

Aidha, alisema mpango huo umelenga kuongeza uwiano wa waathirika wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake waliofanyiwa ukatili kutoa taarifa ndani ya saa 72 baada ya tukio kutoka asilimia 30 ya sasa hadi 65.

Alisema mpango huo unalenga kupunguza ukatili wa kingono kutoka asilimia 17.2 hadi nane na kupunguza ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake wenye miaka kati ya 15-49 kutoka asilimia 39 iliyopo hadi asilimia 10.

Neema alitoa wito kwa jamii kubadili rangi ya mpangilio wa tovuti zao katika mitandao ya kijamii na kuwa rangi ya chungwa katika kipindi cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

# YARA yapaisha mavuno mpunga

**Na Mwandishi Wetu**

HUDUMA za ugani na mbolea zinazotolewa na kampuni ya YARA Tanzania zimewawezesha wakulima wa mpunga katika eneo la Kahe, Malindi mkoani Kilimanjaro kuongeza mavuno.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki na waandishi wa habari waliotembelea eneo la uzalishaji la Malindi mkoani Kilimanjaro, wakulima walieleza kuwa huduma za ugani na mbole za Yara vimekuwa ni mkombozi wa wakulima wenye bidii na kuzingatia maelekezo.

“Tunaishukuru YARA kwa namna walivyokuja na ubunifu wao katika katambua aina ya udongo na ni aina gani ya mbolea itumike na kwa wakati upi itumike, hali hiyo imetufanya tuwe na ongezeko la mavuno, ambapo kwa sasa tunapata magunia 30-35 kwa ekari tofauti na huko nyuma tulipokuwa tunatumia mbolea zingine,” alieleza Manka Mushi, ambaye amekuwa akilima mpunga katika eneo hilo kwa zaidi ya miaka 15.

Mushi alisema wana kila sababu ya kujivunia kilimo cha mpunga ambacho kimewawezesha kusomesha watoto wao na kumudu gharama nyingine za maisha.

“Sasa tunaweza kulipa karo za shule kwa kuwa uzalishaji umeongezeka, lakini tumeweza kugharamia shughuli nyingine za maendeleo ikiwamo ujenzi wa nyumba za kisasa,” alileeza.

Jonathan Mjema, mkulima wa mpunga mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 20, alisema amefurahishwa na mbolea zinazozalishwa na Yara na kueleza kwamba licha ya kuwaongezea uzalishaji, mbolea hizo, zimekuwa ni rafiki kwa mazingira.

Mjema aliwahimiza wakulima wengine kote nchini kutumia mbolea za Yara.

“Ninatoa wito kwa wakulima wa Tanzania kutumia mbolea za Yara hasa katika kipindi hiki ambacho kilimo kimebadilika kutoka kilimo cha kawaida na kuwa kilimo biashara, hakika wataona faida zake,” alieleza Mjema.

## Ndege isiyo na rubani ya Italia yadunguliwa

**TRIPOL, Libya**

VIKOSI tiifu kwa mbabe wa kivita, Khalifa Haftar nchini Libya vimesema vimedungua ndege isiyo na rubani ya Italia, magharibi mwa nchi hiyo, iliyokuwa ikiruka katika eneo la anga wanalolidhibiti.

Wizara ya Ulinzi ya Italia imesema kwamba ndege hiyo isiyo na rubani ilianguka katika eneo la Libya wakati ikifanya kazi ya kuhakikisha usalama wa machimbo ya mafuta pamoja na wavuvi wa Libya.

Hayo yanajiri siku kadhaa baada ya mjumbe wa Umoja wa Mataifa kwa Libya kuzitaka nchi za kigeni kuheshimu vikwazo vya kuingiza silaha.

Libya imetumbukia katika machafuko tangu vuguvugu lililoungwa mkono na jumuiya ya kujihami NATO kumwondoa madarakani na kumuua kiongozi wa muda mrefu wa taifa hilo, Muammar Gaddafi mwaka 2011.

DW

## Mpinzani wa Netanyahu 'achemka' kuunda serikali

**JERUSALEM, Israel**

MPINZANI wa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, Benny Gantz amemwambia Rais wa Israel kwamba ameshindwa kuunda serikali ya umoja. Hivyo Israel inajiandalia uchaguzi mpya wa wabunge.

Gantz alisema alijitahidi kufanya anacho kiweza kujaribu kuunda serikali ya umoja wa kitaifa baada ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu kushindwa, bila mafanikio.

Wakati sheria ilimpa Gants hadi Jumatano saa 5:59 usiku kuwa ameunda serikali ya umoja, lakini aliamua kuachia ngazi na kutangaza kwamba ameshindwa.

Taarifa iliyotolewa na chama chake iliekeza kuwa: "Kiongozi wa chama cheupe na Bluu, Benny Gantz amezungumza na Rais Reuven Rivlin ili kumwambia kuwa ameshindwa kuunda serikali."

Netanyahu, Waziri Mkuu anayemaliza muda wake na mpinzani wake Gantz hawakupata viti vingi bungeni vinavyo mwezesha mmoja kati ya wawili hao kuunda serikali.

Awali Rais Rivlin alimwagiza Netanyahu, ambaye alikuwa madarakani tangu mwaka 2009, kuunda serikali.

RFI

# Mwanaharakati wa haki za binadamu auawa

**MOGADISHU, Somalia**

MWANAHARAKATI maarufu wa mashirika ya kiraia, Almaas Elman ameuawa kwa kupigwa risasi jana wakati akijiandaa kusafiri kwa ndege kwenda jijini Nairobi ambako anaishi.

Elman aliuawa wakati akisafiri kwa gari katika eneo salama karibu na Uwanja wa Ndege wa Mogadishu sehemu ambayo wafanyakazi wengi wa mashirika ya kimataifa wanaishi.

Elman alipelekwa hospitalini mara moja, lakini alifariki dunia wakati alipokuwa akisafirishwa. Inaelezwa kuwa Elman alikuwa mjamzito.

Binti ya mwanaharakati huyo maarufu wa amani nchini Somalia, Elman Ahmed, ambaye aliuawa mwaka 1996, alikuwa amarudi Somalia kukisaidia kituo kilichoanzishwa na mama yake katika mipango ya kupambana dhidi ya unyanyasaji.

Moja ya mipango ya kituo hicho ilikuwa kushawishi watoto na vijana wakubwa kuachana au kujitenga mbali na makundi yenye silaha na hivyo waweze kurudi shuleni.

Mtafiti Laetitia Bader, mtaalamu kutoka Shirika la Kimataifa la Haki za Binadamu la Human Right Watch katika ukanda wa Afrika, alisema Somalia imemkosa mtu muhimu katika masuala ya haki za binadamu.

"Familia yake imepoteza mtu muhimu, lakini pia mashirika ya haki za wanawake na haswa waathiriwa wa dhuluma ya kingono ambao ni wengi leo nchini Somalia," alisema Bader.

Maofisa wa usalama wanabaini walieleza kuwa Elman aliuawa baada ya risasi kumpata.

"Hakuna risasi zilizofyatuliwa kwenye uwanja wa ndege au maeneo yalio karibu kabla ya tukio hilo," alisema Mohamed Omar, ofisa usalama, huku akibaini kwamba uchunguzi umeanzishwa.

*RFI*



Wagombea urais kwa tiketi ya chama cha Demokrat kutoka kushoto, Seneta Cory Booker, Tulsi Gabbard, Seneta Amy Klobuchar, Meya wa South Pete Buttigieg, Seneta Elizabeth Warren, aliyekuwa Makamu wa Rais Joe Biden, Seneta Bernie Sanders na Seneta Kamala Harri. **PICHA: REUTERS**

# Waliouawa na ADF wazikwa kwa maandamano

**BENI, Congo**

WAKAZI wa mji wa Beni jana waligoma kufanya kazi baada ya vijana kuweka vizuizi barabarani kwa ajili ya kufanyika kwa shughuli ya mazishi ya watu waliouawa na ADF katika mji huo juzi.

Mauaji yanayoendeshwa na kundi la ADF wakati operesheni dhidi ya kundi hilo la uasi likiendelea, huenda yakavunja uhusiano ulioko baina ya jeshi na wakazi.

Wanachama wa vyama mbalimbali wengi wao wakiwa ni vijana waliandamana kuomboleza ndugu zao waliopata msiba pamoja na kupinga mauaji ya kila siku katika Wilaya ya Beni.

Wakizungumza katika njia panda kuu ya Beni Nyamwisi, vijana hao ambao waliwapa wanajeshi wa Tume ya Umoja wa Mataifa (Monusco) ilani ya saa 48, ili wawe wameondoka mji wa Beni huku wakisema hawaoni sababu ya wanajeshi hao kuwepo na ikiwa bado wanauawa.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema mauaji yanayoendelea pamoja na mgomo na maandamano huenda yakavunja mapatano yalipo kwa sasa, baina ya majeshi ya serikali yaliyoko kwenye uwanja wa mapambano katika misitu.

Mtazamo huo unapingwa na baraza la wazee wa busara wa mji wa Beni, wanaodhani kwamba, maandamano pamoja na mgomo, ni aina fulani ya wakazi kuomboleza na familia zilizopata msiba, na katu hayawalengi wanajeshi walioko kwenye operesheni dhidi ya waasi kutoka Uganda ADF.

Waasi wa ADF waliwaua watu saba katika mji wa Beni na wengine 14 katika kijiji cha Mavette Wilaya ya Beni ikiwa ni kilomita 36 kutoka Kaskazini Magharibi mwa mji huo.

Tangu yalipoanza mauaji ya wakazi kwa kukatwa kwa mapanga na ADF, raia wasiopungua 3,000 wameshapoteza maisha kulingana na takwimu zinazotangazwa na mashirika ya kiraia.

*DW*

HABARI KITAIFA

# Lucas Lukumbo ukalale mahali pema peponi

**Na Mwandishi Wetu**



KWAHERI Lucas Lukumbo, ndivyo tunavyoweza kusema wakati huu baada ya kusikia taarifa za mwandishi nguli, aliyefariki dunia juzi, jijini Dar es Salaam.

Lukumbo kwa mujibu wa taarifa zilizowafikia wanahabari kutoka kwenye mitandao ya kijamii, alifariki baada ya kulazwa siku kadhaa katika Hospitali ya Mloganzila.

Baada ya kustaafu kazi, aliendelea kufanyakazi za uandishi wa habari na akiishi Kibaha, mkoani Pwani.

Wanahabari wanamkumbuka Lukumbo kwa umahiri wake wa uandishi wa habari na sifa ya uvumilivu na upendo.

Lukumbo ana historia ndefu katika sekta ya habari na amepitia vyombo vikubwa vya habari likiwamo lililokuwa Shirika la Habari Tanzania (SHIHATA ), Daily News na The Guardian Limited.

Akimzungumzia Lukumbo, mwandishi mkongwe, Evarist Mwitumba, ambaye amewahi kufanyakazi naye katika magazeti ya serikali na binafsi, anamkumbuka mwanahabari huyo kwa uandishi mahiri wakati huo wakiwa wote SHITATA.

"Lucas Lukumbo ni miongoni mwa waandishi wa habari waandamizi aliyenipokea Shihata wakati nilipojiunga hapo mwaka 1988 baada ya kuhitimu chuo kikuu. Ninamfahamu kama mtu aliyeipenda sana kazi yake. Alipenda zaidi kuandika habari zenye kuvutia zinazozungumzia masuala ya kijamii au tunaziita 'human interest.' Baada ya SHIHATA nilifanya naye tena kazi kwenye kampuni ya Media Holdings (Tanzania) Limited iliyokuwa inachapisha magazeti ya The Express na Mwananchi, kabla ya kukutana tena Daily News ambako nilifanya naye kazi kwa karibu nikiwa mhariri wa habari na yeye mhariri msanifu ambapo tulikuwa marafiki wakubwa.

Lukumbo ambaye pia alifanya kazi Mwananchi Communications LTD, anakumbukwa na David Chikoko mchora katuni za The Flexibles na Gwiji zinazochapishwa na The Guardian, akisema walikuwa wote Daily News na mwaka 1998 waliondoka pamoja kwenda kutafuta kazi katika sekta binafsi.

"Ni mtu ambaye tuliondoka pamoja Daily News daima ni kaka yangu 'my big brother', tulikuwa pamoja na siku zote tuliitana brother. Nikiwa na Lukumbo nje ya Daily News nilimuona kama ni rafiki ndugu au Mtanzania niliyekutana naye ughaibuni. "

Akiwa mfanyakazi wa The Guardian Limited, Lukumbo alikuwa mahiri kwenye dawati la makala na ataendelea kukumbukwa kwa utu wema na maneno yasiyo mkwaza yeyote.

Alikuwa anazungumza taratibu, akicheka muda wote na hakupenda kuwaza mambo ambayo hakuwa na majibu yake. Kwa mfano ni mtu wa kujichanganya. Hakujali kuwa ana hadhi au kiwango cha juu katika jamii, kwa kuwa alijishusha zaidi kuliko kujikweza.

Mathalani, alikuwa mpenzi wa pweza na ngisi. Alipenda kusema raha jipe mwenyewe. Acha hofu. Hiyo ilitosha kusimama eneo lolote kula pweza na ngisi na kunywa mchuzi wake bila kujali anaweza kukutana na nani au hata kupigwa picha na wanahabari wenzake waliokuwa wanapita barabarani muda huo.

Lukumbo alikuwa rafiki na baadhi ya wanahabari wanamtaja kuwa alitabasamu na kucheka na kila mtu tena muda wote. Hakuwa na kificho ukimkosea anakueleza ukweli, hakuwa mnafiki.

"Jamani poleni sana. Kwa kweli Lucas alikuwa 'very friendly and always smiling' na aliipenda fani yake tena 'serious' kwa kweli tutammisi mpendwa wetu a.k.a. Lucy kama alivyokuwa akiitwa na wanahabari kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), kutokana na ushiriki wake wa habari za kupinga unyanyasaji wa wanawake na watoto." Ujumbe wa mmoja wa wanachama ulieleza.

Mungu amrehemu na kumpa nafasi katika makao yake ya milele huko mbinguni.

# Waziri akerwa kasi ujenzi holela

**Na Munir Shemweta, MOROGORO**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezitaka halmashauri nchini kudhibiti ujenzi holela kwa kutoa vibali vya ujenzi na kusimamia ipasavyo.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo kwa nyakati tofauti jana katika halmashauri za wilaya za Morogoro, Mvomero na Manispaa ya Morogoro wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi katika sekta ya ardhi mkoani hapa.

Alisema halmashauri nchini zina wajibu wa kudhibiti ujenzi holela katika maeneo mbalimbali kwa kushirikiana na watendaji wa mitaa na kuweka taratibu ambazo hazitamruhusu mtu kufanya ujenzi wowote bila kupata kibali cha ujenzi kutoka halmashauri husika.

"Ili kuondokana na ujenzi holela katika halmashauri zenu, mwananchi asifanye ujenzi wowote bila kupata kibali kutoka halmashauri," alisema.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, urasimishaji unaoendelea sasa katika maeneo mbalimbali, si wa kudumu na kulegalega kudhibiti ujenzi holela kutasababisha jambo hilo kutokuwa na maana kwa kuwa ujenzi holela utakuwa ukiendelea.

Kuhusu utoaji hati za ardhi, Dk. Mabula aliagiza hati zilizokamilika katika ofisi za msajili wa hati, wamiliki watangaziwe kupitia njia mbalimbali zikiwamo redio za kijamii sambamba na kutolewa kwa wamiliki wake katika eneo maalum litakaloandaliwa karibu na maeneo wanayoishi.

Alisema njia ya kuwatafuta wananchi ambao hati zao zimekamilika, itasaidia kupunguza mrundikano wa hati zilizokamilika kwenye ofisi za msajili tofauti na utaratibu wa sasa unaomtaka mwenye hati kuifuata ofisi za ardhi au kwa Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Kanda.

Awali, Mkuu wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Patrick Mwakilili, alisema halmashauri yake imepanga kupima viwanja 1,000 kwenye makao makuu ya wilaya, Mvuha, na vingine 3,900 katika mji mdogo wa Kisaki ambao ni lango la kuingilia mradi wa kufua umeme wa Stiglers George na Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, zamani Selous.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa idara, tayari maeneo tisa ya kufanyiwa urasimishaji makazi yameainishwa ambayo ni Pangawe, Mkambarani, Fulwe, Ngerengere, Mvuha, Kisaki, Mtamba, Mkuyuni na Duthumi na kubainisha kuwa halmashauri yake imepokea na kuridhia maombi kutoka kampuni nne kwa ajili ya kazi hiyo.

# Asomewa mashtaka 116 uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

OFISA Masoko wa kampuni ya IG International Limited, Abasal Kassim, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka 116 ya uhujumu uchumi, ikiwamo kughushi nyaraka na wizi wa Dola za Marekani 33, 000.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashitaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Janeth Magoho, alidai kuwa katika shtaka la kwanza mpaka la 30, kati ya Desemba 30, 2013 na Machi, 2015 mshtakiwa anadaiwa kughushi nyaraka kinyume cha sheria.

Katika mashtaka hayo mshtakiwa anadaiwa kwa kujua na kwa nia ovu ya kufanya udanganyifu, alighushi nyaraka zenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani 20,000 kuonyesha zimetolewa na kampuni ya IG International Limited huku akijua si kweli.

Katika shitaka la 31 mpaka 84 mshtakiwa anadaiwa katika eneo la Mbagala, Dar es Salaam, alifungua akaunti Diamond Trust Bank na aliiba Dola za Marekani 33, 000 mali ya kampuni ya IG International Limited.

Aidha, katika shtaka la 85 mpaka 114, mshtakiwa anadaiwa kuwasilisha nyaraka zisizo halali kinyume cha kifungu cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu CPA).

Baada ya mshtakiwa huyo kusomewa mashtaka, Wakili Magoho alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba ipangiwe tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Shaidi alisema mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi, hivyo mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote na kwamba arudishwe mahabusu mpaka Desemba 4, mwaka huu, kesi itakapotajwa.

**Katika shitaka la 31 mpaka 84 mshtakiwa anadaiwa katika eneo la Mbagala, Dar es Salaam, alifungua akaunti Diamond Trust Bank na aliiba Dola za Marekani 33, 000 mali ya kampuni ya IG International Limited.**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*


## KUPOTEA KWA CHETI




**Andrew Stephano Chaula** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2547/0061 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika Shule ya Sekondari Lyandembela.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: IRI/IRI/RB/404300/2019

115527902

## CHETI KIMEPOTEA



**ANDREW HOMBEE MBWETE** anatangaza kupotelewa na cheti cha form six chenye No. S 0465-0790 kilichotolewa na Jamuhuri Secondary school mwaka 2010.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**taarifa ya polisi:**
**DOD/DOD/RB/53970/2019.**

115528202

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA
MAHALI DODOMA
MAOMBI NA. 240 YA 2019
BAINA YA
WAZIRI OMARI KIVALE
NADYA SALUM ABDALAH……………………………WAOMBAJI
DHIDI YA
YUSUF MOHAMED (Msimamizi wa Miradhi ya Marehemu Mohamed Maddar)
CHIEF ASILI COMPANY LIMITED ……………………WADAIWA

KWA:-YUSUF MOHAMED
CHIEF ASILI COMPANY LIMITED
POPOTE MLIPO

YAH:KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 5.12.2019 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo mnatakiwa kuleta utetezi wenu kwa maandishi.

ANGALIZO:-Kama hamkuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa mmepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yenu.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 20 ya Mwezi wa November,2019.

215528501

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)

Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi 79/2019

Ombi la HAWA HAJI kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi Marehemu IDD ADAM MWAMBIAGI
KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 2/12/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

215528302

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY
IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
AT BUKOBA

LAND CASE APPEAL NO. 45/2018

MODEST MUFURUKI…………………APPELLANT
VERSUS
THE BOARD OF TRUSTEES ST PETER CLAVERY ENGLISH MEDIUM & ANOTHER………………RESPONDENTS

TO: LINUS BEGUMISA METHOD LWANOMBE OF BUGENE WARD KARAGWE

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Appellant lodged a case registered as Land Case Appeal No. 45 of 2018 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba. Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 25th day of November, 2019 at 09:00 am before Hon. F.H. Mutulya. You are authorized to appear in person or through your Advocate. Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 8th day of November, 2019.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

115528402

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No; 257/2019

Ombi la ASHA RASHID TOMBO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RASHID NASSORO TOMBO.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 20/11/2019

115528202


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# RONALDO: JUVE NILETEENI POGBA



**TURIN, Italia**

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo amewaomba mabosi wake wampe mkataba kiungo wao wa zamani, Paul Pogba ambaye kwa sasa anakipiga pale Manchester United.

Pogba ambaye timu yake ya Ufaransa ni mabingwa wa Kombe la Dunia, uwezo wake umekuwa ni wa kusuasua ndani ya Old Trafford kutokana na kusumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara.

Real Madrid inayoshiriki Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, imekuwa ikitajwa kuiwania saini ya nyota huyo huku kocha wao, Zinedine Zidane akisema kuwa ni miongoni mwa viungo anaowakubali wakiwa uwanjani.

Mabosi wa United wametaja dau la kukomoa kwa timu inayotaka saini yake ambalo linatajwa kuwa ni pauni milioni 80 na Juventus wanatajwa kuongeza juhudi ili kuinasa saini yake ifikapo Januari wakati wa dirisha dogo la usajili.

## MISRI, IVORY COAST KUIWAKILISHA AFRIKA MICHUANO OLIMPIKI 2020

**CAIRO, Misri**

MATAIFA ya Misri na Ivory Coast yamefuzu kushiriki michuano ya Olimpiki 2020, itakayofanyika Tokyo nchini Japan, baada ya timu zao za taifa chini ya umri wa miaka 23 kutinga hatua ya fainali.

Mataifa hayo yametinga hatua ya fainali ya michuano ya Afrika chini ya umri wa miaka 23, inayoendelea nchini Misri, kwa kuzitupa nje Afrika Kusini na Ghana.

Wenyeji Misri waliibanjua Afrika Kusini kwa mabao 3-0, kwenye mchezo wa nusu fainali, huku Ivory Coast wakiichabanga Ghana kwa changamoto ya mikwaju ya penalti.

Misri waliokuwa wanacheza mbele ya mashabiki wao, walipata bao la kwanza kwa njia ya mkwaju wa penalti kupitia kwa Ramadan Sobhy dakika ya 59, huku Abdel Rahman Magdy akifunga mabao mawili na kukamilisha ushindi wa mabao 3-0 uliowavusha hadi hatua ya fainali.

Hata hivyo, mshiriki wa tatu kutoka Afrika kwenye michuano ya Olimipiki 2020, anatarajiwa kufahamika baada ya mchezo wa kumsaka mshindi wa tatu na wa nne, utakaochezwa leo Ijumaa, kati ya Ghana na Afrika Kusini.

Michuano ya Olimpiki 2020, imepangwa kuanza kunguruma mjini Tokyo, Japan kuanzia Julai 24 hadi Agosti 9, huku michuano ya soka ikipangwa kuanza kutimua vumbi kuanzia Julai 22 hadi Agosti 8.




Katika michuano hiyo upande wa wanaume timu 16 zitashiriki, huku kwa wanawake zikitarajiwa kuwa na timu 12, kutoka kwenye mabara yote.

Viwanja saba vitatumika kushuhudia mi-amba upande wa wanaume na wanawake.

## STERLING KUMPIKU DE GEA MSHAHARA

**LONDON, England**


RAHEEM Sterling anatarajiwa kutia saini mkataba mpya na Manchester City utakaomfanya kuwa mchezaji ghali raia wa Uingereza.

Sterling alitia saini mkataba unaomlipa mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki Novemba, mwaka jana.

Kocha wa Man City, Pep Guardiola amevutiwa na kiwango cha Sterling ambaye amekuwa chachu ya mafanikio pale Etihad.

Mshambuliaji huyo wa England amefunga mabao 14 katika mechi za mashindano mbalimbali msimu huu.

Man City inataka kumwongeza mkataba mpya unaoweza kumpa mshahara wa zaidi ya pauni 300,000 kwa wiki.



Mkataba wa Sterling unamalizika mwaka 2023, lakini Man City inataka kumwongeza baada ya kupandisha kiwango chake katika Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sterling kwa sasa yuko sawa kwa mshahara na kipa wa Manchester United, David de Gea anayelipwa mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki.

Man City inataka kumpiga kitanzi mshambuliaji huyo baada ya klabu za Hispania Real Madrid na Barcelona kutaka saini yake.



# LEWANDOWSKI
## AONYA WAPINZANI BUNDESLIGA

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski anafurahia mwanzo mzuri wa msimu akiwa na Bayern Munich, lakini amesisitiza bado hajaonyesha ubora wake wote.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland ana mabao 23 katika mechi 18 alizoichezea klabu yake msimu huu, yakiwa mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote katika ligi kubwa tano barani Ulaya.

Hata hivyo, Lewandowski anaamini bado hajafikia kiwango chake na kwamba mambo mazuri zaidi yanakuja kutoka kwake na kusisitiza hahisi kama ana umri wa miaka 31.

"Nilifanya kazi kubwa kuwa kwenye kiwango hiki. Kwa sasa naenda vizuri, mwili wangu nauhisi vizuri," alisema akiiambia Sport Bild.

"Ni vizuri kuwa kwenye akili kama hii, lakini haimaanisha kwamba napumzika. Nataka kuwa bora zaidi.

"Najua wakati ninaoweza kufanya mengi zaidi na wakati nikiwa taratibu. Hati yangu ya kusafiria inasema: 'Robert Lewandowski ana umri wa miaka 31'. Lakini hivyo sivyo ninavyojihisi.

"Ubora wangu ndio kwanza unaanza na nina matumaini utaendelea kwa miaka inayokuja. Ubora wangu bado unakuja."

Lewandowski anatarajiwa kurudi kwenye klabu baada ya mechi za kimataifa wakati Bayern ikiivaa Fortuna Dusseldorf.

# Keown aitaka Arsenal kumgeukia Pochettino

**LONDON, England**

ARSENAL inatakiwa kuangalia uwezekano wa kumchukua kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino, kwa mujibu wa beki wa zamani wa 'Washika Bunduki' hao wa London, Martin Keown.

Spurs iliziba nafasi ya Pochettino waliyemfukuza baada ya kukaa hapo kwa miaka mitano kwa kumchukua Jose Mourinho.

Huku awali Mourinho alitumika pale Chelsea, anatazamiwa kusajili wachezaji wakubwa hapo Tottenham kwa kipindi chake atakachokaa pale kwa miamba hao wa London Kaskazini.

Kocha wa sasa wa Washika Bunduki hao, Unai Emery amekuwa kwenye presha kubwa baada ya timu yake kuanza vibaya msimu huu na sasa Keown anaona kocha huyo wa zamani wa Sevilla na Paris Saint-Germain ni wakati wa kuondolewa hapo Arsenal.

Ingawa Keown amebainisha kuwa Arsenal wasifanye haraka katika zoezi hilo.

"Hakuna haja kwa Arsenal kupaniki, ingawa hatupo kwenye msimu mzuri kwa sababu mbalimbali," alisema akinukuliwa na Gazeti la Daily Mail.

"Lakini ili kuwa juu ni lazima kuhakikisha kwamba unachukua makocha makini kama Pochettino.

"Ninamwelewa mno Pochettino na naamini akitua pale Arsenal anaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi chetu."



# Ibrahimovic aanza kuteta na AC Milan



**MILAN, Italia**

ZLATAN Ibrahimovic yupo kwenye mazungumzo juu ya uwezekano wa kurudi AC Milan, lakini mpango huo bado una safari ndefu, kwa mujibu wa Sky Sports Italia.

Aliichezea klabu hiyo kati ya mwaka 2010 na 2012 na anaangalia uwezekano wa kujiunga na klabu mpya baada ya kutangaza kuondoka LA Galaxy mapema mwezi huu.

Maofisa wa Milan walikutana na wakala wa Ibrahimovic, Mino Raiola Jumatano na bado hawajafikia maafikiano.

Kwa mujibu wa Sky Sport Italia kuna kizingiti ambacho Ibrahimovic anatakiwa kukimaliza kabla ya kurudi kwenye ligi hiyo ya Serie A, ingawa mambo hayo yatatakiwa kumalizwa na pande zote mbili.

Imebainisha kwamba, Milan wapo tayari kutoa ofa ya mkataba wa miezi 18 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, lakini mshahara wake unaonekana kuwa ni tatizo, huku kwa sasa ikiwa inatumikia adhabu ya kutoshiriki michuano ya Ulaya kutokana na kuvunja sheria ya usawa wa matumizi ya fedha katika kusajili.

Ibrahimovic, ambaye amefunga mabao 53 katika mechi 58 kwa kipindi cha miaka miwili alichokaa pale Galaxy, ataamua majaliwa yake ndani ya wiki chache zijazo.

Alifunga mabao 56 katika mechi 85 wakati alipocheza pale Milan na kuisaidia kutwaa taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, mwaka 2011.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO: JEMBE LANGU SPURS NI KANE

●●● Amwambia Levy kamwe asiuzwe, apania kufuzu Ligi ya Mabingwa huku...

**London, england**

Jose Mourinho amemweleza Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy ahakikishe Harry Kane haruhusiwi katu kuondoka klabuni hapo.

Spurs, Jumatano ilithibitisha kuteuliwa kwa Mourinho kuinoa timu hiyo ambapo atakuwa akilipwa pauni milioni 15 kwa mwaka, dau ambalo ni karibu mara mbili ya lile la mtangulizi wake Mauricio Pochettino aliyekuwa akipokea mshahara wa pauni milioni 8.5 kwa mwaka, ambaye alitimuliwa Jumanne usiku.

Jambo la kwanza alilolifanya Mourinho baada ya kutua Spurs, lilikuwa ni kuzungumza na wachezaji wa kikosi chake. Kisha akafanya mazungumzo ya ana kwa ana na wachezaji muhimu kuwaelezea malengo yake. Kane, ambaye ni nahodha wa Spurs wakati huu Hugo Lloris akiwa nje kuuguza majeraha, alikuwa ni mmoja wa wachezaji kocha huyo mpya aliyezungumza naye binafsi.

Mourinho anaona mshambuliaji huyo mahiri wa England kama muhimu katika mipango yake na amemwambia Levy kuwa hawezi kuuzwa kwa hali yoyote ile.

Kumekuwa na kuongezeka kwa hofu ndani ya klabu kwamba Kane anafadhaika kutokana na ukweli kwamba hajashinda kombe.

Mourinho, 56, amesaini mkataba wa miaka mitatu na nusu ambapo hili hilo lilisimamiwa na wakala Pini Zahavi, ambaye mara ya kwanza alimleta Mreno huyo kufanya kazi England katika klabu ya Chelsea mwaka 2004.

Mourinho alitoa kilio kisichokuwa na huruma wakati wa mkutano na timu akielekeza nguvu kwa kusisitiza umuhimu wa kuweka ugumu wa msimu nyuma yao ili kupanda katika nafasi za juu kwenye msimamo wa ligi.

Mourinho alikiambia kikosi hicho, ambacho kilishindwa kutwaa kombe wakati kikiwa chini ya Pochettino kwa kipindi cha miaka mitano na nusu, kuwa kitafanikiwa kama wakiweka msukumo pamoja na akaeleza namna alivyo na furaha kufanya nao kazi. Chanzo kimoja kilisema alikuwa "kama biashara".

Mreno huyo hakusita kueleza matumaini ya kutoa changamoto ya kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa, licha ya ukweli kwamba Spurs ipo pointi 11 nyuma ya Manchester City inayoshika nafasi ya nne.

Moja ya sababu kuu nyuma ya uamuzi wa Levy kumtimua Pochettino ilikuwa ni kutokana na mwenyekiti huyo kuamini kwamba klabu hiyo haikuwa na nafasi ya kumaliza nafasi nne za juu ikiwa chini ya Muargentina huyo.

## KWA UFUPI

**BALE KUREJESHWA SPURS**

KOCHA mpya wa Tottenham, Jose Mourinho atajaribu kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Spurs, Gareth Bale, 30, kutoka Real Madrid, Mreno huyo alitaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales wakati akiwa Manchester United. ***(AS - in Spanish)***

**POCHETTINO AVUTWA ARSENAL**

BEKI wa zamani wa Arsenal, Martin Keown anaamini 'Gunners' wanapaswa kuzingatia kumteua kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino kuinoa timu hiyo. (Mail)

**AUBAMEYANG AISIKILIZIA BARCA**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 30, bado hajaongeza mkataba wake na Arsenal kwa sababu anaisubiri Barcelona. ***(Mirror)***

**DZEKO ATAKIWA UNITED**

Manchester United inazingatia kumfuata mshambuliaji wa kimataifa wa Bosnian, Edin Dzeko, 33, katika dirisha la Januari. ***(ESPN)***

**MADDISON AITAFAKARI LEICESTER**

KIUNGO wa England, James Maddison, 22, anataka kusaini mkataba mpya na Leicester licha ya kutakiwa sana na Manchester United. ***(Manchester Evening News)***

**IBRAHIMOVIC ANUKIA MILAN**

WAKALA wa Zlatan Ibrahimovic, Mino Raiola amekutana na AC Milan kuzungumza uwezekano wa straika huyo Mweden kurudi kuichezea klabu hiyo. (Corriere dello Sport - in Italian)

**FERNANDES, MATIC KUTUA SPURS**

JOSE Mourinho pia anamwinda kiungo wa Sporting Lisbon na Ureno Bruno Fernandes, 25, pamoja na beki wa kati raia wa Ureno, Ruben Dias, 22, pamoja na kiungo wa Manchester United, Mserbia Nemanja Matic, 31. ***(Independent)***

**ARSENAL YAMZUNGUKA HAALAND**

Arsenal imepiga hatua kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Erling Haaland, 19, baada ya kumkaribisha baba wa straika huyo, kiungo wa zamani wa Leeds, Alf-Inge Haaland, kutembelea uwanja wao wa mazoezi. ***(Sport Bild, via Metro)***

**BARCA, BAYERN KWA POCHETTINO**

Barcelona na Bayern Munich zipo tayari kumfuata Mauricio Pochettino. ***(Sun)***

**JUVE KUMSHAWISHI MBAPPE**

Juventus itajaribu kumshawishi mshambuliajui Mfaransa Kylian Mbappe, 20, kukataa mpango wa Real Madrid kutaka kumsajili na kisha kujiunga na klabu hiyo ya Serie A akitokea Paris St-Germain. ***(Tuttosport, via Sky Sports)***

**GIROUD AFIKIRISHA INTER**

MPANGO wa Inter Milan kumfuata mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud, 33, unaweza kupeperusha na mahitaji ya Mfaransa huyo. ***(La Gazzetta dello Sport, via Mail)***

**PIATEK, KEAN KUPISHANA**

Everton itakuwa na nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa AC Milan na Poland, Krzysztof Piatek, 24, kutoka na mpango wa 'Toffees' hao kutaka kubadilishana na staika Mtaliano Moise Kean, 19, kwenda Milan. ***(Sport Witness)***

HABARI MICHEZO

# SHIME AIFICHA UGANDA SILAHA ZA NUSU FAINALI

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI jana akijua mpinzani wake kuelekea nusu fainali ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), Bakari Shime, amesema mchezo wa mwisho dhidi ya Zanzibar Queens, aliwapumzisha baadhi ya nyota wake kwa ajili ya hatua hiyo inayofuata.

Kutokana na matokeo ya jana, ambapo Uganda ilikubali kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Kenya na kushika nafasi ya pili kwenye Kundi B, sasa Kilimanjaro Queens itakutana na Waganda hao katika hatua ya nusu fainali wakati Burundi iliyomaliza nafasi ya pili kwenye Kundi A ikikutana na Wakenya.

Kabla ya mechi hiyo timu hizo zilikuwa zikifungana kwa kila kitu, pointi hadi mabao ya kufunga na kufungwa, wakati Ethiopia licha ya kuibuka na ushindi wa mabao 8-0 dhidi ya Djibouti jana, mchezo huo ulikuwa wakukamilisha tu ratiba kutokana na timu hizo kuyaaga mashindano mapema.

Akizungumzia mchezo wao wa juzi wakati Kilimanjaro Queens ilipowavaa ndugu zao, Zanzibar Queens, Shime alimwambia mwandishi wetu kuwa pamoja na kutotumia nyota wake wote, kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake wakati wakishinda 7-0, kilimfurahisha.

Alisema ushindi huo umempa nguvu kuendelea kujipanga kwa mechi ya nusu fainali.

"Nashukuru kwa hatua tuliyofikia wachezaji wangu wameonyesha uwezo mkubwa na hatimaye kutoka na ushindi mnono.

"Mchezo ulikuwa mgumu lakini nashukuru wachezaji wangu kipindi cha pili walifuata maelekezo niliyowapa wakabadilisha taswira nzima ya mchezo, hata hivyo katika mchezo huo kuna baadhi ya wachezaji ambao niliamua kuwapumzisha kwa ajili ya kuwaandaa kwa mechi ijayo," alisema.

Alisema amebaini makosa madogo madogo ambayo amekiri kuyafanyia kazi ili yasijirudie kwa mara nyingine hususan hatua ya nusu fainali ambayo wanatarajia kuwa ngumu zaidi.

Kilimanjaro Queens imemaliza hatua ya makundi ikiwa na jumla ya mabao 20 yaliyopatikana kwa kuizamisha Sudan Kusini 9-0, na kisha mchezo wa pili ikaifumua Burundi 4-0 kabla ya kuhitimisha kwa ushindi wa 7-0 dhidi ya Zanzibar Queens.



Mshambuliaji wa Kilimanjaro Queens, Mwanahamisi Omar (kushoto), akimiliki mpira dhidi ya beki wa Burundi wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 kwenye michuano ya Cecafa Challenge Cup inayoendelea katika Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam.
**PICHA: MAKTABA**

## Donisia anukia Kiatu cha Cecafa Wanawake

**Na Shufaa Lyimo**

WINGA wa timu ya Taifa ya Wanawake ya Kilimanjaro Queens, Donisia Minja, yupo kwenye mbio za kutwaa Kiatu cha Dhahabu kwenye michuano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake baada ya kucheka na nyavu mara tano hadi sasa.

Katika michuano hiyo inayoendelea kwenye Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam, huku ikiwa imefikia hatua ya nusu fainali, mbio hizo za ufungaji bora, Donisia anafukuzana na Nalukenge Juliet wa Uganda na Jentrix Shikangwa wa Kenya, ambao kabla ya mechi yao ya jana kila mmoja alikuwa na mabao matano.

**Mwanahiba Omary wa Kilimanjaro Queens anafuatia katika mbio hizo akiwa na mabao manne huku Asha Rashid (Kilimanjaro Queens), Ikwaput Fazila, Nasuuna Hasifah (Uganda), Mwanalima Jeriko, Mercy Airo (Kenya) na Sakina Said (Burundi) kila mmoja akiwa na mabao matatu.**

Hata hivyo, orodha hiyo ya wafungaji ni kabla ya mechi za jana kati ya Kenya na Uganda na Ethiopia dhidi ya Djibouti.

Akizungumza na gazeti hili, Donisia alisema anafurahi kufikisha idadi hiyo ya mabao na akaahidi kujituma zaidi ili kuweza kutwaa kiatu hicho, lakini akaeleza lengo lake kubwa ni kuona wanatwaa ubingwa.

"Mashindano ni magumu, lakini kwa idadi hii ya mabao nazidi kumuomba Mungu nikishirikiana na wachezaji wenzangu ili zaidi tuweze kutwaa ubingwa," alisema Donisia.

Aidha, aliwashukuru Watanzania kwa sapoti kubwa wanayowaonyesha kwa kujitokeza kwa wingi Uwanja wa Azam Complex, Chamazi ambapo mashindano hayo yanafanyika.

# Da Silva achekelea kuona mwezi Simba

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuziona nyavu kwa mara ya kwanza mbele ya mashabiki wa timu yake ya Simba, Mbrazil Wilker Da Silva amesema sasa ni muda wa kupambana bila kujali aina ya mpinzani wanayekwenda kukutana naye.

Da Silva aliifungia Simba bao pekee wakati ikishinda 1-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya JKT Tanzania iliyopigwa Uwanja wa Chamazi Ijumaa, hii ikiwa ni mara ya kwanza kwa mshambuliaji huyo kufunga bao akiwa na Simba katika ardhi ya Tanzania, kwani mabao mengine aliifungia wakati ikiwa kambini Afrika Kusini kabla ya msimu kuanza.

Kufuatia furaha hiyo, Mbazil huyo amesema: "Nilifurahi sana baada ya kufunga bao. Simba ni timu kubwa na tunapaswa kupambana ili kushinda kila mchezo bila kujali aina ya mpinzani ambaye tunakutana naye."

Simba inayoongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, itashuka katika Uwanja wa Uhuru kesho kuikaribisha Ruvu Shooting ambayo itakuwa ikihitaji ushindi ili kuendeleza ubabe wake dhidi ya vigogo wa soka nchini baada ya awali kuichapa Yanga.

Katika mechi hiyo, Simba inatarajiwa kuongozwa na Kocha Msaidizi, Dennis Kitambi, kufuatia Kocha Mkuu, Mbelgiji Patrick Aussems kuzuiwa kwa muda na uongozi wa klabu hiyo kutokana na kukerwa na tabia yake ya kuondoka nchini na kudai kwenda kwao Ubelgiji kwa matatizo binafsi bila ruhusa ya mwajiri wake. Huku ikidaiwa alikwenda Afrika Kusini kwa mazungumzo ya kutaka kuinoa ya Polokwane.

Uongozi wa klabu hiyo umesema kitendo kilichofanywa na Aussems si sahihi na wanaona si busara kumpa nafasi ya kukiongoza kikosi chao kwenye mchezo huo wa ligi.

# Michezo

Ijumaa Novemba 22, 2019

Nipashe




## Mourinho: Jembe langu Spurs ni Kane

HABARI UK 30

**KITU HICHO...**



Mshambuliaji wa Brazil, Philippe Coutinho, akifunga bao katika ushindi wao wa kwanza tangu Julai, wakati wakishinda 3-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Korea Kusini iliyopigwa Abu Dhabi juzi. Mabao mengine yalifungwa na Lucas Paqueta pamoja na Danilo.
**PICHA: MTANDAO**

# YONDANI, FEI TOTO WAITIBULIA YANGA

●●●Mkwasa amtaja pia Metacha na Makame akimsifu Sibomana, huku Kocha JKT Tanzania akikiri Simba kuisaidia...

**Somoe Ng'itu na Shufaa Lyimo**

WAKATI Yanga ikishuka dimbani leo kuivaa JKT Tanzania kwenye mwendelezo wa Ligi Kuu Bara, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Mkwasa, licha ya kusema kikosi chake kiko fiti kwa mchezo huo, amekiri kupata wakati mgumu kutokana na wachezaji wake waliokuwa katika majukumu ya timu ya Taifa, Taifa Stars kushindwa kufika mazoezini jana na kujifua na wenzake.

Wachezaji wa Yanga waliokuwapo katika majukumu ya timu taifa nchini Tunisia wakati wakiivaa Libya na kuangukia kichapo cha mabao 2-1, ni Kelvin Yondani, Metacha Mnata, Feisal Salum 'Fei Toto' na Abdulaziz Makame, ambao walirejea juzi usiku na jana asubuhi kutokana na uchovu wakashindwa kujiunga na wenzao mazoezini kujiandaa na mechi dhidi ya JKT Tanzania itakayopigwa Uwanja wa Uhuru leo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkwasa alisema licha ya Patrick Sibomana naye kuwapo katika majukumu ya timu ya Taifa ya Rwanda, aliwahi na kuungana na wachezaji wenzake wa Yanga mazoezini jana, hivyo anaweza kumtumia katika mchezo huo wa leo.

"Yondani, Metacha, Fei Toto na Makame hawakufanya mazoezi na wenzao jana, ila Sibomana licha naye kuwa katika majukumu ya timu yake ya Taifa [Rwanda], aliwahi na kufanya mazoezi jana.

"Nitaangalia namna nitakavyowaona [Yondani, Metacha, Fei Toto na Makame] hali zao, ila uwezekano wa kucheza labda waanzie benchi lakini si kuanza katika kikosi cha kwanza," alisema Mkwasa.

Hata hivyo, Mkwasa alisema ametumia vizuri muda wa mapumziko kwa kuwapa wachezaji wake mbinu mpya kwa ajili ya Ligi Kuu na kwamba kwa sasa wachezaji wote wana morali nzuri ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo wa leo.

"Nashukuru kikosi changu kipo vizuri kila mchezaji ana morali ya ushindi kuelekea katika mchezo huo," alisema Mkwasa huku akiwataka mashabiki wao kujitokeza kwa wingi uwanjani leo ili kuipa sapoti timu yao.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Abdallah Bahressa, alisema ataingia kwa tahadhari kubwa katika mchezo huo, kwa kuwa ni mchezo ambao utakuwa mgumu na wenye ushindani mkali.

Alisema anashukuru kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Simba kwa kuwa timu hiyo imewasaidia kubaini makosa yaliyopo kikosini mwake, ambayo ameyafanyia kazi.

"Makosa ambayo niliyabaini tulipokutana na Simba na kufungwa bao 1-0, tayari nimeyafanyia kazi na kila mchezaji ana shauku ya ushindi,"alisema Bakhressa.

Yanga iliyopo nafasi ya 15 na pointi zake 10 wakati huu ikiwa imecheza mechi tano, inashuka dimbani leo kuivaa JKT Tanzania inayoshika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 15 baada ya kucheza mechi 10.

## Samatta afurahia kupondwa Stars

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wadau na wachambuzi mbalimbali wa soka nchini wakiponda na kueleza kutofurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, mshambuliaji huyo amefurahia namna wanavyomkosoa huku akieleza kwake anachukulia kama changamoto ya kufanya vizuri.

Katika michezo miwili ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Cameroon 2021, Samatta aliyeichezea Taifa Stars, wakati ikishinda 2-1 Uwanja wa Taifa dhidi ya Equatorial Guinea na ule wa nchini Tunisi wakipokea kipigo kama hicho kutoka kwa Libya, hakuonyesha ubora wake kama ambavyo amekuwa akiichezea klabu yake ya KRC Genk ya Ubelgiji, jambo ambalo wadau wa soka wamejiuliza maswali mengi.

Miongoni mwa wadau wa soka walionukuliwa wakitoa maoni yao ni pamoja na Kocha wa zamani wa Simba, Jamhuri Kihwelo 'Julio' ambaye amemtaka Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mrundi, Etienne Ndayiragije, kutoona aibu ya kumuanzisha benchi Samatta.

"Inabidi Ndayiragije asione aibu kumuanzisha Samatta benchi ili ausome vizuri mchezo, unaona kama mechi ya juzi alicheza lakini mechi ilikuwa imemkataa kabisa," alisema Julio.

Hata hivyo, wapo waliomtetea Samatta wakisema, anakabwa na mabeki kuanzia wawili hadi watatu, hivyo wachezaji wenzake wa Stars ndio wanaopaswa kutumia mwanya huo kufunga mabao.

"Kwanza tazama, Samatta anavyokabwa na wenzake kubaki huru, lakini pia nani anayemchezesha kama ambavyo anakuwa akichezeshwa na wenzake pale Genk? Pia tukumbuke kuna siku mchezo unamkataa mchezaji na si suala kwamba anaogopa kuumia," alisema Ally Majaliwa mkazi wa Mwenge jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Samatta kupitia akaunti yake ya Twitter @Samagol77, aliandika: "Nimepata meseji na Comment [maoni] kutoka kwa watu kadhaa kuwa hawajaelewa kiwango nilichoonesha katika mechi za timu ya taifa, 'anyway' ukweli nimefurahi kuona watu wanasema ukweli sichukii binafsi, bali nachukulia kama chachu itakayonifanya nijitume zaidi ili niweze [kuwa] bora zaidi. HAINA KUFELI."


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >